**15 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 15 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika: (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha *(Monetary Policy statement)* kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 638

### Hitaji la watumishi wa afya – Mbinga

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa sekta ya afya kufikia asilimia 50 ya mahitaji katika Halmashauri ya Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji makubwa ya watumishi wa afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yaliyosababishwa na maboresho ya miundombinu yaliyofanyika katika ngazi ya afya ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilipata kibali cha ajira na kuajiri watumishi wa kada ya afya 12,653 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imepangiwa watumishi 68.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kada ya afya kadri Bajeti ya Serikali itavyo ruhusu

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwanza niishukuru Serikali kwa kutoa watumishi hao 68. Lakini sasa kutokana na ongezeko hili kubwa la ujenzi wa vituo vya afya, ambapo tuna vituo viwili tayari vimekamilika, Kituo Cha Afya cha Mkumbi na Kituo cha Afya Matili, pamoja na ongezeko hili havijapata watumishi;

Je, ni nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu uliopo Serikali iko tayari kuipa kipaumbele halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kutokana na upungufu Mkubwa uliopo wa watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali mawili ya myongeza ya Mheshimiwa Benaya Kapinga. Kwanza hili la vituo viwili vya afya ambavyo vimejengwa na havijapata watumishi, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuweza kufika katika vituo hivi viwili vya afya ambavyo amevitaja Mheshimiwa Kapinga na kufanya tathimini yake na kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukafanya msawazo wa watumishi ndani ya Mkoa wa Ruvuma walau kuanza kupeleka watumishi wachache ili waanze kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, Serikali itaweka kipaumbele cha kupeleka watumishi kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo kule Mbinga Vijijini kwa Mheshimiwa Kapinga. Na Kadri tutakavyoendelea kluajiri basi tutaweka kipanumbele kwenye maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jimbo la Mbulu vijijini tumepata vituo vya Afya vitatu na tuna upungufu wa watumishi. Je, ni lini mnatuletea watumishi hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Massay, hivi sasa Serikali imetoka kuajiri watumishi 8070 wa kada ya afya nchini kote katika mwaka huu wa fedha 2022/2023. Pia tumeweka kipaumbele katika maeneo yenye upungufu ikiwemo kule Jimboni Mbulu Vijijini. Hivyo, basi ni wajibu wao na Mkurugenzi kuhakikisha kwamba hawa watumishi watakaopelekwa katika halmashauri yao wapangiwe kwenye maeneo ambayo yana upungufu zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa sisi Namtumbo tuna vituo viwili vya afya ambavyo vimejengwa na viko mwishoni kabisa kukamilika;

Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuanza kutuletea vifaa tiba na watunishi ili iweze kuanza na majengo yale yasikae muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** Mheshimiwa Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Kapinga kwa kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, anapotembelea kule Mbinga vijijini basi afike kule Namtumbo kwa Mheshimiwa Vita Kawawa ili kufanya tathimini kwenye vituo hivi vya afya ambavyo amevitaja Mheshimiwa Kawawa na kuona ni namna gani Serikali inaweza ikapaleka watumishi pale. Vile vile katika mwaka huu wa fedha tunaouanza wa 2023/2024 kuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kote nchini. Hivyo basi, tutaona ni namna gani vituo hivyo vya Namtumbo vinapata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Mji wa Mafinga kutokana na sababu za kijiografia inahudumia zaidi ya halmashauri tano. Je, Serikali iko tayari kutufanyia upendeleo wa kipekee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba Serikali imeajiri watumishi 8,070 wa kada ya afya kote nchini na muda sio mrefu wametoka kuchukua barua zao katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kuweza kuripoti katika maeneo ya kazi waliyopangiwa ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Hivyo basi, ni imani yangu kuwa halmashauri hii imepata watumishi hawa wa kada ya afya. Ni wajibu wa Mkurugenzi kuwapangia kule kwenye upungufu ikiwemo katika hospitali ya wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Vituo vya Afya vya Mwang'aranga, Mwigumbi na Ukenyenge ni vituo ambavyo vina upungufu mkubwa sana wa watumishi;

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inapeleka watumishi kwenye vituo hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, katika Vituo hivi vya Afya vya Mwang'aranga, Mwigumbi na hicho kingine alichokitaja Mheshimiwa Butondo, muda sio mrefu Serikali imetoka kuajiri watumishi wa kad ya afya, hivyo tutakwenda kuangalia na kuona ni wangapi wamepangiwa kwenda katika Halmashauri ya Shinyanga *DC* na kuweza kuona ni

namna gani wanaweza wakapelekwa katika vituo vya afya alivyovitaja Mheshimiwa Butondo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 639

**Malipo ya posho za Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji kupitia Bajeti ya Serikali Kuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura Na. 290, kila Halmashauri inatakiwa kuweka utaratibu wa malipo ya posho kwa wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 222 kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa halmashauri zote nchini. Hivyo Ofisi ya Rais – TAMISEMI inahimiza halmashauri zote nchini kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya kukusanya na kutumia fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa posho ya Waheshimiwa Madiwani inayotumika hivi sasa ni shilingi 350,000 imekaa takribani miaka kumi sasa.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuongeza posho ya waheshimiwa Maadiwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa halmashauri nyingi nchini zinapata mapato madogo, ikiwemo halmashauri ya Mbulu, na kushindwa kulipa posho ya wenyeviti wa vijiji na mitaa;

Je, Serikali haioni kuwa ndio wakati muafaka wa kutazama jambo hili ili kila halmashauri nchini zitekeleze takwa hili la kikanuni kwa mujibu wa huduma wanazotoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issaay, kwanza kuhusu hili la posho kuwa zimekuwa ni za muda mrefu. Mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Serikali kuu ilichukua jukumu la kulipa posho hizi Madiwani moja kwa moja kutoka hazina, hivyo, kuwapunguzia mzigo mamlaka hizi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupunguza hilo, na kwa sababu ni jambo la kisheria na Mheshimiwa Issaay ni Mheshimiwa Diwani kwenye halmashauri yake ilitakiwa wakae ili zile fedha am,bazo wanafanya *saving* baada ya Serikali Kuu kuchukua la kulipa posho za Madiwani waone ni namna gani wanatenga kwa ajili ya wenyeviti wao wa vijiji na wenyeviti wao wa mitaa n.k.

Mheshimiwa Spika, pia, fedha nyingi zimekuwa zikipelekwa kutoka Serikali kuu. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka fedha nyingi kwenye miundombinu, afya na elimu. Hivyo, halmashauri nyingi zimepunguziwa ule mzigo

mkubwa. Ni wajibu wao kutenga na kuhakikisha wanalipa kama inavyosema Sheria ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia kujibu swali lake la kwanza la nyongeza, mwaka huu wa fedha tunaokwenda kuuanza wa 2023/2024 Serikali Kuu vile vile, imewapunguzia mzigo halmashauri zote nchini kwa kuanza kulipa zile stahiki za wakuu wa idara, na zitaanza kulipwa moja kwa moja na Serikali kuu. Hivyo, kuwaacha halmasahuri kuwa na uwezo wa mapato zaidi na kuweza kutenga fedha za kulipa wenyeviti hawa na madiwani vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, linalohusu mapato kuwa madogo. Halmashauri huanzishwa kwa mujibu wa sheria; na moja ya kigezo kikubwa cha uanzishwaji wa halmashauri au mamlaka za Serikali za mitaa ni uwezo wake wa kukusanya mapato. Vile vile, huwa wanaainisha vyanzo zaidi ya 30. Na kwa mujibu wa Sheria ile Na. 287 ya Mamlaka za Wilaya, 288 Mamlaka za Miji inaelezea wazi. Vile vile, Sheria ile ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Kifungu cha (6) (7) (8) na (9) inaelezea wazi namna ambavyo wanatakiwa kubanana kuweka mapato yao sawa.

Mheshimiwa Spika, ukisema kila kitu kichukulliwe na Serikali Kuu ina maana dhana nzima ya *D by D* inakuwa imeondoka.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 640

**Ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mulungu – Muhambwe**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mulungu Jimbo la Muhambwe.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 500 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kizazi. Aidha wananchi wa Kata ya Kizazi wamejenga jengo la *OPD* hadi kufikia hatua ya lenta.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Kituo cha Afya katika Kata ya Mulungu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante. Nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu yake nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Katika Wilaya ya Buhigwe Kata ya Mkatanga, wananchi wa Kijiji cha Kitambuka waliomba kujengewa kituo cha afya na ombi hilo walilitoa mbele ya Makamau wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, na tayari wanayo matofali.

Je, Serikali iko tayari kutoa pesa ili wananchi waweze kujengewa kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu *DC,* Kata ya Kagera Nkanda iko umbali mrefu sana kutoka yaliko Makao Mkauu ya Halmasahuri ya Kasulu *DC,* ambapo ni kilometa 77 kutoka Makao Makuu.

Je, Serikali iko tayari kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kagera Nkanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali yote mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Genzabuke. Kuhusu Kata hizi za Mkatanga pamoja na Kagera Nkanda nichukue nafasi hii kumwelekeza Mgamga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kuweza kutembelea katika Kata hizi na Kufanya tathimini ili kuona kama vigezo vile vya kuwa na vituo vya afya vinatimia. Kama vigezo vile vinatimia basi Mganga Mkuu awasilishe taarifa il;e katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Genzabuke amekuwa akifuatilia sana Kituo hiki cha Afya cha Kagera Nkanda muda mrefu na tutakaa nae kuona ni namna gani katika mwaka wa fedha ujao tunaweza tukatenga fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO k. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mahongole wana kituo cha afya;

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa kituo cha Afya Kata ya Mahongole?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itamalizia Kituo cha Afya cha Mahongore kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kituo cha Afya cha Ipogolo ni kati ya vituo vikongwe vya afya na vinahudumia zaidi ya wanawake 600 kwa mwezi lakini hakina *combined ward.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, swali lako.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Swali langu hakina *combined ward* kwa ajili ya wanawake...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, unataka Serikali ikwambie nini?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, je, Serikali onaweza kutusaidia kutujengea *combined ward* katika kituo hiki ili kupunguza msongamano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutatuma timu kwenda Halmasahuri ya Manispaa ya Iringa kwa ajili ya kufanya tathimini ya kituo hiki cha afya cha Ipogolo na kuona kama eneo linaruhusu kuweza kujenga maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameomba na kama inaruhusu tutaweka katika mipango yetu ya kutafuta fedha ili kuweza kujenga kituo hiki cha afya ambacho ni kongwe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye kata ya Salale Kijiji cha Nyamisati tuna shida kubwa sana ya kituo cha afya ukizingatia zahanati ya pale inahudumia wilaya mbili…

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha, uliza swali.

**MHE TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, je, lini Serikali mtatujengea kituo cha afya pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ina vigezo vyake vya kuanza kujenga vituo vya afya. Hivyo, basi tutauma timu kwa ajili ya kwenda kule katika Kijiji cha

Nyamiisati, kata ya Salale, Jimboni Kibiti kuweza kufanya tathimini na kuona kama vigezo vile vimefikiwa vya kuweza kujenga kituo hiki vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza;

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha Afya Kata ya Sawida wilaya ya Itilima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga kituo hicho cha afya baada ya kufanya tathimini ya kuona uhitaji ulioko pale lakini vile vile kadri ya upatikanaji wa fedha; na tutatenga katika bajeti za miaka ya fedha inayofuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami kwa nunipa swali la nyongeza. Kituo cha afya cha Misha katika kata 29 za Tabora kimekamilika lakini bado hakina vifaa vya Afya vya kutosha;

Je, ni lini serikali itapeleka vifaa hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya hiki Misha kipo pembezoni mwa Manispaa ya Tabora na tayari katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambao tunaenda kuumaliza Serikali ilikuwa imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika kituo hiki cha afya,

nitakaa na Mheshimiwa Mwakasaka ili tuweze kupitia hivi na kuona tunapeleka hivi vifaa tiba kwa haraka sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na kuona, maana yake Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya *compilation* ya ahadi zote za viongozi wetu Wakuu wa Nchi na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na kuona namna gani tutapata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hizi. Hivyo basi, nimtoe mashaka Mheshimiwa Kajege kwamba baada ya kukaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na kuona ni namna gani Serikali itapata fedha hizi, tutaanza ujenzi huu wa Hospitali hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kituo cha Afya Mtina kilitengewa milioni 250 katika bajeti tunayoendelea nayo ili kujenga jengo la akinamama na watoto. Je, ni lini pesa hiyo itaenda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nitakaa na Mheshimiwa Mpakate ili kuona katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 tunaoenda kuanza kutekeleza kama Kituo hiki cha Afya cha Mtina kimetengewa fedha na kama hakijatengewa fedha, basi tutaangalia ni namna gani tunaweza tukakiweka katika mipango ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Je, ni nini mpango wa Serikali wa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Likawage, Jimbo la Kilwa Kusini, kata ambayo iko mbali kutoka sehemu ambayo huduma ya afya inapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutatuma timu kwenda katika Kata ya Likawage kufanya tathmini na kuona kama vile vigezo vya idadi ya watu na kadhalika vimefikiwa eneo walilolitenga wao katika maeneo hayo na kama vigezo vile vimefikiwa, basi tutaweka katika mipango yetu ya kutafuta fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kujua tu, ni lini Serikali italeta vifaa tiba katika vituo vyetu vya afya na hospitali ya wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nitakaa na Mheshimiwa Sima kuweza kupitia katika fedha iliyokuwa imetengwa ya ununuzi wa vifaatiba kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kuona Halmashauri ya Manispaa ya Singida imetengewa kiasi gani na kama ilikuwa haijatengewa tutaangalia katika mwaka wa fedha huu tunaoenda kuanza kuutekeleza wa 2023/2024 ili tuweze kuona namna gani fedha hiyo inaenda kwa haraka kupata vifaa tiba hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 641

**Kuviwezesha Vikundi vya Wanawake vya Ufugaji – Tanga**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuviwezesha Vikundi vya Wanawake vya Ufugaji Mkoani Tanga ili viweze kuongeza tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamilu Zodo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 hadi mwezi Machi, Halmashauri za Mkoa wa Tanga zimetoa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.56. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi Bilioni 1.82 zimekopeshwa kwenye vikundi vya wanawake vinavyojishughulisha na biashara ndogondogo pamoja na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchanganuo huo hapo juu, vikundi vya Wanawake 102 vyenye wanufaika 875 vinavyojishughulisha na kazi za ufugaji wa mifugo ya aina mbalimbali vimekopeshwa kiasi cha Shilingi Milioni 575 na kuweza kutengeneza ajira zipatazo 253.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali toka robo ya tatu imesitisha kutoa mikopo hii ya asilimia 10 mpaka sasa na kwa

kuwa akina mama wanahangaika na mikopo ya kausha damu huko mitaani; je, ni lini sasa Serikali inakwenda kuanza kutoa mikopo hii ya asilimia 10?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilisitisha utoaji wa mikopo hii ili kufanya tathmini na mapitio ya namna ambavyo mikopo hii inatolewa na hili lilikuwa ni agizo la Kamati ya Kudumu ya Bunge lako tukufu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivi sasa timu ile imeshaundwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tayari wameanza kufanya kazi ya kufanya mapitio na vilevile ilikuwa ni malekezo yake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mapitio haya yanafanyika haraka ili fedha zile nyingi zisipotee pale mikopo inapotolewa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu tunaelekea mwisho pengine mngetoa maelekezo zile pesa sasa ziendelee kuwekwa au zitumike kwenye maeneo mengine mpaka huo utaratibu utakapokuja, yaani zinaendelea kutunzwa au zinatumika kwenye maeneo mengine? *(Makofi)*

Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, tayari tumeshatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri. Kwa mujibu wa kifungu au Kanuni ya 24(2) ya kanuni za utoaji wa mikopo hii, tayari kila Halmashauri ina akaunti mahususi kabisa ya mikopo hii na tumewaelekeza hakuna kusimama katika kupeleka asilimia 10. Kwa hiyo hela zitapelekwa na pili utaratibu mpya utakapotangazwa, basi tutakuwa tuna hela tayari kwa ajili ya kupeleka kwenye huo utoaji wa mikopo.

Kwa hiyo, hawatakiwi kusimama, wanatakiwa kuendelea kuzitenga katika akaunti za mikopo. Kilichosimama tu ni ule utoaji kwenda katika vikundi vya wanufaika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Raymond, swali nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali sasa itapeleka vifaranga bora vya mbuzi, kuku na ng'ombe ili kuboresha mikopo hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuweza kuona ni namna gani tunapata mbegu bora kwa ajili ya kupeleka kwenye vikundi hivi ili waweze kufanya ufugaji ambao una tija na ambao utawaongezea kipato vilevile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali itazingatia kuongeza umri wa vijana kutoka ile miaka ya awali 30 mpaka kufikia 45 kama tulivyopendekeza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**AIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, umri ule wa vijana uliowekwa pale ni kwa mujibu wa miongozo ya kimataifa ambayo inataja umri wa vijana ni upi. Kwa hiyo sisi tunaendana na *convention* zile za kimataifa na mikataba ya kimataifa. Kwa hiyo umri wa vijana utabaki vilevile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumeona changamoto kubwa kwenye suala zima la mikopo; je, Serikali iko tayari sasa kubadili mfumo wa mikopo badala ya kutoa fedha kwenda kuwapa huduma kama ni ufugaji wa kuku, Serikali ikaamua kuwanunulia kuku ikawapatia

wana kikundi badala ya kuwapa fedha ambazo haziendi kutimiza malengo ya ule mkopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo yale ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kufanya mapitio ya utoaji wa mikopo hii ya asilimia kumi na maelekezo ya Kamati yako ya Bunge ya TAMISEMI, hivi ni vitu ambavyo vinaenda kuangaliwa na timu ile ambayo ameiteua Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na . 462

**Tatizo la magugu maji - Ziwa Victoria**

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kuondoa magugu ambayo yanasababisha uchafuzi katika Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali wa Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti magugu maji yasiendelee kuleta athari katika Ziwa Victoria, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kutekeleza Mradi wa Hifadhi ya Mazingira katika Ziwa Victoria *(Lake Victoria Environmental Management Project)* ambao pamoja na mambo mengine ulitekeleza shughuli zilizolenga kudhibiti magugu maji kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo za kibaiolojia;

(ii) Kutoa elimu na kuwajengea uwezo wananchi wanaoishi karibu na Ziwa namna ya kujitolea katika kazi za kutokomeza na kuenea kwa magugu maji kila yanapojitokeza Ziwani; na

(iii) Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa na inatekeleza Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kukabiliana na Viumbe Vamizi wa mwaka 2019-2029 ambao unatoa mwongozo wa namna ya kuzuia kuingia na kuenea kwa viumbe vamizi na pia una mipango endelevu ya kushughulikia viumbe vamizi waliopo na wale wale wanaoweza kuingia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi hizi za kupambana na magugu maji katika Ziwa Victoria ili kudhibiti uhabirifu wa mazingira na athari zitokanazo na uharibifu huo nchini, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA;** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Serikali imeshaandaa mkakati maalum wa kukabiliana na changamoto ya viumbe vamizi. Je, ni lini mkakati huu utaanza kufanya kazi rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shitobela kuwa mkakati huu umeshaanza kufanya kazi na umeshaanza kufanya kazi takribani karibu miaka miwili nyuma iliyopita. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta kama vile Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo lakini pia Wizara ya Mifugo na sisi Mazingira tumekuwa tukishirikiana kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunashirikiana kwa ajili ya kutoa elimu na takribani vikundi 40 tumeshavipa taaluma namna bora ya kutumia ziwa hili na kupunguza huu ueneaji wa haya magugu maji.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kutafuta fedha, lengo na madhumuni ikiwa ni kuhakikisha kwamba, tunapambana na hili jambo kwa sababu ni jambo ambalo Ziwa Victoria limeingiza nchi tatu au nchi nyingine.

Kwa hiyo, sisi huku tukiyakata kwa wenzetu yanaendelea kumea, kwa hiyo na mwisho wa siku yanarudi tena kwetu, lakini hata hivyo tunaendelea kupambana changamoto hii, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata nafasi hii. Ziwa jipya lililoko Wilayani kwangu Mwanga mpakani na Kenya, upande wa Tanzania unakaribia kupotea kabisa kwa ajili ya magugu maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi yake ya kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali hii ni kuhakikisha kwamba tunaondosha changamoto zote zinazogusa kwenye eneo la mazingira ikiwemo changamoto ya kuenea kwa magugu

maji. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kuzitafuta fedha kokote ziliko ili kuhakikisha kwamba tunaondoa magugu maji katika maeneo yote. Pia nimwambie kwamba siyo hili tu, yapo maziwa mengi yana changamoto hii. Hivyo, nimwambie tu kwamba hata katika Ziwa Jipe tutahakikisha tunakwenda kuondosha kabisa changamoto ya magugu maji, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona; je, Serikali ina mpango gani wa kuokoa Ziwa Basutu ambalo kwa sasa linaonekana limejaa mchanga na kusababisha maji kusambaa kwenda kwenye makazi ya watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ziwa hili limekuwa lina changamoto kubwa ya kuingia kwa mchanga ambao sasa unakwenda kuleta athari kubwa ya kimazingira. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tumeshashirikiana na wenzetu wa halmashauri na baadhi ya taasisi nyingine kama ambavyo nimeanza kujibu awali, kuhakikisha kwamba kwanza tunaendelea kuwapa elimu wananchi, kwa sababu tuligundua kwamba changamoto hii ya uingiaji wa mchanga na hayo masuala ya magugu maji, mengi tukiwatizama changamoto za kimazingira zinasababishwa na wananchi wenyewe hasa kwenye shughuli zao za kibinadamu za kawaida. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, awe na subra Serikali inakwenda kushughulikia hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felix Kavejuru.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na mimea vamizi nchi kavu na majini ikiwa Dodoma tayari tuna mmea vamizi ambao unaitwa Kongwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, moja miongoni mwa changamoto siziiti mpya, lakini miongoni mwa changamoto za kimazingira ambazo tuko nazo sasa hivi ni changamoto ya kuvamiwa na viumbe vamizi ikiwemo mimea na wadudu. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili tumeliona na tumeshaanza kulifanyia utafiti kwa sababu tumegundua kuna baadhi ya mimea mingine ni vamizi lakini haina athari kimazingira. Kwa hiyo, kwa hii ambayo ni vamizi na ina athari kimazingira tutahakikisha kwamba tunakwenda kulishughulikia na tutalifanyia kazi katika mikoa yote kwa sababu siyo Dodoma tu hata mikoa mingine tumegundua ipo hiyo changamoto. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kumbe ni makofi ya ninii. Mheshimiwa Stella Manyanya nadhani una swali hili linalofuata sasa naona umesimama, unataka la nyongeza kwenye hili?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, naomba swali lake namba 643 lipatiwe majibu.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa sijaingia kwenye swali lingine bado. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa suala la magugu maji limekuwa ni tatizo kubwa, ni kwa nini Serikali isifanye utafiti kuona kama kuna eneo ambalo magugu maji haya yanayotumika kama *raw material* ili yaweze kuvunwa kirahisi zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelishauri ni jambo jema na kwa sababu tumegundua kwamba hata nchi jirani wameshaanza hivyo na ndio maana unakuta changamoto ya kuenea kwa magugu maji inakuwa kubwa sababu sisi tukiyatoa, kwa wenzetu yanakuwepo na kwa sababu Ziwa ni moja yanarudi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Uganda wameshaanza kulifanyia hilo, wanatengeneza mikeka na mambo mengine na sisi tumo kwenye kufanya utafiti, nini ambacho tunaweza tukatengeneza. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha na sisi tunatumia magugu maji kama *raw material* kwa ajili ya kuinua vipato vya wananchi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

Na. 643

**Mabadiliko ya tabianchi na usalama wa viumbe hai**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K.n.y. MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa tishio kwa usalama wa viumbe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge Wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa sera, mikakati na mipango ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo inatoa elimu na namna bora ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wadau wote muhimu wakiwemo wananchi katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanahamasishwa kuacha shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira na kusababisha athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwemo kukata miti ovyo, kuepuka kilimo kisichoendelevu katika vyanzo vya maji, kuepuka ufugaji unaoharibu mazingira pamoja na uvuvi haramu. Vilevile, Serikali inachukua hatua kwa kuanzisha na kutekeleza miradi ya kuzuia madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inaendelea kusimamia sera, mipango na mikakati ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (www.vpo.go.tz )

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Jacqueline ana maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwenye nishati mbadala ikiwemo majiko ya gesi pamoja na gesi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa maeneo yanayochimbwa madini kama makaa ya mawe pamoja na mchanga yanafukiwa au kurejeshwa katika hali yake ya asili kwa wakati na inavyostahili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishiriki kwenye mjadala mmoja muhimu sana wa kitaifa ambao ulikuwa unazungumzia masuala ya kupunguza nishati ya matumizi ya kuni. Katika mjadala ule kuna maelekezo yalitoka tulipewa sisi Wizara tunaohusika na masuala ya mazingira na Wizara nyingine:-

(i) Tuendeleze kutoa elimu kwa wananachi;

(ii) Tunatakiwa tusimamie sheria, zipo Sheria za Mazingira; na

(iii) Tunatakiwa tuhamasishe wananchi wapande miti kwa wingi ili tuirejeshe miti ambayo ilishakatwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo alilolishauri la kuhakikisha kwamba tunaweka ruzuku kwenye matumizi haya ya nishati hasa gesi na nishati nyingine, tutalichukua tunakwenda kulifanya kazi kuona namna ambavyo tunakwenda kuhamasisha zaidi wananchi katika masuala ya kutumia nishati bora ya kupikia *instead of* kutumia kuni.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tayari tulishatoa maelekeza kwa wachimbaji wote wa madini au wachimbaji wote wa makaa ya mawe kuhakikisha kwamba mashimo wanayoyabakisha baada ya kuchimba wayafukie. Pia tulishatoa maelekezo kwa Mameneja wetu wote wa *NEMC* wahakikishe kwamba wanawapa taaluma na taaluma wameshapewa wachimbaji wote wa makaa ya mawe ili kuweza kuepuka athari kubwa ya mazingira ambayo inaweza ikajitokeza hapo mbele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanasababisha mvua kunyesha pasipo utaratibu na mafuriko pia. Je, Serikali imejipanga vipi katika kukabiliana na hali hiyo ya njaa pamoja na mfumuko wa bei katika nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi hilo swali lako hapo mwishoni hebu litengeneze lirudi kwenye hoja yako kwa sababu mfumuko wa bei sasa utaelekea Wizara nyingine.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi yanaathiri sana wakulima pamoja na makazi ya watu. Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na hali hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika …

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri yote yaliyopita, lakini swali la Mama Mariam Kisangi ni swali la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Idara ya Hali ya Hewa wanatuambia hivi sasa kiwango cha mvua maeneo mengine kimeshuka. Inaonesha wastani wa mita 1,500 sasa imefika mpaka mita 750, lakini tunakumbuka hivi karibuni tumekumbana na changamoto kubwa sana ya ukame katika Mikoa mbalimbali hasa Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara. Katika hili ndiyo maana Serikali tumejielekeza kuelekeza suala zima la utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 238(L) kinachosema kwamba kila Halmashauri ipande miti milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge hawa na Watanzania na wadau wengine hatuna jinsi yoyote ya

kupambana na hali hii, ni lazima tupande miti kwa kiwango kikubwa sana. Ninawaomba Watanzania wote tushirikiane na Serikali katika kulinda mazingira kupambana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Afya, Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 644

**Bima ya Afya kwa wanafunzi wa shule na vyuo**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwasajili wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati kwenye utaratibu wa Bima ya *NHIF*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imeanzisha mpango wa bima ya afya kwa wanafunzi wa ngazi zote kwa kuchangia shilingi 50,400 kwa mwaka ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za matibabu wakiwa masomoni, likizo na wakati wa mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2023 mfuko umeshasajili jumla ya wanafunzi 342,933 ikiwemo wa Shule za

Msingi, Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu. Zoezi hili la kusajili wanafunzi ni endelevu kupitia shule na vyuo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi hili ni endelevu, je, Serikali imejipangaje sasa kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao hawajasajiliwa wanasajiliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pili; kwa kuwa utekelezaji wa zoezi hili si kwa takwa ama kwa mujibu wa sheria. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba sheria hii inawekwa kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanasajiliwa katika Bima ya Afya? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni nini tutafanya ili kusajili wanafunzi wengi zaidi, kikubwa ni kuendelea kuhamasishana kuwaomba wakuu wa shule na wazazi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu wote kwa pamoja tuone umuhimu wa watoto wetu kuwa na bima ya afya kwa sababu ugonjwa hauji kwa kusema, ugonjwa unakuja kwa ghafla na vizuri kujipanga wakati wote, hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mpango gani, kwa sababu hili suala haliko kisheria, tunafanya nini. Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ndiyo maana Serikali ilikuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ili kulifanya hili jambo liwe sasa la kisheria. Kikubwa ambacho nawomba Watanzania, nawaomba ninyi Wabunge tuendelee kuelewa na kupigana kwa pamoja kuhakikisha Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote unarudi hapa ili

tuweze kufanya hili suala la kisheria kwa sababu masuala ya afya ni muhimu na afya ni uchumi wa nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 645

**Chanzo cha ugonjwa wa manjano kwa watoto wachanga**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, nini chanzo cha ugonjwa wa manjano kwa watoto wachanga?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tafiti nyingi zimefanyika Kitaifa na Kimataifa kujua chanzo cha watoto wachanga kugeuka njano mara baada ya kuzaliwa. Tafiti hizo zimeonesha kuwa hali ya umanjano hutokea ndani ya masaa 24 baada ya kuzaliwa inaonyesha tatizo la kiafya na linahitaji kutambua sababu na kutoa tiba stahiki.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili likitokea baada ya masaa 24, mara nyingi linatokana na sababu za kawaida za mwili wa mtoto kupunguza chembechembe nyekundu nyingi alizokuwa nazo tumboni kwa mama, hata hivyo hili pia uchunguzi wa kina ni muhimu ili kujihakikishia.

Mheshimiwa Spika, suala la utafiti ni muhimu na ni suala endelevu katika tiba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa kwenye jibu la msingi Waziri ametuambia chanzo ni upungufu wa chembechembe nyekundu kwenye mwili wa mtoto. Sasa je, tunamshauri nini mama mjamzito ili kuondokana na tatizo hili? *(Makofi)*

Swali langu la pili; mtoto akishazaliwa na akagundulika ana tatizo hili la manjano, wataalam wetu huwashauri wazazi kuwaanika watoto juani. Ni, lini tiba ya ugonjwa huu itapatikana ili kuondokana na changamoto kubwa ya wazazi wanaokumbana na ugonjwa huu wa manjano, baadhi wanapoteza maisha na hatimaye kupunguza nguvu kazi ya Taifa letu? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Swali lake la kwanza anasema kwamba tumesema chanzo ni upungufu, siyo upungufu, wakati mwingine watoto wanapokuwa wamezaliwa halafu wanakuwa na chembechembe nyingi za damu ambazo alitoka nazo tumboni zinapokuwa zinasafishwa kunakuwepo sasa na *bilirubin* ambayo inasababisha hiyo hali ya umanjano kwamba sasa hicho ndiyo kinachotokea. Wakati mwingine kwa sababu ini la mtoto anapozaliwa ndani ya siku 14 anakuwa bado ini lake halijakua vya kutosha, kwa hiyo, uwezo wa kubadilisha ile kitu kinachosabisha umanjano haina uwezo wa kutosha ndiyo maana unaona huo umanjano, kwa hiyo, ni kitu cha kawaida. Ikitokea kama tulivyosema ndani ya masaa 24 basi ni tatizo tunalifuatilia na kujua. Hata hivyo ikitokea baada ya masaa 24 ni muhimu vilevile wataalam kumuangalia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni suala la kwamba watoto wanaanikwa juani. Nimuambie tu Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshafanya *revolution* kubwa sana, ndiyo maana umeona trilioni 1.3 imefanya mabadiliko makubwa sana ya tiba ya afya. Leo unaona vifaa vingi sana

vimesambazwa kwenye maeneo yetu na vituo vyetu vya afya, utaona kuna vifaa maalum vya kuwaweka watoto ambavyo vinatoa mionzi maalum kwa ajili ya kuondoa hilo tatizo. Kwa hiyo, watoto wetu kwa *revolution* aliyoifanya Dkt. Samia Suluhu Hassan mpaka kwenye vituo vyetu na zahanati sasa vifaatiba vinaenda kununuliwa na hili tatizo litaondoka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ninaomba kuuliza, je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa *rheumatic heart disease* ambao unaonekana unaongezeka kwa kasi kubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho naweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge moja ni elimu, watu kuangalia afya zao kila wakati na kupata tiba stahiki mapema, ndiyo maana unaona leo, hata Taasisi yetu ya Jakaya Kikwete keshokutwa inakwenda Pemba kwenda kabisa kule vijijini kuhakikisha watu wanafanyiwa uchunguzi na kuhakikisha haya matatizo yanagundulika mapema na watu kupata tiba stahiki mapema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa.

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia wagonjwa wanaohitaji viungo bandia kama vile miguu bandia, kwani gharama zake ziko juu sana kwa mgonjwa wa kawaida. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, alichokisema Mheshimiwa Ndakidemi ni kweli na kuna tatizo hilo na ndiyo maana bado tulikuwa tunasisitiza, mwarobaini wa tatizo hili la uwezo wa kulipia tiba ni Bima ya Afya kwa wote hilo ndiyo la

kwanza. Kumekuwepo na utaratibu wa Serikali kusaida Watanzania wasiojiweza, wale ambao watathibitika hawana uwezo wa kujilipia basi kuna utaratibu unakwenda kwa Mtendaji wako wa Kata anaandika barua na kuna *social welfare* kwenye hospitali zetu wanazipitia basi anapata *exemption* anaweza kuhudumiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, sasa aulize swali lake.

Na. 646

**Tamko kwa mabasi yasiyoingia stendi**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa mabasi yasiyoingia stendi na ambayo hushusha abiria nje ya stendi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabasi yote ya masafa marefu hupangiwa ratiba na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)* ambazo huonyesha stendi za kupakia na kushusha abiria pamoja na muda wa kusimama kwenye stendi hizo. Aidha, mabasi ya masafa marefu yamepangiwa kusimama katika stendi moja tu kwa kila Mkoa isipokuwa pale ambapo basi hilo lina abiria anayeshuka katika stendi ya Wilaya. Utaratibu huo umepangwa ili kuondoa usumbufu na ucheleweshaji wa abiria wa masafa

marefu kwa kuwalazimisha kuingia kwenye stendi hata kama hawana abiria wa kupanda au kushuka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Ngassa anatoka Igunga, naomba kumtaarifu kuwa, Stendi ya Igunga haimo kwenye stendi ambazo mabasi ya masafa marefu hulazimika kuingia ama kusimama isipokuwa kama yana abiria wa kupanda au kushuka kwenye stendi hiyo. Hata hivyo, stendi hiyo hutumika kwa magari yote yanayotoa huduma ndani ya Mkoa wa Tabora na Mikoa jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa madereva wanaokaidi kuingia stendi na kushushia abiria nje ya stendi hususan barabarani, madereva hao wanakiuka maelekezo ya Kifungu cha 50(1) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 kinachomzuia mtu yeyote kuegesha au kusimamisha gari barabarani bila kujali watumiaji wengine wa barabara, hivyo, huvunja Sheria. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Anachokieleza Naibu Waziri uhalisia kule si kweli kwa sababu mabasi yanayotoka masafa marefu unakuta yana abiria lakini yanasingizia hayana abiria matokeo yake yanawaacha wananchi juu kwa juu. Kwa mfano, pale Igunga maeneo ya mnadani wananchi wanafika wanashushwa tu wanaachwa wanaanza kuhangaika kutafuta bajaji na bodaboda kurudi Mjini.

Je, ipi ni kauli ya Serikali katika hili ili kuepusha adha kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, moja ya mwongozo wa Serikali ni kuhakikisha Halmashauri zetu zinakusanya mapato na Halmashauri nyingi vyanzo vyetu vya mapato ni pamoja na hizi stendi za mabasi lakini mabasi yanatumia kigezo cha kusema hawana abiria lengo wasiingie Halmashauri ili tusipate mapato. Pia naomba kauli ya Serikali katika hili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kujibu kwenye jibu langu la msingi kwamba Sheria ya Usalama Barabarani, lakini pamoja na wadau, tulikaa na wadau mwaka jana tarehe 24, Mwezi wa Nne 2022, wadau wote wa usafirishaji, tulikubaliana kwamba ili kupunguza gharama kwa abiria ni pamoja na mabasi haya ambayo hayana abiria wa kushusha ndani wala hakuna anayepakia yasiingie ili kupunguza muda wa mabasi hayo kwenda kwa sababu wanasafiri umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kama kuna basi lolote ambalo limeshusha abiria njiani na wakati eneo hilo kuna kituo cha mabasi kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Kifungu cha 50 (1) na Sura ya 168 kimeelekeza wazi kwamba dereva huo lazima achukuliwe hatua za kisheria. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na jeshi la polisi tutaendelea kusimamia jambo hili ili mabasi haya yafuate utaratibu huu kama ambavyo tulikubaliana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu suala la mapato katika Halmashauri zetu hususan katika vituo hivyi vya mabasi, ni kwamba siyo kila basi kama nilivyokwisha kusema litaingia kwenye kituo, lakini kwa mabasi yale ambayo yataingia kwa masafa mafupi yana wajibu wa kulipa ushuru katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ninataka kufahamu Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi mpya ya mabasi Bukoba Mjini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa stendi katika Mkoa wa Kagera, Bukoba tutawasilina na wenzetu TAMISEMI ambao wanasimamia jambo hili na naamini katika bajeti yao mwaka huu huenda wamepanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 647

**Kuondoa nauli za kwenye vivuko kwa watu wenye ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, Serikali inaonaje ikapunguza au kuondoa nauli kwenye vivuko vyote nchini kwa watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwepo na Watu Wenye Ulemavu wa aina mbalimbali ambao wanatumia huduma za vivuko kote Nchini. Aidha, suala la kupunguza au kutolipa nauli kwenye vivuko halijatamkwa kwenye Sheria ya Leseni za Usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, suala la kupunguza au kuondoa nauli limekuwa likifanyika kwa Watu Wenye Ulemavu

waliopo kwenye mazingira hatarishi katika vyombo mbalimbali ikiwemo usafiri wa vivuko. Hii imefanyika kupitia ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu utaratibu huu wa kupunguza au kuondoa nauli kwa Watu Wenye Ulemavu au wenye mahitaji maalum. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa uhalisia hawa Maafisa Ustawi wanakua hawapo kwenye hivi vivuko wakati watu hawa wanatumia huduma hii. Nini kauli ya Serikali kwa vivuko vyote nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili halijatamkwa wazi kwenye Sheria ya Leseni za Usafirishaji Nchini. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba suala hili linatamkwa wazi kwenye Sheria hii ya Leseni za Usafirishaji Nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kweli kwamba hatuwaweki watu wa ustawi wa jamii kwenye vivuko lakini tunachotaka wafanye ni kwamba waende kwenye ofisi za Wakuu wa Wilaya pamoja na ofisi za ustawi wa jamii ambapo wanapewa barua ama vibali kwamba waweze kusaidiwa kwa sababu hawana uwezo hivyo waweze kuvuka kwenye vivuko ama kutumia kwenye vivuko kwa kupunguziwa ama bila kulipa, ndiyo maana tumesema Waheshimiwa Wabunge waendelee pamoja na Wakuu wa Wilaya na watu wa ustawi kuwafahamisha watu wenye ulemavu ama mahitaji maalum kwenda kabla hajaanza safari basi apate kile kibali ama

barua ambayo atakapofika kwenye kivuko husika hatabughudhiwa na hilo limekuwa likifanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutamka kisheria, kulipa ama kutolipa kwa watu wenye ulemavu linategemea na uwezo. Watu Wenye Ulemavu, kuna ulemavu wa aina mbalimbali, wako wenye ulemavu ambao kimsingi wana uwezo nadhani hapa tunachoongela kupunguza ama kutolipa ni wale kabisa ambao wamethibitika hawana uwezo na ndiyo maana pengine wanatakiwa waende kwenye ofisi husika ambao watasema kweli huyu hana uwezo kwa hiyo hastahili kulipa, lakini wale wenye uwezo nadhana ndiyo maana sheria haikutungwa ili waweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama kutakuwa na umuhimu nadhani tunazo sekta mbalimbali ambazo zinashughulikia hawa Watu Wenye Ulemavu labda sasa litachukuliwa na Serikali liangaliwe kama kuna haja ya kulitungia sheria. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Licha ya *LATRA* kutoa mapendekezo ya nauli kutoka Njombe kwenda Makete, ni takribani mwaka mzima sasa barabara imepanda kiwango cha lami lakini nauli haijashuka: Ni ipi kauli ya Serikali nauli iweze kushuka ili wananchi wa Makete wapate unafuu wa kusafiri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali hilo inabidi lije kama swali la msingi ili lipate majibu mahususi. Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa watu wenye ulemavu kwanza kwa idadi siyo wengi, lakini wengi wao hupata changamoto hata ya kuwa na kipato: Ni kwa nini kusiwepo na tamko dhahiri kwamba kila mwenye ulemavu *at least* unaoonekana aweze kuvuka bure kwenye vivuko ili kuwapunguzia adha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, nimesema watu wenye ulemavu wanatofautiana kwa kiasi kikubwa sana, na wapo watu wenye ulemavu ambao wana uwezo pengine kukuzidi hata wewe Mheshimiwa Mbunge. Sasa ukisema tu mtu mwenye ulemavu yeyote asilipe, nadhani pia tutakuwa hatuwatendei haki. Tumesema watu wenye ulemavu ambao kweli vyombo vinaweza vikatambua huyu hana uwezo kwa kweli, hao wanatakiwa wasaidiwe, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake.

Na. 648

**Ujenzi wa barabara ya Mlowo – Utambalila – Kamsamba**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami kwa Barabara ya Mlowo - Utambili hadi Kamsamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami mwaka 2020. Aidha, Serikali imeanza kuijenga kwa awamu barabara hii ambapo imekamilisha ujenzi wa Daraja la Momba lenye urefu wa mita 80 na barabara za maingilio zenye urefu wa mita 950.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha ujao wa 2023/2024 barabara hii imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali, imesikia kilio cha wananchi wa Mbozi na Momba kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

Swali langu la kwanza; je, ni kilomita ngapi sasa Serikali itaanza kwa awamu hii?

Mheshimiwa Spika, pili; je, ni lini mchakato wa kumpata mkandarasi utaanza ili ujenzi uanze? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 147 kwa mwaka ujao wa fedha tumepanga kuanza kuijenga kilometa 50.

Swali lake la pili kuhusu ni lini tutaanza, barabara hii tutaanza kuijenga ama kutafuta mkandarasi tutakapoanza utekelezaji wa bajeti wa 2023/2024, na ndipo tutakapoanza kutekeleza mpango huu wa kuanza kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hiyo. Kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuanza kusaini kesho barabara karibu nane kwa mfumo wa *EPC and F,* maana Bungeni hapa imezungumzwa muda mrefu kuhusu hilo suala; je, mara baada ya kutangaza habari ya kusaini hiyo

kesho, ni lini ujenzi utaanza kwa barabara hizo ikiwemo Mafinga – Mgololo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niseme, barabara ambazo tunategemea kutia sahihi ni barabara saba. Pengine tu nilijulishe Bunge hili kwamba kazi kubwa ambayo tulikuwa Mheshimiwa Rais anakwenda kuifanya ni kusaini mikataba ya hizi barabara zote saba ambazo tumeziongelea sana hapa za *EPC + F* na kazi hiyo itafanyika kesho hapa Dodoma Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu pengine Wabunge wengine hawajapata taarifa, tungetamani pia Wabunge wote ambao hizo barabara zinapita waweze kushuhudia kitu kikubwa ambacho kinafanyika kuanza kujenga hizo kilometa 2,035 kwa mpigo. Muda ungetosha ningeweza kuwakumbusha zile barabara lakini kwa sababu ya muda, ni hizo barabara zote saba ambazo kwa ruhusa yako labda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ni barabara ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Kilosa – Kwa Mpepo hadi Lumecha Namtumbo, nyingine ni barabara ya Igawa – Mbeya Mjini – Songwe hadi Tunduma, barabara ya Kongwa – Kibaya – Orkesumet – Rosinyai hadi Arusha, barabara ya kutoka Karatu - Mbulu – Hydom – Sibiti – Lalago hadi Maswa na mwisho ni barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 649

**Ujenzi wa barabara ya Galapo – Orkesumeti – Babati**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Babati Galapo hadi Orkesumeti kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *TANROADS,* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami mwezi Februari, 2023. Kwa sasa Serikali inaendelea na zoezi la kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaoathirika na mradi lililoanza tarehe 5 Juni, 2023 na inatarajiwa kukamilika tarehe 5 Julai, 2023. Baada ya zoezi la uthamini kukamilika na waathirika kulipwa fidia, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali iko tayari kutenga fedha katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni lini Serikali itasaini mkataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kilomita nane za barabara ya lami ya *Dareda Center* kwenda *Dareda Mission* ikiwa sehemu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hiyo kutoka Dareda kwenda Dongobesh? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ndiyo inayounganisha Makao Makuu ya Mji wa Manyara, Babati na Wilaya mbili ya Kiteto na Simanjiro. Kwa hiyo, ni wazi kama tulivyosema kwenye mpango wetu kwamba tutaziunganisha hizo barabara kwa kiwango cha lami, kwa hiyo, naamini kwa mwaka wa fedha utakaokuja, hizi barabara zitaingia kwenye mpango na ndiyo maana sasa hivi tunakamilisha usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Dareda – Dongobesh ambayo tutaijenga kwa kuanza na kilomita nane, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za manunuzi zimekamilika na tunategemea pengine kabla ya tarehe 22 kama taratibu zitakwenda kama tulivyopanga, mkandarasi awe ameonyeshwa *site* kuanza ujenzi wa hizo kilomita nane, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imefanya mapinduzi makubwa ya kutumia utaratibu wa *EPC + Financing* na kesho inasainisha mikataba saba hiyo; je, ipo tayari kuifikiria barabara ya Makofia – Mlandizi – Mzenga – Mwanarumango kwenye utaratibu huo siku za usoni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba hii barabara aliyoitaja tumekuwa tunaitengea bajeti na bado hatujakamilisha kulipa fidia hasa kwa kipande cha Makofia hadi Mlandizi, lakini mpango ni kuijenga hii barabara yote kwa kiwango cha lami. Sasa kama itaingia kwenye utaratibu wa kawaida ama utaratibu wa *EPC + F* itategemea na kipindi hicho ambapo sasa tutaanza kuijenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, wakati najibu barabara za *EPC* nilisahau pia kuwakumbusha watu wa kuanzia Handeni – Kiberashi – Kibaya – Kwamtoro hadi Singida, pia hiyo barabara itakuwepo kesho, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 650

**Mgogoro wa mpaka kati ya Pori la *Usumbwa Forest Reserve* na Hifadhi ya Pori la Kigosi Moyowosi**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka wa Pori la Usumbwa *Forest Reserve* na Hifadhi ya Pori la Kigosi Moyowosi – Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la *Usumbwa Forest Reserve* ambalo kwa sasa ni Hifadhi ya Taifa Kigosi, haina mgogoro wowote wa mpaka na wananchi wa Ushetu. Kwa sasa kilichopo, wananchi wa Ushetu waliwasilisha maombi ya kumegewa eneo ambapo Serikali inaendelea na tathmini na pindi itakapokamilika, wananchi watajulishwa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza naishukuru Serikali kwa kuendelea kushughulikia suala la kuwamegea wananchi maeneo. *Usumbwa Forest Reserve* ni ina *GN Number 442* ya mwaka 1958, wakati Kigosi Myowosi inapanda hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)*. Pori hili pia lenye hekta 36,000 lilichukuliwa kuingizwa huku na mipaka yote ikahamishwa kulimega hili pori lote ambalo ni la Halmashauri. Hawakushirikishwa wananchi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, natambua hili ni swali lako la msingi, lakini nalitazama hapa swali lako linahusu mgogoro wa mpaka wa Pori la *Usumbwa Forest Reserve* na Hifadhi ya Pori la Kigosi Myowosi. Hili swali unalouliza kuhusu *GN,* ni sehemu ya hili?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo…

**SPIKA:** Washa kisemeo.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, hili pori ambalo ni la hekta 36,000 ni *Usumbwa Forest Reserve* ambayo ina *GN Number* yake, lakini walipokuja kuweka mipaka ya kuipandisha Kigosi wakaweka nje ya Kigosi wakalichukua na hili pori kuliingiza Kigosi hata wananchi hawakushirikishwa na Madiwani hawakushirikishwa. Ndiyo maana namwomba sasa Mheshimiwa Waziri, kama wanaona wao hakuna mgogoro, waje sasa wapitie mipaka hiyo. Nimemtumia barua ambayo pia *RAS* ameiandika kwa ajili ya kuhakikisha mipaka hiyo inakuja kupitiwa upya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa nimekuelewa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mambo kama haya huko kwenye jamii yanaleta changamoto nyingi sana, ili swali lake liweze kutendewa haki, litajibiwa na Waziri au Naibu Waziri anayehusika na hii Sekta atakapokuwa hapa. Kwa sababu huyu amekuja kujibu kwa niaba. Sasa akiwekewa na mambo mengine inaweza ikawa kidogo tunamweka kwenye mazingira magumu.

Kwa hiyo, swali lako hili la msingi, siyo hilo ulilouliza, hili la msingi litarejea hapa Bungeni siku Waziri akiwepo na Naibu Waziri ili liweze kutendewa haki. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge mliokuwa mmesimama kwa ajili ya maswali ya nyongeza kwenye swali hili pia niliwaona, lakini sasa kwa sababu swali la msingi litakuja kujibiwa hapo baadaye akiwepo Waziri au Naibu Waziri, basi pengine mtapata nafasi wakati huo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutafute viti tuketi. Waheshimiwa Wabunge, mliosimama tutafute viti tuketi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, makofi ya muhimu sana hayo na sitasema sababu kwa sababu nilishaisema huko nyuma na watu hamkunielewa, sasa mtanielewa nilikuwa namaanisha nini. Nimeshafafanua hoja hiyo mara kadhaa, leo sitafafanua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni. Ninayo matangazo mawili hapa na hawa wageni tutakaoanza kuwatangaza ni wale walioko Jukwaa la Spika. Wageni tisa wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Viongozi wa Chama cha Walimu Wilaya ya Ruangwa wakiongozwa na Mwalimu Tabibu Kiwanga, Kaimu Mwenyekiti CWT Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Juma Othman Hija ambaye anatoka Zanzibar Mjini. Huyu aliyeandika hili tangazo sijui Zanzibar Mjini ndiyo sehemu gani, lakini ni Mbunge Mstaafu, Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao tukonao Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na

hawa ni Viongozi wa UVCCM, Tarafa ya Sadani kutoka Mufindi Kaskazini Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kutoka Zanzibar, Ndugu Juma Vuai Bakari; pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Aysharose Mattembe ambao ni watoto wake kutoka Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Haji Amour Haji ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Zanzibar Mjini Magharibi. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambao ni Viongozi wa Wadi ya Muyuni kutoka Zanzibar Kusini Unguja. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Daniel Sillo kutoka Babati Mkoa wa Manyara; na pia tunao wageni 80 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi na Madiwani kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndugu Yasinta Bura, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni watangazaji wa Redio *Sibuka FM* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Mussa Sima ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Singida Mjini. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben ambaye ni *Corporate Relations Director* kutoka *Serengeti Breweries,* Ndugu John Wanyancha. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ambao ni Wajumbe wa SMAUJATA kutoka Same, Mkoa wa Kilimanjaro; na pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zaytun

Swai kutoka *New Safari Hotel* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambaye ni mwasisi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Misenyi Kagera, huyu ni Mzee Abdu Mwanandege Nyembo. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa wa Mara CCM kutoka Musoma; na vile vile wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Jimbo la Kawe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambao ni walimu kutoka Shule ya Msingi Majengo, Tabora. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Samweli Hhayuma kutoka Hanang, Manyara. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hamida Abdallah ambaye ni mtoto wake kutoka Mtwara. Sijui amekaa upande gani? Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 42 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Anna ya Jijini Dar es Saalam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 111 na walimu 13 kutoka Shule ya Msingi Nyamata ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi wa Ofisi ya Bunge kwamba katika kuadhimisha miaka 60 ya kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Jeshi hilo

limeandaa mbio maalum zinazoitwa *JKT Marathon 2023* zitakazofanyika tarehe 25 Juni, 2023 katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. Aidha, Jeshi la Kujenga Taifa wapo viwanja vya Bunge nyuma ya jengo la Msekwa kwa ajili ya kuandikisha Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi watakaoshiriki mbio hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa kushiriki tukio hili la kihistoria kama mlivyoambiwa hapo awali kwamba JKT inatimiza miaka 60 kwa hiyo, uwe sehemu ya historia ya hiyo miaka 60 kwa sababu mpaka ije ifike 60 nyingine humu ndani sina uhakika sana wangapi watakuwa bado wamejaaliwa kuendelea kuwa wazee wa nchi hii. Kwa hiyo, ni muhimu sana kushiriki historia hii ya miaka 60. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa majina mengine ya wageni ambao wako hapa ambao hawakuja kwenye hili tangazo la mwanzo; tunao wageni na wao wako Jukwaa la Spika, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango; yupo Dkt. Natu El-Maamry Mwamba ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bi. Jenifa Omolo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Bi. Amina Shaaban ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana Emmanuel Tutuba ambaye ni Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Albina Chuwa ambaye ni Mtakwimu Mkuu wa Serikali karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Bwana Alphayo Kidata ambaye ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Frank Nyabundege ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Lilian Mbassy ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya *TIB,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana David Kafulila ambaye ni Kamishna wa *PPP* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Bwana Rished Bade ambaye ni Kamishna wa Fedha za Nje, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana Meshack Anyingisye ambaye ni Kamishna wa Bajeti, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana Elijah Mwandumbya - Kamishna wa Sera, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Bwana Godfrey Malekano ambaye ni Mtendaji Mkuu Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mwanyika Semroki ambaye ni Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali karibuni sana, sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyoada nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya hali ya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024 na taarifa zilizopo katika vitabu hivi ndio msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 nitakayowakilisha katika Bunge lako Tukufu leo alasiri.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana tena kwa mara nyingine katika Bunge hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nitoe pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti aliouonesha tangu alipoingia madarakani. Kupitia uongozi wake tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta mbalimbali ikijumuisha sekta za uzalishaji, huduma za jamii na miundombinu wezeshi. Aidha, Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuimarisha hali ya kisiasa hapa nchini na mahusiano ya kimataifa. Hakika nchi yetu imebarikiwa kuwa na Rais mwenye maono makubwa katika kuboresha ustawi na maendeleo ya nchi pamoja na watu wake. Hakika mama hana baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri na jitihada zao katika kuhakikisha wanamsaidia Mheshimiwa Rais na Taifa letu kupata maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na mhimili mzima wa utoaji wa haki kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha,

nipongeze vyombo vya ulinzi na usalama vinavyoongozwa na Mkuu wa Majeshi kwa kuendelea kusimamia ulinzi na usalama wa nchi yetu kuwezesha shughuli za maendeleo kuweza kumanyika kwa amani, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikupongeze wewe binafsi, na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa weledi mkubwa. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua kwa ushauri mahiri ambao wamekuwa wakiutoa katika kutengeneza taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi na weledi mkubwa ili kutimiza matarajio yake aliyonayo kwa wananchi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa Uchumi kwa Mwaka 2022. Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ya Aprili 2023 inaonesha kuwa, kasi ya ukuaji wa uchumi duniani itapungua kutoka asilimia 6.3 mwaka 2021 hadi asilimia 3.4 mwaka 2022. Upungufu huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi kutokana na madhara ya UVIKO-19; vita vya Ukraine na sera za kupunguza ukwasi katika chumi za Ulaya ili kukabiliana na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afrika na Kikanda, ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua kufikia wastani wa asilimia 3.9 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa upande wa Pato la Taifa

Mwaka 2022, thamani halisi ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi trilioni 141.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 135.5 mwaka 2021. Aidha, kiwango halisi cha ukuaji wa pato la Taifa ni asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.9 kwa mwaka 2021. Kiwango hicho cha ukuaji kilitokana na mikakati iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za vita nchini Ukraine, uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli pamoja na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi na shughuli zingine ambazo zimechachuliwa kutokana ukuaji wa sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022, Pato ghafi la Taifa kwa bei za mwaka husika lilikuwa shilingi trilioni 170.3 sawa na Dola za Marekeni bilioni 77.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 156.4 mwaka 2021 sawa na Dola za Marekani billioni 69.94.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa ndani ya lengo la wigo wa kuwa chini ya asilimia 5. Mwaka 2022, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei hadi mwezi Mei, 2023 umebaki kama ilivyokuwa katika kipindi hicho hicho mwaka 2022 ikiwa ni wastani wa asilimia 4.0. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma na kuongezeka kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya maeneo nchini na nchi jirani kulikosababishwa na upatikanaji wa mvua katika maeneo yanayotegemea mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ujazi wa Fedha, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei linalotokana na mitikisiko ya kiuchumi duniani bila kuathiri kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Kutokana na utekelezaji wa sera hiyo, ukuaji wa ujazi wa fedha ulikuwa ndani ya malengo katika kipindi kilichoishia Aprili 2023, ambapo ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia shilingi bilioni 39,961.5 kutoka shilingi bilioni 34,087.8 mwezi Aprili 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi kwa mwaka 2023 vimeendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 15.91 mwezi Aprili 2023 ikilinganishwa na asilimia 16.31 Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za nje, kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, urari wa malipo yote ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,414.2 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,516.1 kwa kipindi kama hicho. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kutokana na athari hasi za kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na ugavi wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 6,065.6 kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,556.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, pia urari huu umechangiwa na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo tunaitekeleza ikiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)* ambao *material* nyingi tunazozitumia tunaziagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,198.7 kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,585.1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa akiba ya fedha za kigeni. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 4.88 ambayo inatosheleza uagizaji wa huduma kutoka nje kwa kipindi cha takriban miezi 4.4. Mahitaji ya nchi kisheria ni kuwa na kiasi cha fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda usiopungua miezi 4.0.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mwenendo wa Thamani ya Shilingi. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi

washirika wakuu wa kibiashara imeendelea kuwa tulivu, licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali za kiuchumi duniani hususan ongezeko la bei za bidhaa. Hali hii imetokana na utulivu wa mfumuko wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wetu wa kibiashara, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, na uwepo wa chakula cha kutosha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la Taifa hadi kufikia April 2023, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 79,100.19 sawa na ongezeko la asilimia 13.9 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 69,440.01 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 51,162.60 na deni la ndani ni shilingi bilioni 27,937.59. Ongezeko la deni limetokana na kupokewa kwa fedha za mikopo kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya. Aidha, Tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika Desemba, 2022 imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni viko ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mafanikio ya utakelezaji wa mpango kama unavyofahamu Serikali imekuwa ikitekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Utekelezaji wa Mpango huu umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na uongozi mahiri wa Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 katika sekta mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli, kuendelea na ujenzi wa njia ya Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (kilometa 300) utekelezaji wake umefikia asilimia 98.14; kipande cha Morogoro –

Makutupora (kilometa 422) utekelezaji wake umeshafikia asilimia 93.83 na ujenzi katika kipande cha Tabora - Isaka ambapo utekelezaji wake umeshafikia asilimia 2.39. Ujenzi kipande cha Mwanza-Isaka umeshafikia asilimia 31.07. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria kwa ajili ya reli ya kati; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa 52 ya mizigo na mabehewa sita ya abiria na kuanza kwa huduma katika reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bwawa la Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115: Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umeshafikia zaidi ya asilimia 86.89 ambapo ujenzi wa handaki la kuchepusha maji na ujenzi wa kingo ndogo za juu na chini umeshakamilika. Aidha, ujenzi wa ukuta wa bwawa kuu umefikia asilimia 94.85, handaki la kupeleka maji kwenye mitambo umeshafikia asilimia 99.08, jengo la mitambo, kituo cha kupokea na kusafirishia umeme asilimia 98.87, kingo saidizi za kuzuia maji yasitoroke asilimia 84.47. Vilevile zoezi la ujazaji maji katika bwawa linaendelea ambapo hadi tarehe 23 Mei, 2023, kimo cha maji ya bwawa kimefikia mita 160.51 ambapo ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania kumefanyika kwa sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege nne ambazo ni ndege moja aina ya Boeing 767-300F ya mizigo iliyowasili tarehe 3 Juni, 2023, ndege mbili aina ya *Boeing 737-9 Max* zinazotarajiwa kuwasili Agosti, 2023 na Desemba, 2023 na ndege moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* inayotarajiwa kuwasili Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuboresha usafiri na usafirishaji wa abiria katika Maziwa Makuu tunaendelea na ujenzi wa meli mpya MV Mwanza Hapa Kazi Tu, yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 hadi tani 400 za mizigo. Kwa upande wa uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam tunaendelea na zoezi la uchimbaji na upanuzi wa lango la kugeuzia meli hadi kufikia kina cha mita 15.5 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 96.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TARURA* utengenezaji wa barabara vijijini na mijini zinazosimamiwa na *TARURA* jumla ya kilometa 163.83 za lami zimejengwa na jumla ya kilometa 4,724.15 za changalawe zimejengwa na madaraja 75 na makalavati 95 yamejengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa kilomita 14,826.35 tayari zimefanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za afya Serikali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa hapa nchini, lengo ikiwa ni kurahisisha upatikanaji wake ambapo jumla ya wagonjwa 25 wamepatiwa huduma za upandikizaji wa uroto katika Hospitali za Muhimbili pamoja Benjamin Mkapa. Upatikanaji wa huduma hizi hapa nchini umepunguza gharama za kufuata huduma nje kutoka shilingi milioni 250 hadi kufikia shilingi milioni 70, sawa na punguzo la asilimia 72.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa programu ya elimu ya msingi bila malipo, elimu ya sekondari bila ada pamoja na jumla ya shilingi bilioni 295.3 tayari zimeishatolewa. Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 652.1 kwa wanafunzi laki mbili na mbili mia nane sabini na saba wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari katika mikoa 26 ya Tanzania Bara, kuendelea na ukamilishaji wa madarasa 1,072 ya shule kongwe za msingi, kuendelea na ukamilishaji wa maboma 809 ya madarasa katika shule za msingi, kuendelea na ukamilishaji wa vyumba 271 vya maabara za sayansi katika shule za sekondari na kuendelea na ukarabati na ujenzi wa vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi *(FDCs)* na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji vijijini na mijini hali ya upatikanaji wa maji nchini inaendelea kuimarika ambapo kwa upande wa vijijini wastani wa upatikanaji wa maji umefikia asilimia 77.0 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 70.1 kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuzalishwa na kusambazwa kwa tani 1,004 za mbegu bora za ruzuku za alizeti kwa wakulima katika wilaya 39 za mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya, Mwanza na Singida, kuzalishwa na kusambazwa kwa tani 80 za mbegu bora za ruzuku za ngano katika halmashauri ya wilaya ya Makete, kutolewa na kusambazwa kwa tani 449,795 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho 160 kwenye mamlaka 83 za Serikali za Mitaa, kununuliwa kwa lita 52,560 za dawa ya kuogesha mifugo kwa ajili ya majosho 2,644 na kusambazwa kwenye mashamba ya Wizara na taasisi zake na kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo kwa mifugo dozi 679,827,610.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi mafaniko yaliyopatikana ni kuendelea kwa ujenzi wa Bandari ya uvuvi Kilwa Masoko kule Lindi, ambapo usanifu wa kina umekamilika na kuanza uchimbaji na kuendelea na taratibu za ununuzi wa meli mbili za uvuvi wa bahari kuu zenye vifaa vya kisasa. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha *TAFIRI* – Dar es Salaam na kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa makubwa matatu na madogo sita katika Kituo cha Rubambagwe – Geita, kuendelea na ujenzi wa mashamba darasa sita ya ufugaji wa samaki katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Iringa, Njombe, Songea, Tandahimba na Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini muhimu na madini mkakati na makampuni matatu kutoka Australia yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 667. Mafaniko mengine ni ununuzi wa mawe mawili makubwa ya madini ya Tanzanite yenye jumla ya uzito wa kilo 5.22 kutoka kwa wachimbaji wadogo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.24.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa TEHAMA, habari na mawasiliano. Mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi mpya wa kilomita 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vituo 15 vya kutoleo huduma ya Mkongo, kuendelea na ujenzi wa njia mpya za mkongo wa Taifa wa mawasiliano na jumla ya kilomita 4,442 kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuimarishwa kwa miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi na kutangazwa vivutio vya utalii kupitia programu maalum ya Tanzania *the Royal Tour* ambayo imewezesha kuwepo kwa ongezeko la idadi ya watalii wa ndani na kimataifa wanaotembelea maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwekezaji, viwanda na biashara Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini kwa kufanya mapitio ya Sera mbalimbali ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022 na kuendelea na uwekezaji wa miundombinu wezeshi katika maeneo maalumu ya uwekezaji. Pia kushiriki makongamano mbalimbali ya kuwezesha kufanyika yaliyofanyika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kusajiliwa kwa miradi mitano katika vituo vya mauzo nje vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 15.6 inayotarajiwa kuchangia mauzo ya nje yenye thamani ya dola za Marekani milioni 12.6, na kuzalisha ajira zaidi ya 1,247, na kukamilika kwa usimikaji wa mifumo katika dirisha moja la kutolea huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utawala Bora na Utawala wa Sheria baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuhakikisha kuwa utawala bora na utawala wa sheria unaendelea kushamiri nchini. Serikali imeendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya kitaasisi na utoaji haki, uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama katika Wilaya ya Manyoni, kuendelea na ujenzi wa Mahakama katika Wilaya ya Liwale ambapo utekelezaji wake umeishafikia zaidi ya asilimia 70, Kwimba zaidi ya asilimia 80,

Ulanga zaidi ya asilimia 35. Vilevile kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tisa ambapo Mahakama ya Mwanzo Madale utekelezaji umeishafikia zaidi ya asilimia 75, Kinesi (Rorya) asilimia 99, Mahenge (Kilolo) asilimia 97, Luilo (Ludewa) asilimia 80, Newala (Newala) asilimia 75, Usevya kule Mlele asilimia 95. Vilevile Nyakibimbili kule Bukoba asilimia 90, Kabanga kule Ngara asilimia 80, Mlimba kule Mang'ula na Morogoro asilimia 80 na mengine ni kukamilika kwa majengo ya Mahakama Kuu Tabora, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Wizara katika mji wa Serikali hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utamaduni, Sanaa na Michezo baadhi ya mafanikio ni kutolewa mikopo kwa awamu mbili yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wasanii, wadau 45 katika tasnia za utamaduni na sanaa. Aidha, Serikali imeratibu matamasha mbalimbali yenye lengo la kudumisha urithi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio mengine ambayo yamepatikana ni pamoja na timu ya mpira wa miguu ya watu wenye ulemavu *(Tembo Worriers)* ilifanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali ya kombe la dunia kwa watu wenye ulemavu na kuiweka nchi yetu kwenye orodha ya timu kumi bora za duniani. Pia Timu za Taifa za Wanawake *(Serengeti Girls)* kushiriki fainali ya Kombe la Dunia nchini India na kufika hatua ya robo fainali mwezi Oktoba, 2022. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na nchi kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Mpira wa Miguu *(CAF)* ambayo imefanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana, kwa namna ya pekee kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake alizoziweka katika kuhamasisha timu zetu katika michezo ya Kimataifa kwa kununua kila goli linalofungwa na timu zetu zinapokuwa katika mashindano ya Kimataifa. Kutokana na juhudi hizo timu ya Simba imepata shilingi milioni 55 na timu ya Yanga shilingi milioni 135, Yanga hoyee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutoa pongezi kwa klabu ya Simba kwa kuendelea kufanya vizuri kimataifa ambapo

imefika hatua ya robo fainali katika michuano ya klabu bingwa. Aidha, kwa kipekee kabisa napenda kuipongeza timu ya Yanga kwa kufika hatua ya fainali katika kombe la Shirikisho Barani Afrika pamoja na kutoa mfungaji bora na kipa bora, mfungaji bora alikuwa Mayele na Kipa Bora alikuwa Diara. Hakika timu ya Simba mna mengi pia ya kujifunza kutoka timu ya Yanga; na zingine zijifunze ili mwaka kesho tuwe na timu nyingi zinazofanya vizuri kama Simba na Yanga walivyofanya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa mpango yanapatikana katika kitabu cha mpango sura ya pili.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa 2050 ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 3 Aprili, 2023 hapa Dodoma. Aidha, Serikali imepanga kufikia makundi yote ya wadau katika zoezi la ukusanyaji wa maoni ili kuhakikisha dira inakuwa na maono jumuishi. Nitumie fursa hii, kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya Dira 2050 yatahusisha tathimini ya utekelezaji wa Dira 2025, ambapo matokeo ya tathmini hiyo yataweka msingi wa maandalizi ya Dira 2050. Hivyo, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa maandalizi ya Dira Bora kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo yatategemea ushiriki mkubwa na maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ikijumuisha wale waishio nje, kwa maana ya *Diaspora,* na washirika wetu wa maendeleo. Hivyo, usisite kutoa maoni yako pale utapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) yenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023 na Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda, kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika

Mashariki 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo Afrika na malengo endelevu 2030.

Mheshimiwa Spika, malengo na shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2023. Malengo hayo ya ukuzaji wa uchumi katika kipindi cha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.2 kwa mwaka 2023 kutoka asilimia 4.7 kwa mwaka 2022;

(ii) Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia tatu hadi saba katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2023/2024 kutoka asilimia 14.4 kwa mwaka 2022/2023;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12 ya Pato la Taifa na matarajio kutoka matarajio ya asilimia 11.5 mwaka 2022/2023;

(v) Nakisi ya bajeti kuwa chini ya asilimia tatu ya Pato la Taifa na mwisho;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kiwango cha kukidhi uagizaji wa bidhaa usiyopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, kimsingi misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asilia na yasiyo ya asilia;

(iii) Kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kushuka kwa uchumi wa dunia;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula;

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu ndani ya nchi yetu na nchi Jirani; na

(vi) Kuendelea kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Reli ya Kisasa *(SGR),* Mradi Mkuu wa Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere, kuboresha Shirika la Ndege *ATCL*, kuchakata na kusindika gesi asilia ya kimiminika *(LNG)* – Lindi, kufua umeme wa maji wa Ruhudji na Rumakali kule Njombe, Daraja la JPM kule Kigongo (Busisi), ujenzi wa barabara na madaraja makubwa kanda maalumu za kiuchumi ikiwemo maeneo maalumu ya uwekezaji Bagamoyo na programu ya kuendeleza ujuzi adimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani huduma mbalimbali katika kukuza sekta za uzalishaji zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi zitaendelea kutekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na programu za kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili pamoja na miradi ya kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2024 miradi mikubwa ambayo ipo katika maandalizi ya kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* ni pamoja na kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika Mikoa ya Dodoma kule Zuzu, Singida kule Manyoni, Kilimanjaro kule Same. Miradi ya Uzalishaji wa Umeme kwa kutumia maji kule Ruhudji, Rumakali, Mradi wa Miundombinu ya Kusambaza Gesi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Mradi wa Kusafirisha Umeme Tanzania kwenda Malawi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni ya Reli ya Dar es Salaam, Reli ya Mtwara – Bamba Bay, uendeshaji wa reli, uendeshaji wa barabara ya haraka *(expressway)* kutoka Kibaha kwenda Morogoro pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, Serikali inaendelea na hatua za mwisho za utekelezaji wa matakwa ya kisheria kwa upande wa Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango unaweza kuathiriwa na vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi hivyo ni pamoja na mabadiliko ya viwango vya riba na mikopo katika soko la ndani na nje, uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu, migogoro na hali ya siasa inayoendelea katika nchi jirani, kikanda pamoja na kimataifa ambayo inaweza ikaongeza kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ugharamiaji wa mpango. Katika mwaka 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 14,077.2 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,795.1 sawa na asilimia 77.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.1 sawa na asilimia 23 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Fedha hizi zitakusanywa kutoka katika mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo nafuu, mikopo ya ndani na mikopo ya nje yenye masharti ya biashara. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo utaratibu huo wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024 ni wa tatu katika utekelezaji wa mpango wa tatu wa maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Utekelezaji wa mpango utaendelea kuimarisha mahusiano ya kisiasa, ulinzi, diplomasia ya uchumi na nchi nyingine na kuendelea kutekeleza kasi ya miradi ya maendeleo, kuchochea uwekezaji viwandani hususani kwa kutumia rasilimali watu na malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini ikiwemo mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, madini, misitu na gesi asilia. Pia kuimarisha viashiria vya uchumi jumla, kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani ikiwemo kuimarisha majadiliano na wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuendelea na mashirikiano na sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na ya kimkakati. Kuimarisha sekta za uzalishaji ili kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi, kufungua fursa zaidi za ajira na maendeleo ya watu, kuboresha upatikanaji wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwemo huduma za afya, elimu, umeme, maji safi na salama mijini na vijijini pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi ya uwekezaji na biashara kwa ajili ya masoko ya kimataifa hususani ya nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kukabiliana na athari za majanga mbalimbali ya asili na yasiyo ya asili yakiwemo mabadiliko ya tabianchi, magonjwa na vita. Aidha, tutaendelea kuimarisha utekelezaji kwa kuweka mipango madhubuti ya kupunguza athari zitokanazo na vita inayoendelea kule Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha; kwa niaba ya Serikali naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, washirika wa maendeleo, taasisi za elimu na tafiti, taasisi za dini, sekta binafsi, asasi za kiraia, wananchi wote kwa namna walivyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Wadau hao wamekuwa na mchango mkubwa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa msingi huo, ninawaomba na kuwasihi wadau wote waendelee kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na Rais shupavu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Mawaziri wenzangu, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Viongozi wote wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024. Aidha, hotuba hii isingeweza kukamilika bila jitihada kubwa zilizofanywa na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, kwa dhati ya nafsi yangu naomba nitoe shukrani za dhati kipekee kwa Mhe. Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na

Mipango, Naibu Waziri wa Viwango vya Wizara ya Fedha, nakupongeza sana; pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bingwa kabisa wa Uchumui Dkt. Natu El-Maamry Mwamba kwa kujitoa usiku na mchana kukamilisha kwa wakati na kwa ubora Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa wa mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa kutenga muda wao kunisikiliza. Aidha, napenda kuwataarifu Wabunge wote kuwa hotuba hii pia ipo katika pamoja na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ni www.mof.go.tz.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2022 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(a) **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Taarifa zilizopo katika vitabu hivi, ndiyo msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 nitakayoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu leo alasiri.

(b) **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana tena kwa mara nyingine katika Bunge hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali.

(c) **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa, nitoe pongezi zangu za dhati; kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti aliouonesha tangu alipoingia madarakani. Kupitia uongozi wake mahiri, tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta mbalimbali ikijumuisha sekta za uzalishaji, huduma za jamii na miundombinu wezeshi. Aidha, Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kimataifa. Hakika nchi yetu imebarikiwa kuwa na Rais mwenye maono makubwa katika kuboresha ustawi wa maendeleo wa nchi pamoja na watu wake. ***HAKIKA MAMA HANA BAYA.***

(d) **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri na jitihada zao katika kuhakikisha Taifa letu linakuwa na maendeleo endelevu.

(e) **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na mhimili mzima wa utoaji wa haki kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, pongezi za pekee ziwaendee Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuendelea kusimamia ulinzi na usalama wa nchi na hivyo kuwezesha shughuli za kiuchumi nchini kufanyika kwa amani, usalama na utulivu.

(f) **Mheshimiwa Spika**, vile vile naomba nikupongeze wewe binafsi, na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa Sillo Daniel Baran (Mb) na Mheshimiwa

David Mwakiposa Kihenzile (Mb) kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mheshimiwa Sillo Daniel Baran (Mb) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua (Mb.) kwa ushauri wao mahiri wakati wa uandaaji wa taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii. Maoni na ushauri wao umezingatiwa kikamilifu katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/24 ambao utekelezaji wake utaanza tarehe 01 Julai, 2023.

(g) **Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika nafasi ya Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi na weledi mkubwa ili kutimiza matarajio yake aliyonayo kwangu na Wizara ya Fedha na Mipango. Ninawashukuru pia, wanachama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa namna tunavyoendelea kushirikiana katika kukiimarisha zaidi chama chetu na kuhakikisha tunatekeleza yale yote yaliyokusudiwa katika Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, kipekee napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuzidi kunitia moyo na kushirikiana nami katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

**MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022**

**Uchumi wa Dunia**

**8. Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2023 inaonesha kuwa, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.3 mwaka 2021 hadi asilimia 3.4 mwaka 2022. Upungufu huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa China na India; madhara ya janga la UVIKO-19; vita kati ya Urusi na Ukraine; na sera za kupunguza ukwasi katika chumi za Ulaya ili kukabiliana na mfumuko wa bei. Aidha, Uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua zaidi na kufikia ukuaji wa asilimia 2.8

mwaka 2023 kutokana na kuendelea kwa vita kati ya Urusi na Ukraine, mabadiliko ya Tabia Nchi na Sera za Marekani kuongeza riba.

**Uchumi wa Afrika na Kikanda**

**9. Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua kufikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2021. Aidha, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikua kwa wastani wa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2021. Vile vile, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa ni asilimia 5.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2021. Upungufu huo ulitokana na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine uliyosababisha mfumuko wa bei za nishati ya mafuta na vyakula.

**Uchumi wa Taifa**

**Pato la Taifa**

9. **Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2022, thamani halisi ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi trilioni 141.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 135.5 mwaka 2021. Aidha, kiwango halisi cha ukuaji wa pato la Taifa kilifikia asilimia 4.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2021. Kiwango hicho cha ukuaji kilitokana na: mikakati iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za vita nchini Ukraine; uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi; na kuongezeka kwa shughuli za utalii. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji kwa mwaka 2022 ni pamoja na: sanaa na burudani (asilimia 19.0); madini (asilimia 10.9); fedha na bima (asilimia 9.2); malazi na huduma ya chakula (asilimia 9.0); na umeme (asilimia 7.6). Aidha, kutokana na hatua madhubuti zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali thamani ya Pato ghafi la Taifa

linatarajiwa kufikia dola za Marekani bilioni 85.42 mwaka 2023/24.

10. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2022, Pato ghafi la Taifa (kwa bei za mwaka husika) lilikuwa shilingi trilioni 170.3 (sawa na Dola za Marekeni bilioni 77.6) ikilinganishwa na shilingi trilioni 156.4 mwaka 2021 (sawa na Dola za Marekani billioni 69.94). Aidha, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu Tanzania Bara ilikuwa 59,851,347 ikilinganishwa na makadirio ya idadi ya watu 57,724,380 mwaka 2021. Hivyo, Pato la Taifa kwa Mtu (GDP per capita) kwa mwaka 2022 lilikuwa shilingi 2,844,641 ikilinganishwa na shilingi 2,708,999 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Kiasi hicho ni sawa na dola za Marekani 1,229.1 mwaka 2022 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na dola za Marekani 1,173.3 mwaka 2021. Hali hii inaendelea kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ngazi ya chini.

**Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

**12. Mheshimiwa Spika,** mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa ndani ya lengo la wigo wa kuwa chini ya asilimia 5. Mwaka 2022, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei hadi mwezi Mei, 2023 umebaki kama ilivyokuwa katika kipindi hicho hicho mwaka 2022 ikiwa ni wastani wa asilimia 4.0. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma; na kuongezeka kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya maeneo nchini na nchi jirani kulikosababishwa na upatikanaji wa mvua katika maeneo yanayotegemea mvua.

**Ujazi wa Fedha**

**13. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei linalotokana na mitikisiko ya kiuchumi duniani bila kuathiri kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Kutokana na utekelezaji wa sera hiyo, ukuaji wa ujazi wa fedha ulikuwa ndani

ya malengo ambapo katika kipindi kilichoishia Aprili 2023, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia shilingi bilioni 39,961.5 kutoka shilingi bilioni 34,087.8 mwezi Aprili 2022. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 15.6 hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 31,048.8 mwezi Aprili 2023 kutoka shilingi bilioni 26,861.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

**14. Mheshimiwa Spika,** viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi kwa mwaka 2023 vimeendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 15.91 mwezi Aprili 2023 ikilinganishwa na asilimia 16.31 Aprili 2022. Vilevile, wastani wa viwango vya riba za amana za muda maalumu na za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 6.79 kutoka asilimia 6.81 mwaka 2022. Mwenendo huu ulichagizwa na utekelezaji madhubuti wa sera wezeshi ya Fedha.

**Sekta ya Nje**

15. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, urari wa malipo yote ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,414.2. ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,516.1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kutokana na athari hasi za kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na ugavi wa bidhaa duniani ikilinganishwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 6,065.6 kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,556.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

16. **Mheshimiwa Spika** urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,198.7 kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,585.1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 38.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na usafirishaji

kulikosababishwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia kutokana na kupungua kwa athari za UVIKO-19. Vile vile, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,866.9 kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,971.7 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

**17. Mheshimiwa Spika,** akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 4.88 ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.4. Mahitaji ya nchi kisheria ni kuwa na kiasi cha fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda usiopungua miezi 4.0.

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

**18. Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara imeendelea kuwa tulivu, licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali za kiuchumi duniani hususan ongezeko la bei za bidhaa. Hali hii imetokana na utulivu wa mfumuko wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wetu wa kibiashara, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, na uwepo wa chakula cha kutosha nchini. Katika mwezi Aprili, 2023 dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,324.07 ikilinganishwa na shilingi 2,322.16 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Aprili 2022 hadi Aprili 2023 dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,310.14.

**Mwenendo wa Sekta ya Kibenki**

19. **Mheshimiwa Spika,** sekta ya benki nchini imeendelea kubaki imara, himilivu na yenye kutengeneza faida ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha katika kutoa mikopo kwa sekta za uchumi na kupunguza umaskini. Mikopo kwa sekta binafsi

imeongezeka kufikia shilingi bilioni 28,702.95 kwa mwaka ulioishia Aprili 2023 kutoka shilingi bilioni 23,422.5 Aprili 2022 sawa na ongezeko la asilimia 22.5. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 15.8 katika kipindi cha Aprili 2022 hadi Aprili 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022 na lengo la asilimia 10.7 kwa mwaka 2022/23. Ukuaji huu umechochewa na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo ulipaji wa malimbikizo ya madai na jitihada nyingine za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, hali iliyochochea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kiliendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 5.5 Aprili, 2023 kutoka asilimia 8.3 Aprili, 2022.

20. **Mheshimiwa Spika,** utendaji wa sekta ndogo ya bima ulikuwa wa kuridhisha ambapo hadi kufikia Machi 2023, iliandikisha na kutoa leseni 1,196 zikijumuisha kampuni za bima, kampuni za uwakala na wadau wote wanaohusika na biashara ya bima nchini. Aidha, kwa upande wa sekta ndogo ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, mtaji wa soko la hisa kwa kampuni za ndani, uliongezeka kwa asilimia 16.97 Machi 2023 na kufikia shilingi trilioni 10.82 ikilinganishwa na shilingi trilioni 9.25 katika kipindi kilichoishia Machi 2022. Vilevile, uwekezaji kwenye Mifuko ya UTT AMIS uliongezeka na kufikia shilingi trilioni 1.44 katika kipindi kilichoishia Machi 2023, ikilinganishwa na shilingi bilioni 852.21 katika kipindi kilichoishia Machi 2022 sawa na ongezeko la asilimia 69.17.

21. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha ambapo hadi kufikia Machi, 2023, ilitoa jumla ya leseni 1,187 kwa Watoa huduma daraja la pili ikilinganishwa na jumla ya leseni 736 zilizotolewa Machi 2022, leseni 780 kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo ikilinganishwa na leseni 615 zilizotolewa machi 2022 nakusajili vikundi 37,937 vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ikilinganishwa na vikundi 24,835 vilivyokuwepo Machi 2022. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa mafunzo kwa waratibu 115 wa biashara ya huduma ndogo za fedha kutoka katika mikoa 13 mwezi Mei, 2023. Vilevile, watoa huduma

ndogo za fedha Daraja la Pili walikopeshwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 870 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini.

**Deni la Serikali**

22. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2023, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 79,100.19 sawa na ongezeko la asilimia 13.9 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 69,440.01 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 51,162.60 na deni la ndani ni Shilingi bilioni 27,937.59. Ongezeko la deni limetokana na: kupokewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya. Aidha, Tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika Desemba, 2022 imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

23. ***Mheshimiwa Spika***, mnamo Machi 2023, kampuni za Fitch Ratings na Moody's Investors Service zilianza zoezi la kuifanyia nchi tathmini ya kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa. Zoezi hilo lilikamilika ambapo kampuni ya Moody's Investors Service ilichapisha matokeo ya tathmini hiyo mwezi Mei 2023 na kampuni ya Fitch Ratings mwezi Juni 2023. Kwa mujibu wa matokeo hayo, Tanzania imewekwa katika daraja la B2 POSITIVE na Kampuni ya Moody's Investors Service na daraja la B POSITIVE na Kampuni ya Fitch Ratings ambayo yanaashiria taswira chanya kwa nchi kimataifa. Pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi, usimamizi makini wa deni la Taifa, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa pamoja na kuleta maridhiano ya kisiasa ndani ya nchi. Kukamilika kwa zoezi hilo, kutaiwezesha nchi kutambulika katika masoko ya fedha ya kimataifa na hivyo, kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa Serikali na sekta binafsi.

24. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu taarifa ya hali ya uchumi yanapatikana katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23**

**25. Mheshimiwa Spika,** kama unavyofahamu Serikali imekuwa ikitekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, wenye dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Utekelezaji wa Mpango huu umekuwa wa mafanikio makubwa kutokana na uongozi mahiri wa Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 katika sekta mbalimbali ni pamoja na:

(i) **Miundombinu ya Reli:** Kuendelea na ujenzi wa njia ya Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 98.14; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) utekelezaji umefikia asilimia 93.83; kipande cha Makutupora - Tabora (km 371) asilimia 7.0; kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka (km 165) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 2.39; na ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) umefikia asilimia 31.07. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria kwa ajili ya reli ya kati; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa 52 ya mizigo na mabehewa sita (6) ya abiria na kuanza kutoa huduma katika reli ya kati; na kukamilika kwa uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

(ii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115**: Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 86.89 ambapo ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (diversion

tunnel) na ujenzi wa kingo ndogo za juu na chini umekamilika. Aidha, ujenzi wa ukuta wa bwawa kuu umefikia asilimia 94.85, handaki la kupeleka maji kwenye mitambo (power waterway) (asilimia 99.08), jengo la mitambo (power house) (asilimia 68.30), kituo cha kupokea na kusafirishia umeme (switchyard) (asilimia 98.87), kingo saidizi za kuzuia maji yasitoroke (asilimia 84.47). Vile vile, zoezi la ujazaji maji katika bwawa linaendelea ambapo hadi tarehe 23 Mei, 2023, kimo cha maji ya bwawa kimefikia mita 160.51 ambapo ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari.

(iii) **Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania:** Kufanyika kwa sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege nne (4) ambazo ni ndege moja (1) aina ya Boeing 767-300F ya mizigo iliyowasili tarehe 03 Juni, 2023, ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 Max zinazotarajiwa kuwasili Agosti 2023 na Desemba 2023 na ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner inayotarajiwa kuwasili Februari, 2024; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika karakana ya KIMAFA katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85.0. Aidha, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 24 ambapo vituo 14 ni vya ndani ya nchi na vituo 10 ni vya nje ya nchi. Vituo vya ndani ya nchi ni Arusha; Bukoba; Dar es Salaam; Dodoma; Geita; Kilimanjaro; Kigoma; Songwe; Mpanda; Mtwara; Mwanza; Songea; Tabora na Zanzibar na vituo vya nje ya nchi ni: Bujumbura; Entebbe, Hahaya; Guangzhou; Harare; Lubumbashi; Lusaka; Mumbai; Nairobi na Ndola.

(iv) **Miradi ya Umeme:** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Sekta hii ni wezeshi katika uzalishaji viwandani, kukuza biashara na kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini. Hadi Mei 2023 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa ulifikia MW 1,872.05, sawa na ongezeko la asilimia 10.5

ikilinganishwa na MW 1,694.55 zilizokuwepo mwaka 2021/22. Aidha, hatua zilizofikiwa katika utelekezaji wa baadhi ya miradi ya umeme ni pamoja na: kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185 ambapo mitambo yote minne (4) yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 185 imewashwa na umeme huo kuingizwa katika Gridi ya Taifa; na kufikia asilimia 99 ya utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa maji Rusumo (MW 80). Kwa upande wa miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme, Serikali imeunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kutokea kituo cha Nyakanazi na imeunganisha Wilaya za Ngara na Biharamulo kwenye kituo cha gridi ya Taifa cha Nyakanazi. Aidha, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze umefikia asilimia 93.5 na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze umefikia asilimia 64. Vile vile, hadi Mei, 2023 jumla ya vijiji 10,127 kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 82.21 vimeunganishwa na huduma ya umeme.

(v) **Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege:** Kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, uzio wa kiwanja, maegesho ya magari katika Kiwanja cha Ndege Mwanza; kukamilika kwa upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Mtwara na Songea; Kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege Dodoma; na kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Geita. Shughuli zinazoendelea ni pamoja na: ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Awamu ya Kwanza inayohusisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na jengo la abiria ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18; Kiwanja cha Ndege Iringa (asilimia 50), Songwe (asilimia 98) na Musoma (asilimia 47). Aidha, kazi nyingine zilizofanyika ni kuanza maaandalizi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga.

(vi) **Uendelezaji wa Bandari: Bandari ya Dar es Salaam:** kuendelea na zoezi la uchimbaji na upanuzi wa lango la

kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli hadi kufikia kina cha mita 15.5 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 96. **Bandari ya Tanga**: kuendelea na uboreshaji wa Bandari katika awamu ya pili ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 99. **Bandari za Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kuendelea na maandalizi ya awali ya ujenzi wa Bandari za Bukoba na Kemondo Bay; na kuendelea na hatua za mwisho za kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya *Mwanza North* ikijumuisha miundombinu ya Reli (SGR). **Ziwa Tanganyika**: kukamilika kwa ujenzi wa Gati katika Bandari mpya ya Karema; na kuendelea na usanifu wa ujenzi wa jengo la abiria (*Passenger Lounge)* na ukuta wa mizigo wa *Lighter Quay* katika Bandari ya Kibirizi na gati la Bandari ya Ujiji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 69. **Ziwa Nyasa**: Kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi; kuendelea na ujenzi wa sehemu ya kuegesha meli (ramp) katika bandari ya Kiwira; na kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya kuegesha meli katika bandari ya Ndumbi.

(vii) **Kuboresha Huduma za Usafiri na Usafirishaji wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu:** Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83; kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Umoja na MT Sangara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75.8 na 90.7 mtawalia; kukamilisha taratibu za kupata Mkandarasi wa ujenzi wa meli mpya tatu (3) pamoja na chelezo ambapo meli mbili (2) zitajengwa katika Ziwa Tanganyika, meli moja (1) Ziwa Victoria na Chelezo Ziwa Tanganyika.

(viii) **Barabara na Madaraja Makubwa:** Kuendelea kuboresha mtandao wa barabara nchini kwa kujenga barabara za mikoa na barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani na barabara za mijini na vijijini. Miradi ya barabara iliyokamilika ni pamoja na: ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege sehemu za Lusitu – Mawengi (km 50); Moronga – Makete (km 53.5); na Kisorya - Bulamba (km 51). Aidha, ujenzi wa madaraja ya Tanzanite (Dar es Salaam),

Wami (Pwani), Kiyegeya (Morogoro) na Kitengule (Kagera) umekamilika. Vile vile, ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa km 3.2 unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 72.

Kwa upande wa barabara za vijijini na mijini zinazosimamiwa na TARURA, jumla ya kilometa 163.83 za lami, kilometa 4,724.15 za changarawe madaraja 75 na makalvati 95 yamejengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa 14,826.35 zimefanyiwa matengenezo.

(ix) **Huduma za Afya**: Serikali imeendelea kuboresha **huduma za kibingwa** nchini kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake ambapo jumla ya wagonjwa 25 wamepatiwa huduma ya upandikizaji wa uroto katika hospitali za Muhimbili na Benjamin Mkapa. Upatikanaji wa huduma hii hapa nchini umepunguza gharama za kupata huduma nje ya nchi kutoka shilingi milioni 250 hadi kufikia milioni 70 sawa na punguzo la asilimia 72 ya gharama zilizohitajika; kuanza kutoa huduma za kibingwa ya kibobezi ya kupunguza uzito kwa kuweka puto (Intragastric ballon) katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili – Mloganzila ambapo jumla ya wagonjwa 87 wamepatiwa huduma hiyo; na kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha upandikizaji viungo na ukarabati wa wodi za watoto mahututi (NICU) katika hospitali ya Muhimbili – Mloganzila.

Kwa upande wa **hospitali za rufaa za kanda** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa majengo ya wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Bugando; kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za tiba - mionzi kwa magonjwa ya saratani katika hospitali ya KCMC; na kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), jengo la huduma za dharura (EMD), chumba cha tiba mtandao, katika hospitali ya rufaa Mbeya.

**Kwa upande wa hospitali za rufaa za mikoa** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya OPD, afya ya uzazi, EMD, ICU, upasuaji,

mifupa, wodi, sehemu ya kufulia, damu salama na kichomea taka katika hospitali ya Njombe; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 94) katika hospitali ya Simiyu; na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la afya ya uzazi na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi katika hospitali ya Geita ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.

Aidha, Serikali imeendelea kuboresha **huduma za afya kufikia ngazi za chini** ambapo inaendelea na: ujenzi wa hospitali 59 na ukarabati wa hospitali kongwe 19 za Halmashauri; ukamilishaji wa zahanati 300 katika halmashauri 184; na ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya afya 150, zahanati 300, na hospitali za Halmashauri 71.

Kwa upande wa upatikanaji wa **huduma za bima za afya**, idadi ya watanzania wanaopata huduma za bima ya afya imeongezeka kutoka asilimia 21.2 mwaka 2019/20 hadi asilimia 30.6 mwaka 2021/22.

(x) **Elimu:** Kuendelea na utekelezaji wa programu ya Elimumsingi na Sekondari Bila Ada ambapo jumla ya shilingi 295.3 zimetolewa; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 652.1 kwa wanafunzi 202,877 wa elimu ya juu; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara; kuendelea na ukamilishaji wa madarasa 1,072 ya shule kongwe za msingi; kuendelea na ukamilishaji wa maboma 809 ya madarasa ya shule za msingi; kuendelea na ukamilishaji wa vyumba 271 vya maabara za Sayansi katika Shule za sekondari; na kuendelea na ukarabati na ujenzi wa vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi (FDCs) na vyuo vikuu.

(xi) **Maji Mijini na Vijijini:** Hali ya upatikanaji wa maji nchini inaendelea kuimarika ambapo kwa upande wa vijijini wastani wa upatikanaji wa maji umefikia asilimia 77.0 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 70.1 mwaka 2020. Aidha, kwa upande wa mijini hali ya upatikanaji wa

huduma ya majisafi imeongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2020 hadi asilimia 88.0 mwaka 2022. Vile vile, jumla ya miradi 586 yenye vituo 5,748 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,086,442 kwenye vijiji 1,293 imekamilika. Kadhalika, uchimbaji wa visima vitano (5) katika jiji la Dodoma, ujenzi wa choteo jipya katika mradi wa maji na usafi wa mazingira mji wa Kigoma, awamu ya kwanza ya mradi wa uboreshaji maji katika miji ya Tinde na Shelui, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita milioni 15 katika eneo la Kisarawe II na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika eneo la Kimbiji umekamilika. Ujenzi wa mradi wa maji na usafi wa mazingira Arusha unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 92.67; Mugango – Kiabakari - Butiama (asilimia 79); na mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika mji wa Lindi (asilimia 71).

(xii) **Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

**Kilimo:** kuzalishwa na kusambazwa kwa tani 1,004 za mbegu bora za ruzuku za Alizeti kwa wakulima katika wilaya 39 za mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya, Mwanza na Singida; kuzalishwa na kusambazwa kwa tani 80 za mbegu bora za ruzuku za ngano katika halmashauri ya wilaya ya Makete; kutolewa na kusambazwa kwa tani 449,795 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini; kubainisha mashamba makubwa (Block farms) yenye ukubwa wa ekari 264,841.50 kwa ajili ya vijana katika mikoa ya Kigoma (ekari 36,719.75) Mbeya (ekari 52,165), Njombe (ekari 87,000), Dodoma (ekari 33,4543), Singida (ekari 50,000) na Kagera (ekari 5,503.75); kununuliwa kwa viuatilifu lita 106,000 za kudhibiti visumbufu vya milipuko ya viwavijeshi na lita 82,124 zimesambazwa katika Halmashauri 58 za Mikoa ya Manyara, Singida, Tabora, Katavi, Tanga, Geita, Simiyu, Shinyanga, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa vihenge 20 na maghala manne (4) katika Wilaya za Babati, Mpanda na Sumbawanga; kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA kununua mahindi tani 17,257.857 na mtama tani 1,036.457 na Bodi ya Mazao

Mchanganyiko – CPB kununua mahindi tani 34,484, alizeti tani 2,776, mafuta ghafi tani 85.82, mchele tani 1,797, ngano tani 277, maharage tani 406, mtama tani 3,035.06, maharage ya soya tani 393, maharage ya njano tani 30, korosho ghafi tani 523, na mpunga tani 7,065; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha TANECU (Newala) cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 za korosho kwa mwaka; na kuendelea na ujenzi wa skimu mpya za umwagiliaji 19 kati ya 25 zenye ukubwa wa hekta 45,564.

**Mifugo**: Kukamilika kwa ujenzi wa majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho 160 kwenye mamlaka 83 za serikali za mitaa; kununuliwa kwa lita 52,560 za dawa ya kuogesha mifugo kwa ajili ya majosho 2,644 na kusambazwa kwenye mashamba ya Wizara na Taasisi zake; kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo za mifugo dozi 679,827,610 za magonjwa mbalimbali ya kipaumbele; kununuliwa kwa mitamba 1,160 na kununuliwa kwa matrekta 3, Bailer 5, mower 5 na Hay rake 5 na kusambazwa katika mashamba ya serikali; kuhimilisha ng'ombe 60,697 kupitia kambi za uhimilishaji; kuzalishwa kwa jumla ya dozi 116,558 za mbegu za mifugo katika kituo cha NAIC kwa ajili ya uhimilishaji; kununuliwa kwa magari 13 yakiwemo Toyota Hard Top (2) na Toyota Double Cabin (11) na pikipiki 1200 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184; kujengwa kwa minada 19 na kukarabati minada minne (4) katika maeneo mbalilmbali nchini; kuendelea na ujenzi wa mabwawa 11 katika maeneo mbalimbali nchini; kununuliwa kwa tani 8.56 za mbegu za malisho na vipando vya miti malisho 18,025 kutoka mashamba ya Serikali na binafsi na kusambazwa kwa wafugaji; na kuanzishwa kwa vituo nane (8) vya uwekezaji vya vijana vyenye uwezo wa kuchukua jumla ya vijana 240 kwa mwaka kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata uzoefu katika kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji kibiashara, ambapo jumla ya vijana 238 wamesajiliwa katika vituo Atamizi vya LITA na TALIRI.

**Uvuvi:** Kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko – Lindi ambapo usanifu wa kina umekamilika na kuanza uchimbaji; kuendelea na taratibu za ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi wa Bahari Kuu zenye vifaa vya kisasa; kukamilika kwa ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam; kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa makubwa matatu (3) na madogo sita (6) katika Kituo cha Rubambagwe (Geita); kuendelea na ujenzi wa mashamba darasa sita (6) ya ufugaji wa samaki katika Halmashauri za wilaya za Kongwa, Iringa, Njombe, Songea, Tandahimba na Ruangwa; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa boti za uvuvi 158 ikiwa ni awamu ya kwanza kwa ajili ya kukopesha wavuvi; kuvunwa kwa tani 426,555.46 za samaki zenye thamani ya Shilingi trilioni 2.86; kuuzwa nje ya nchi kwa jumla ya tani 29,466.98 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 453.8 na idadi ya samaki hai wa mapambo 150,308 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.82; na kuendelea na tafiti mbalimbali za kujua uwingi, aina, bioanuwai na mtawanyiko wa samaki kwenye Maziwa, Bahari na Mabwawa.

(xiii) **Madini:** Kusainiwa kwa mikataba ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini muhimu na madini mkakati na kampuni tatu (3) kutoka Australia yenye thamani ya dola za Marekani milioni 667; ununuzi wa mawe mawili (2) makubwa ya madini ya Tanzanite yenye jumla ya uzito wa kilo 5.22 kutoka kwa mchimbaji mdogo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.24; kununuliwa na kusimikwa (commissioning) kwa vifaa vya utafiti wa jiosayansi na vifaa vya maabara na uchunguzi; ununuzi wa mitambo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo; ununuzi wa mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa mkaa mbadala na utengenezaji wa mkaa unaotokana na makaa ya mawe; na kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba choronge *(core shade)* eneo la Kizota - Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 75.

(xiv) **Habari, Mawasiliano na TEHAMA**: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi mpya wa Kilomita 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vituo 15 vya kutoleo huduma za Mkongo; kuendelea na ujenzi wa njia mpya za mkongo wa Taifa wa mawasiliano wenye jumla ya kilomita 4,442; kukamilika kwa uboreshaji wa programu ya Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi; na kukamilika kwa uhakiki wa taarifa za miundombinu ya Anwani za Makazi pamoja na taarifa za makazi zilizokusanywa katika Operesheni Anwani za Makazi kwenye Halmashauri 23.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuongeza upanuzi na usikivu wa shirika la utangazaji TBC ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa taratibu za ununuzi za kuwapata wazabuni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa usikivu redio zinazomilikiwa na TBC katika maeneo tisa (9); na kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya TBC Jijini Dodoma.

(xv) **Maliasili na Utalii:** Kuimarisha miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi na kutangaza vivutio vya utalii kupitia programu maalum ya Tanzania - *the Royal Tour* imewezesha kuwepo kwa ongezeko la idadi ya watalii wa ndani na kimataifa waliotembelea maeneo ya hifadhi na Makumbusho ya Taifa kutoka watalii 1,711,625 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 3,818,180 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 123. Katika ongezeko hilo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022 sawa na asilimia 57.7 na watalii wa ndani wameongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022 sawa na asilimia 199.5. Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,310 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,527.72 kwa mwaka 2022 sawa na asilimia 93. Vile vile, Serikali imeimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu.

(xvi) **Uwekezaji, Viwanda na Biashara:** Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini kwa kufanya mapitio ya Sera mbalimbali ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2022, kuendelea na uwekaji wa miundombinu wezeshi katika maeneo maalumu ya uwekezaji na kushiriki makongamano mbalimbali ya uwekezaji yanayofanyika ndani na nje ya nchi. Kutokana na juhudi hizo baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na usajili wa jumla ya miradi mipya 240 (Wazawa 89, wageni 94 na ubia 57) katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ikilinganishwa na miradi 206 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Miradi hii inatarajiwa kuwekeza jumla ya Dola za Marekani milioni 4,387.17 na kuzalisha ajira 39,245.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni: Kusajiliwa kwa miradi mitano (5) katika vituo vya mauzo nje yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 15.6 inayotarajiwa kuchangia mauzo nje yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.6 na kuzalisha ajira 1,247; na kukamilika kwa usimikaji wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa Njia ya Kielektroniki (Tanzania Electronic Investment Single Window - TeIW) awamu ya kwanza pamoja na kuunganisha taasisi saba (7).

(xvii) **Utawala Bora na Utawala wa Sheria:** katika kuhakikisha kuwa utawala bora na utawala wa sheria unaendelea kushamiri nchini, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya Kitaasisi na utoaji haki, uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama ya wilaya ya Manyoni; kuendelea na ujenzi wa Mahakama za wilaya za Liwale ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70, Kwimba (asilimia 80), na Ulanga (asilimia 35); kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tisa (9) ambapo Mahakama ya Mwanzo Madale (Dar es Salaam) utekelezaji umefikia asilimia 75, Kinesi - Rorya (asilimia 99), Mahenge - Kilolo (asilimia 97), Luilo – Ludewa (asilimia 80), Newala – Newala (asilimia 75), Usevya – Mlele (asilimia 95), Nyakibimbili - Bukoba (asilimia 90);

Kabanga – Ngara (asilimia 80) na Mlimba na Mang'ula – Morogoro (asilimia 85); kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Tabora na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi; na kuendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Wizara katika mji wa Serikali Mtumba ambapo ujenzi wa majengo 24 umefikia wastani wa asilimia 60 na ujenzi wa jengo moja (1) la Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) umefikia asilimia 50 kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

(xviii) **Utamaduni, Sanaa na Michezo:** Kutolewa mikopo kwa awamu mbili (2) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wasanii na wadau 45 katika tasnia za utamaduni na sanaa. Aidha, Serikali imeratibu matamasha mbalimbali yenye lengo la kudumisha urithi wa utamaduni ikiwemo: Tamasha kubwa la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam; Tamasha la tano (5) la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki, (JAMAFEST) lililofanyika Septemba, 2022 Jijini Bujumbura - Burundi; Tamasha la 41 la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa la Bagamoyo; na Tamasha la Msimu wa Utamaduni kati ya Tanzania na Afrika Kusini mwezi Novemba, 2022; na kuandaa na kuendesha mashindano ya Kimataifa ya Urembo na Utanashati kwa viziwi (Miss and Mr. Deaf International – MMDI, 2022) ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika Barani Afrika.

Aidha, timu ya mpira wa miguu ya watu wenye ulemavu (Tembo Worriors) ilifanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali ya kombe la dunia kwa watu wenye ulemavu na kuiweka nchi kwenye orodha ya timu kumi bora za dunia; na Timu ya Taifa ya Wanawake (Serengeti Girls) kushiriki fainali za kombe la dunia nchini India na kufikia hatua ya robo fainali mwezi Oktoba, 2022.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na: Nchi kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) mwaka 2022 uliofanyika Jijini Arusha na Mkutano wa Kimataifa wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya IV uliofanyika Jijini

Arusha ambapo Tanzania ilichaguliwa kuwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Baraza hilo; na Tanzania kuwasilisha zabuni ya kuomba kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika – AFCON 2027 kwa ushirikiano na nchi za Kenya na Uganda.

Aidha, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuleta hamasa kwa timu zetu katika michezo ya Kimataifa kwa kununua kila goli linalofungwa na timu zetu zinapokuwa katika mashindano ya Kimataifa ambapo kutokana na juhudi hizo timu ya Simba imepata shilingi milioni 55 na Yanga shilingi milioni 135. ***YANGA HOYEE!!.*** Vile vile, napenda kutoa pongezi kwa klabu ya Simba kwa kuendelea kufanya vizuri kimataifa na kufikia hatua ya robo fainali ya michuano ya klabu bingwa Afrika. Aidha, kwa kipekee kabisa napenda kuipongeza timu ya Yanga kwa kufika fainali ya kombe la Shirikisho barani Afrika pamoja na kutoa Mfungaji Bora (Mayele) na Kipa Bora (Diara). ***HAKIKA TIMU YA SIMBA MNA MENGI YA KUJIFUNZA KUTOKA TIMU YA YANGA.***

26. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Mpango yanapatikana katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Pili.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa mchakato wa Maandalizi ya Dira ya Taifa 2050 ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 03 Aprili, 2023 Dodoma. Aidha, Serikali imepanga kuyafikia makundi yote ya wadau katika zoezi la ukusanyaji wa maoni ili kuhakikisha Dira inakuwa na maono jumuishi. Nitumie fursa hii, kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya Dira 2050 yanahusisha tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025, ambapo matokeo ya tathmini hiyo yataweka msingi wa maandalizi ya Dira 2050. Hivyo, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya Dira Bora kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo yanategemea ushiriki mkubwa na maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote (ikijumuisha wale waishio nje kwa

maana ya Diaspora) na Washirika wetu wa Maendeleo. Hivyo, usisite kutoa maoni yako pale utapohitajika kufanya hivyo.

**MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24**

**28. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wenye dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Mpango umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24; na Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

**29. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2023/24, msisitizo mkubwa utawekwa katika sekta za uzalishaji na zinazozalisha ajira zinazowagusa wananchi wengi ambazo ni kilimo, mifugo, na uvuvi. Aidha, Mpango huu unalenga kukamilisha miradi mingi ambayo ilianza katika utekelezaji wa mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano (2021/22-2025/26), ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira 2025. Vile vile, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24 unatarajia kuleta matokeo chanya ikiwemo: kuimarika kwa ukuaji wa Pato la Taifa; kuimarika kwa miundombinu ya huduma za kiuchumi na kijamii hususan afya, elimu, maji na umeme; kudhibitiwa kwa kasi ya mfumuko wa bei; kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara; kuvutia ushiriki wa sekta binafsi; na kuimarika kwa maisha na ustawi wa jamii.

**Malengo na Shabaha za Uchumi Jumla kwa Mwaka 2023/24**

30. **Mheshimiwa Spika**, malengo na shabaha za ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2023/24, ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022;

(ii) Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi asilimia 7.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 14.4 mwaka 2022/23

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 11.5 mwaka 2022/23;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

31. **Mheshimiwa Spika**, misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(iii) Kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kushuka kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini;

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani; na

(vi) Kuendelea kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii.

**Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2023/24**

**32. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Miradi hiyo inajumuisha: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) – Njombe; Daraja la JPM - Kigongo – Busisi (Mwanza); Ujenzi wa barabara na Madaraja Makubwa; kuendeleza Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo; na Programu ya Kuendeleza Ujuzi Adimu.

**33. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/24 Serikali itatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia maeneo matano (5) ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26 kama ifuatavyo:

**(a) Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi**: Katika eneo hili nguvu kubwa itaelekezwa kwenye miradi inayolenga kuboresha miundombinu, kuimarisha mifumo ya kitaasisi pamoja na miradi inayolenga kuleta mapinduzi ya TEHAMA. Utekelezaji wa miradi hiyo utaimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza utulivu wa kiuchumi. Miradi hiyo ni pamoja na:

(i) **Barabara**: miradi itakayotekelezwa ni ile inayolenga kufungua fursa za kiuchumi, za kuunganisha Tanzania na nchi jirani pamoja na za kupunguza msongamano ikiwemo: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499); Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220); na Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235); Handeni – Kibaya – Singida (Km 460).

(ii) **Madaraja Makubwa:** kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Daraja la Sibiti (Singida); na kuanza ujenzi wa Madaraja ya

Chakwale (Morogoro), Nguyami (Morogoro) na Mbambe (Pwani).

(iii) **Usafiri wa Majini:** Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu ikijumuisha: Kukamilisha ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu; kukamilisha ukarabati wa meli za MV Umoja na MT. Sangara; kuanza ujenzi wa meli mpya (Wagon ferry) katika Ziwa Victoria na meli mpya (Barge/Cargo ship) ya kubeba shehena ya mizigo katika Ziwa Tanganyika

(iv) **Bandari: Bandari ya Dar es Salaam**, kuendelea uchimbaji wa kina na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli na uboreshaji wa Gati Na. 8 – 11 na kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati Na. 12 -15; **Bandari ya Tanga**, kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Tanga na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya gati la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga); **Bandari ya Mtwara**, kuendelea na maboresho ya maeneo ya kuhudumia shehena za mizigo; **Bandari ya Bagamoyo**, kuanza maandalizi ya utekelezaji wa bandari; kuendelea na uboreshaji wa Bandari za Bukoba, Kemondo Bay na Mwanza North katika **Ziwa Victoria**; Kuendelea na ujenzi wa Access Road, Cargo Shed, Passenger Wharf and Lounge) pamoja na kuendelea na ujenzi wa Passenger Lounge na ukuta wa mizigo wa Lighter Quay katika Bandari ya Kibirizi na gati la Bandari ya Ujiji katika **Ziwa Tanganyika.**

(v) **Usafiri wa Anga:** Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Msalato, Mwanza, Mtwara, Kigoma, Sumbawanga, Shinyanga, Songwe, Mpanda, Tabora, Bukoba, Geita, Iringa, Ruvuma (Songea), Simiyu, Lake Manyara, Tanga, Moshi, Lindi na Mara (Musoma), Dodoma, Manyara na Arusha.

(vi) **Nishati**: Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kufua, kusafirisha na kusambaza umeme (nishati) ikiwemo: Kufua Umeme wa Maji Kikonge (MW 300); Kufua Umeme wa Maji Malagarasi (MW 49.5); Uimarishaji wa Gridi ya Taifa

(National Grid Stabilization); Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi; na Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 – North – West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi).

(vii) **Mapinduzi ya TEHAMA**: Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya Anwani za Makazi na Tanzania ya Kidijitali; kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA; na ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA.

**(b) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Huduma**: miradi itajielekeza katika kukuza sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. Miradi hiyo ni pamoja na: programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili; mradi wa kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo na mazao yake; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kwa kujenga skimu mpya 25 na kukarabati skimu 30 zenye jumla ya hekta 95,005 katika mikoa mbalimbali; na kuimarisha huduma za ugani. Aidha, msukumo wa pekee utawekwa katika kuboresha Viwanda Vidogo – SIDO na Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC; kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na kongani za viwanda.

**(c) Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za maendeleo. Kipaumbele kitakuwa katika kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint); kuboresha huduma za biashara na masoko; kuratibu programu za kuimarisha mifumo ya udhibiti wa uwekezaji inayolenga katika kupunguza gharama za uwekezaji nchini; na kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo kwa wawekezaji katika Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja.

**(d) Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Miradi itakayotekelezwa imelenga kuboresha maisha ya watu pamoja na kuimarisha ustawi wa jamii. Miradi hiyo ni pamoja na: miradi ya afya kwa kuimarisha huduma za afya katika hospitali za kitaifa, hospitali

za rufaa za kanda na mikoa; hospitali za halmashauri; vituo vya afya na zahanati; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kugharamia elimumsingi na sekondari bila ada; utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; kuendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa na wilaya, miji midogo na vijijini; na kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi pamoja na kuimarisha mipaka ya kimataifa.

**(e) Kuendeleza Rasilimali Watu:** Kuendelea na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya kukuza ujuzi nchini ili kuongeza ajira kwa vijana kwa kutoa mafunzo ya ufundi na stadi za kazi kupitia programu mbalimbali zikiwemo: kuimarisha programu ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini; kuboresha mfuko wa maendeleo ya vijana; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu; na kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha.

**34. Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kuwa, sekta ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) ilipewa jukumu la kugharamia shilingi trilioni 21 sawa na asilimia 17 ya Bajeti ya kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Katika kutekeleza jukumu hilo la kimkakati, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na wadau wengine imeweza kubainisha jumla ya miradi 48 inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

**35. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 miradi mikubwa ambayo ipo kwenye maandalizi ya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ni pamoja na: kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika mikoa ya Dodoma (Zuzu MW 60) Kilimanjaro (Same MW 50) na Singida (Manyoni MW 100); Mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia maji wa Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222); mradi wa miundombinu ya kusambaza gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara ;na mradi wa kusafirisha umeme wa Tanzania – Malawi – (TAMA) *interconnection* wenye urefu wa km 82.

**36. Mheshimiwa Spika,** Miradi mingine ni: Reli ya Dar es Salaam (Dar -Commuter Rail); Reli ya Mtwara-Bamba Bay; Uendeshaji

wa Reli (Rolling stocks); Uendeshaji wa Barabara ya haraka (expressway) kutoka Igawa-Tunduma; Barabara za kupunguza msongamano katikati ya Jiji la Dar es Salaam (Inner and Outer Ring Roads); Barabara za haraka kutoka KibahaChalinze-Morogoro hadi Dodoma na kuunganisha Jiji la Dodoma na Dar es Salaam kwa barabara za haraka; Bandari kavu katika eneo la Kisiwa/Mgao – Mtwara; na Kuboresha na Upanuzi wa bandari katika Ziwa Victoria - Mwanza na Nansio - Ukerewe.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Umuhimu wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Serikali inaendelea na hatua za mwisho za utekelezaji wa takwa la kisheria la kuanzisha Kituo cha Ubia (PPP-Center) kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika usimamizi wa jukumu hili kubwa na la kimkakati. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.82 kwa ajili ya maandalizi ya miradi ya Ubia (PPP Faciliatation Fund-PPPFF) ili kuwezesha maandalizi ya maandiko ya miradi ya maendeleo yenye mvuto wa uwekezaji wa sekta binafsi nchini. Vile vile, Serikali imejipanga kukabili changamoto za kisheria, kimfumo na kiutendaji zilizochangia kuchelewa kwa miradi ya ubia kwa zaidi ya muongo mmoja. Katika kuhakikisha hilo, Serikali iliwasilisha muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta Umma na Binafsi, Sura Na 103 ambapo tarehe 13 Juni, 2023 Bunge lako Tukufu liliuridhia na kuupitisha. Hivyo, ni rai yangu kwa Mawaziri wenzangu na watendaji wa Serikali kutumia fursa hiyo kushirikiana na Sekta Binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo nchini.

**38. Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2023/24 yanapatikana katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Tatu.

**Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2023/24 na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

**39. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango unaweza kuathiriwa na vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: mabadiliko ya viwango vya riba za mikopo katika soko la ndani na nje; uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu; migogoro na hali ya siasa inayojitokeza

kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa; na kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na vihatarishi husika, Serikali inalenga kuchukua hatua mbalimbali ikijumuisha: kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ili kupunguza utegemezi katika misaada na mikopo kutoka nje; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira ili kudhibiti uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu; kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani; na kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo.

**Ugharamiaji wa Mpango 2023/24**

**41. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Serikali imetenga shilingi bilioni 14,077.2 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,795.1 sawa na asilimia 77.0 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.1 sawa na asilimia 23 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Fedha hizi zitakusanywa kutoka katika mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo nafuu, mikopo ya ndani na mikopo ya nje yenye masharti ya biashara. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

**Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango 2023/24**

**42. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyokusudiwa, suala la ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji limeendelea kupewa msukumo wa pekee katika shughuli za kila siku za Serikali. Katika kutekeleza hilo, mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 211 kati ya lengo la miradi 300 iliyopangwa kufuatiliwa katika kipindi cha mwaka 2022/23.

Aidha, miradi iliyofuatiliwa ilihusisha miradi kutoka sekta za ujenzi, uchukuzi, viwanda, elimu, afya, utawala bora, kilimo, mifugo, maji na biashara inayotekelezwa na serikali pamoja na sekta binafsi.

**43. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 kupitia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2022; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha; Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 Kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti.

**44. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Sheria hizo na miongozo hiyo, Serikali pia inaendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ambapo hatua iliyofikiwa ni kukamilika ukusanyaji na uchambuzi wa maoni kutoka kwa wadau na kuanza kwa uandishi wa Taarifa ya Kizio (*Baseline Report)*. Kukamilisha kwa uandishi wa Taarifa Kizio kutajenga msingi wa uandishi wa Sera ambayo inatarajiwa kutatua changamoto za uratibu wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini chini. Aidha, shughuli ya ufuatiliaji na tathmini ni suala mtambuka na inahusisha wadau mbalimbali katika ngazi tofauti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kushirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi katika kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo wa

Mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na: kuandaa Mpango Kazi wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini; kutenga rasilimali fedha zitakazowezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini; kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mipango kazi iliyowekwa; na kuendelea kuwajengea uwezo watumishi katika tasnia ya ufuatiliaji na tathmini.

**46. Mheshimiwa Spika**, Serikali inazielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuaandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha taarifa husika Wizara ya Fedha na Mipango.

**MAJUMUISHO**

**47. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya ***"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".*** Utekelezaji wa Mpango utaendelea kuimarisha mahusiano ya kisiasa, ulinzi na diplomasia ya uchumi na nchi nyingine, kuendelea kutekeleza kwa kasi miradi ya maendeleo, kuchochea uwekezaji viwandani hususan kwa kutumia rasilimali watu na malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwemo mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, madini, misitu na gesi asilia, kuimarisha viashiria vya uchumi jumla, kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani ikiwemo kuimarisha majadiliano na wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuendeleza mashirikiano na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**48. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na ya kimkakati, kuimarisha sekta za uzalishaji ili kutoa

mchango katika ukuaji wa uchumi, kufungua fursa zaidi za ajira na maendeleo ya watu, kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwemo huduma za afya, elimu, umeme na maji safi na salama mijini na vijijini pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi ya uwekezaji na biashara kwa ajili ya masoko ya kimataifa hususan ya nchi jirani.

**49. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na jitihada za kukabiliana na athari za majanga mbalimbali ya asili na yasiyo ya asili yakiwemo mabadiliko ya tabianchi, magonjwa na vita. Aidha, tutaendelea kuimarisha utekelezaji kwa kuweka mipango madhubuti ya kupunguza athari zitokanazo na vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ikiwemo kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi pamoja na kukabiliana na Athari za UVIKO–19.

**HITIMISHO**

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Elimu na Tafiti, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na Wananchi wote kwa namna walivyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Wadau hao wamekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa msingi huo, ninawaomba na kuwasihi wadau wote waendelee kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na Rais shupavu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**51. Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Viongozi wote wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Aidha, hotuba hii isingeweza kukamilika bila jitihada kubwa zilizofanywa na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, kwa

dhati ya nafsi yangu naomba nitoe shukrani za pekee kwa Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Natu El-Maamry Mwamba kwa kujitoa usiku na mchana kukamilisha kwa wakati na kwa ubora Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24.

**52. Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla kwa kutenga muda wao kunisikiliza. Aidha, napenda kuwataarifu wadau wote kuwa, hotuba hii pamoja na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ni ***www.mof.go.tz***.

**53. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24.

**54. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana. Nimeletewa ujumbe hapa kwamba wapo wageni ambao hawakutangazwa Watoto wa Mheshimiwa Kunti Majala, haya karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja kua imeungwa mkono tutaendelea baadaye kama ilivyo ada. Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili jioni leo.

*(Saa 5.03 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)*

**15 JUNI, 2023**

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa ajili ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Wapambe wa Bunge sasa wamlete Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa Waziri wa Fedha na Mipango (Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba) Aliingia Ukumbini Akisindikizwa na Wapambe wa Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri karibu uwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2023/2024.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na nianze kwa maneno mawili ya utangulizi. La kwanza, namshukuru Mungu kwa afya njema mpaka muda huu tunapowasilisha Bajeti. La pili, Bajeti hii nawasilisha imebeba maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, alivyokusudia kugusa maisha ya Watanzania na kubadilisha maisha ya Watanzania ili kuweza kutengeneza ajira na kuwaondolea umaskini Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, popote pale mtakapoona mapungufu, hayo ni mapungufu yetu sisi Wizara ya Fedha katika kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais, sisi ni binadamu mtakuwa na

muda wa kutushauri ili tuweze kutafsiri sambamba na maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kifungu cha 124(4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2023 ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa ikiwemo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) ambao umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Pia umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2022 - 2027; Makubaliano mengine ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia pamoja na Hotuba mbalimbali za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kulijalia Taifa letu amani, mshikamano, umoja chini ya Rais Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutimiza miaka miwili katika uongozi wake uliolenga mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amedhihirisha kuwa yeye ni kiongozi makini, mwadilifu, msikivu, mchapakazi na aliye na maono thabiti ya kuendelea kuliletea Taifa letu maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameendelea kutekeleza miradi ya zamani kwa miradi mipya, ameendelea kutekeleza miradi inayochochea uchumi kwa miradi ya huduma za jamii. Ameendelea kusimamia deni la Serikali na kulipa madai yaliyopita, ameendelea kufanyia kazi maslahi ya watumishi wa umma na wastaafu na ameendelea kukuza demokrasia nchini na diplomasia ya uchumi. Hali hiyo inadhihirisha kuwa hakuna kilichosimama bali vimeongezeka isivyoweza kusimuliwa kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee pia naomba nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Komredi Daniel Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, kwa namna anavyofuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Narudia hiyo, kwa namna anavyofuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Mwaka 2025, kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziara hizo zimekuwa na tija kubwa kuchochea kasi ya ukamilishwaji wa miradi ya maendeleo iliyokuwa imekwama. Nawaelekeza watendaji wote wa Serikalini, kutekeleza maelekezo yanayotolewa na chama na kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wawakilishi wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inasonga mbele licha ya nchi zote duniani kupita kwenye msukosuko wa kiuchumi. Jarida la Shirika la Fedha la Kimataifa la Aprili 2023, limeonesha kuwa uchumi wa Tanzania unatarajiwa kufikia dola za Kimarekani bilioni 85.4 kwa mwaka 2023 kutoka dola bilioni 69.9 mwaka 2021. Tanzania sasa imepanda hadi nafasi ya sita ikilinganishwa na nchi zingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiongozwa na Kenya ambayo ina dola bilioni 116, Ethiopia ina dola bilioni 120, Angola ina dola bilioni 121.4, Afrika Kusini ina dola bilioni 405.7 na Nigeria yenye dola bilioni 477.4. Nchi nyingine ambazo ziko chini ya Tanzania kiuchumi ni Ghana yenye dola bilioni 72.8, Cote D'Ivoire yenye dola bilioni 70.0, DRC yenye dola bilioni 62.8 na Uganda yenye dola bilioni 48.8.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeshaingia sita bora tunaelekea fainali. Hivyo, Watanzania tunapotoa mifano ya wapi tunapoelekea, tuyajue mataifa yalioko mbele yetu na kwa programu hizi alizoanzisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Uenyekiti wa CCM, chini ya uongozi wa CCM, Tanzania itaweza kuzivuka nchi ambazo ziko mbele yetu siku siyo nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianza kufufua mchakato mpya wa kufanyia tathmini uwezo wa nchi yetu kukopa na kukopesheka *(sovereign credit rating),* mchakato ule ambao ulianza mwaka 2008, ambapo zoezi hilo halikukamilika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mdororo wa uchumi pamoja na mambo mengine ya kuyumba masoko ya fedha duniani. Hata hivyo, chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imefanikiwa kukamilisha zoezi hilo lililokuwa ni kikwazo katika ufuatiliaji wa fedha na mitaji kwenye masoko ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo Machi 2023, kampuni za *Fitch Ratings* na *Moody's Investors Service* zilianza zoezi la kuifanyia nchi yetu tathmini kukopesheka katika masoko ya fedha za kimataifa. Zoezi hilo lilikamilika ambapo kampuni ya *Moody's Investors Service* ilichapisha matokeo ya tathmini hiyo mwezi Mei, 2023 na kampuni ya *Fitch Ratings* ilitoa matokeo mwezi Juni, 2023. Kwa

mujibu wa matokeo hayo, Kampuni ya *Moody's Investors Service* imeipa Tanzania daraja la *B2 POSITIVE* na Kampuni ya *Fitch Ratings* daraja la *B POSITIVE*, ambayo yanaashiria taswira chanya kwa nchi yetu kimataifa. Matokeo hayo ni bora kuliko nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, zote za Afrika Mashariki na Kati, Tanzania iko juu kwenye matokeo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi, usimamizi makini wa deni la Taifa, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa pamoja na kuleta maridhiano ya kisiasa ndani ya nchi. Kukamilika kwa zoezi hilo, kutaiwezesha nchi kutambulika katika masoko ya fedha ya kimataifa na hivyo kuongeza sifa za kuvutia uwekezaji na kuongeza wigo wa upatikanaji kwa fedha kwa miradi ya Serikali pamoja na miradi ya sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafanikio tunakumbuka kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alishika madaraka ya kuongoza nchi katika kipindi ambacho dunia ilikuwa inapita katika msukosuko kama ambavyo nimetoka kueleza. Pamoja na kupokea kijiti cha uongozi katika kipindi cha majanga hayo, uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan umetekeleza sera na mikakati mbalimbali iliyowezesha uchumi wa nchi yetu kuhimili majanga hayo ikiwemo utekelezaji madhubuti wa sera za kifedha na sera za kibajeti. Ni dhahiri kuwa, utekelezaji wa sera na mikakati hiyo umeleta mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha uongozi wa Awamu ya Sita. Mafanikio haya yalishaelezewa na Wizara za kisekta naomba na mimi niyaelezee kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mapato, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka na kufikia shilingi trilioni 24.40 mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na shilingi trilioni 20.59 mwaka 2020/2021. Hadi kufikia Desemba 2022, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipata kiasi cha shilingi trilioni 2.63 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kukusanywa tangu Mamlaka ya Mapato ianzishwe mwaka 1996. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwenendo huu mzuri na ni ishara ya Serikali ya Awamu ya Sita kuwa ipo makini katika kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato, kuzingatia sheria na miongozo na taratibu pamoja na jitihada za kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta za uzalishaji; kwa kutambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi vijijini ambao kilimo ndiyo msingi wa ustawi wa maisha ya wananchi wetu, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea na dhamira yake ya kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294.0 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi shilingi bilioni 954 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na sasa imeongeza na kufikia shilingi bilioni 970.8 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bajeti hii kumewezesha kutekeleza miradi mbalimbali kama ambavyo imeelezewa kwa kina na Wizara ya kisekta. Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa chakula kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa maghala 14 na vihenge 20 kwa ajili ya kuhifadhi nafaka. Hatua hizi zilichangia utoshelevu wa chakula kufikia 114% kwa mwaka 2022/2023. Serikali itaendelea kuuwezesha Wakala wa Uhifadhi wa Chakula *(NFRA)* kununua mazao kutoka kwa wakulima. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya tani 400,000 zinatarajiwa kununuliwa na *NFRA*. Lengo la Serikali ni kuwa na akiba ya chakula inayokidhi mahitaji yasiyopungua miezi minne kama tunavyoongelea kwenye upande wa akiba ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea ili kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa gharama nafuu ambapo hadi Aprili 2023, shilingi bilioni 214.8 zimetolewa ikijumuisha fedha za ndani na fedha za nje. Kutolewa kwa ruzuku hiyo kuliwezesha wakulima kupata mbolea kwa bei ya kati ya Sh.50,000 hadi Sh.70,000 kwa mfuko wa kilo 50, badala ya bei ya soko ya wastani wa Sh.140,000.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia katika kuimarisha sekta ya kilimo, sote tumeshuhudia maendeleo mazuri ya utekelezaji wa miradi ya kilimo. Serikali itaendelea kuongeza fedha kwenye sekta hii kadri ufanisi utakavyoongezeka ikiwa ni motisha kwa utendaji mzuri. Hivyo, nasisitiza sekta izingatie utaratibu wa *Performance for Results (P4R)* na hatua hii inaweza kuongeza fedha zaidi ya utekelezaji wa miradi ya kilimo na kufikia shilingi trilioni 1.27 katika mwaka wa fedha. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia iko kazini, tunataka kupiga vita umaskini kwa vitendo na tutaelewana tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mifugo na Uvuvi; katika kuimarisha sekta hizo Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo wanatekeleza miradi mbalimbali kama ambavyo iliainishwa na Wizara ya kisekta, ambapo matokeo ya mafanikio yake yamepatikana.

Mheshimiwa Spika, katika uvuvi Serikali imeimarisha Sekta ya Uvuvi na kuendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara katika taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* iliyoko Dar es Salaam, ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa, kujenga na kukarabati miundombinu ya ukuzaji viumbe maji na kuendelea na ujenzi wa mialo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Mifugo, mafanikio ambayo yameshakamilika ni pamoja na kukamilika majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho mengine 160 katika Mikoa 25. Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa vituo atamizi nane na kutoa ujuzi wa unenepeshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ambazo wanapitia wafugaji hapa nchini. Tatizo la malisho, maji, maeneo ya malisho kutumika kwa shughuli nyingine za kiuchumi, kama vile kilimo, tija ndogo ya shughuli za mazao yanayotokana na mifugo na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametuelekeza tuyafanyie kazi masuala haya Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Mifugo. Mifugo siyo laana wala siyo umasikini katika nchi yetu, mifugo ni utajiri katika nchi yetu. Wengi tuna historia zinazofanana, mimi nimesomeshwa kwa mifugo na bado nakumbuka hata rangi za ng'ombe waliouzwa na majina yao wakati naenda shule. Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, itafanya tathmini ya kina kwa utaratibu ambao utakuwa shirikishi kwa kuwashirikisha wafugaji nchi nzima kupata maoni na namna bora ya kujenga na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya ufugaji na miundombinu ya mifugo sambamba na kutekeleza mapendekezo yaliyowasilishwa na Wizara ya kisekta kuhusu kuboresha sekta ya mifugo. Kuna mabadiliko makubwa yanakuja kwenye sekta hii ya mifugo na uvuvi ili kuwezesha sekta hizi ziweze kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini wa Watanzania na kukuza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini katika kuongeza thamani na kudhibiti utoroshaji wa rasilimali za madini, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuanzisha vituo vya madini ambapo jumla ya vituo vipya 40 vimefunguliwa katika kipindi cha Awamu ya Serikali ya Sita na hivyo kufanya vituo vya madini kufikia 93. Kukamilisha ujenzi wa vituo vya umahiri katika shughuli za madini vya Songea, Mpanda na Chunya. Kununua madini ya Tanzanite yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2.2 pamoja na mitambo midogo mitano ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Katika mwaka wa fedha ujao, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya madini ili iweze kuchangia zaidi kwenye uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vya kusafishia dhahabu *(refineries)*, Serikali itaendelea kuweka vivutio kwa viwanda hivyo ili viweze kupata malighafi ya kutosha. Katika kutekeleza hilo, Serikali imepunguza mrabaha wa madini yanayouzwa kwenye *refineries* kutoka asilimia sita hadi asilimia nne. Aidha, Serikali itaendelea kuchambua sera, sheria, taratibu za kiutawala na za kikodi ili kuwezesha dhahabu inayozalishwa kwenye migodi yetu isafishwe kabla ya kuuzwa nje.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekamilisha taratibu za kununua dhahabu kupitia Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuanzisha akiba ya dhahabu hapa nchini *(Gold Reserve)*. Tunataka tunapotaja akiba ya fedha za kigeni tutaje na akiba ya dhahabu tuliyonayo. Hatua hii itawapatia wachimbaji bei nzuri zaidi na kuimarisha sarafu ya nchi yetu. Hii ni baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia bajeti ya Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Fedha na hotuba mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kukwamua mradi wa Liganga na Mchuchuma pia Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwenye eneo la mradi na taratibu za kulipa zimeanza kama ambavyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maliasili na Utalii. Pamoja na sekta hiyo kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na janga la UVIKO-19, hatua ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutangaza sekta ya utalii kwa vitendo kupitia programu ya *Royal Tour*, ambayo imekuwa na mafanikio makubwa, mafanikio hayo yameongeza idadi ya watalii wa nje na wa ndani na kufikia 922,692 kwa mwaka 2021 hadi watalii 1,454,920 kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mazingira ambayo yamewezeshwa kwa wananchi kwa upande wa kodi kupitia mwongozo mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023. Msamaha huo ulilenga kuwapunguzia wananchi gharama na hivyo umewezesha ulipaji wa deni la msingi. Katika kukabiliana na changamoto za gharama za umilikishaji ardhi, Serikali inafanya mapitio ya tozo na ada mbalimbali ili kutoa unafuu wa umiliki pia kuongeza kasi, kama nitakavyosema hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu wezeshi. Kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, Serikali imeendelea kutoa fedha

kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara, ikiwemo barabara za kufungua fursa za kiuchumi na kuunganisha na nchi. Jumla ya kilometa 1,151.37 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 1,483.74 zinaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami na kilometa 1,124.3 za barabara za Mikoa zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Vilevile, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetoa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara inayotoka Kibaha – Morogoro kilometa 205 na kipande cha Morogoro hadi Dodoma ili iweze kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma ambapo ni kilometa 112.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 1.43 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami kilometa 798.1 na changarawe kilometa 23,251 pamoja na madaraja 177 na makalavati 1,002 kupitia *TARURA*. Hayo ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya kujenga barabara za kudumu za mitaa na vijijini ili kuondokana na utaratibu ambao barabara hizo zimekuwa zikiharibika kila baada ya mvua kunyesha. Tumejifunza kutokana na utaratibu wa *Performance for Results (P4R)* unaotumika kwa fedha tunazopokea kutoka kwa wafadhili na utekelezaji wa miradi ya elimu pamoja na maji. Hivyo, ili kuboresha usimamizi wa rasilimali, eneo hili litapatiwa fedha kwa utendaji wake kwa kuongezewa fedha kadri ufanisi unavyoendelea na tumeshaongea na Wizara ya kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaweza kuongeza fedha zaidi ya utekelezaji wa miradi ya *TARURA* kwa kiasi cha shilingi bilioni 350 zaidi ya zile ambazo zilikuwa zimeombwa. Ongezeko la fedha hizi linalenga kujenga barabara ambazo ni kiungo muhimu cha kufungamanisha maeneo ya uzalishaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, Mama yuko Kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sekta ya Uchukuzi Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya

kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo bandari, viwanja vya ndege. Hadi kufikia Aprili, 2023, ujenzi wa njia za reli kipande cha Dar-es-Salaam – Morogoro utekelezaji wake umeshafikia zaidi ya asilimia 98.14, kipande cha Morogoro – Makutupora zaidi ya asilimia 93.83 na kipande cha Mwanza – Isaka zaidi ya asilimia 31. Serikali imeanza ujenzi wa kipande cha Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka na kipande cha Tabora – Kigoma. Mchakato wa ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa upande wa Uvinza – Malagarasi na badae Msongati na baadae kwenda Gitega hadi Uvira kule DRC unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nishati. Mafanikio katika sekta hii ni pamoja na kuendelea na ugharamiaji wa ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji wa nishati katika Bwawa la Mwalimu Nyerere ambapo ufanisi umeshafika zaidi ya asilimia 86.89, Rusumo umefika zaidi ya asilimia 99 kwa upande wa nishati ya umeme kwa gesi *Kinyerezi Extension*. Aidha, Serikali itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya usambazaji wa umeme kwa kuunganisha katika Gridi ya Taifa Mkoa wa Kigoma, upande wa Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu pamoja na Buhigwe pamoja na Wilaya za Ngara na Biharamulo za Mkoa wa Kagera. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme unaozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea na usambazaji wa umeme vijijini ili ifikapo 2025, vijiji vyote viwe vimefikiwa na umeme, na katika hatua hiyo, hadi Aprili 2023 kiasi cha shilingi bilioni 903.8 kimetolewa na zaidi ya asilimia 81 ya vijiji vimefikishiwa umeme. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kuendelea, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini na baadhi ya ngazi za vitongoji, hii ni ishara kwamba Mama amedhamiria kufikisha umeme nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mama yuko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi wa kidijitali katika mwaka wa fedha 2023, Serikali itaendelea kusimamia mapinduzi ya kidijitali nchini. Mapinduzi ya kidijitali ndiyo

yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika uchumi wa kidigitali, sekta zenye kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano na mwingiliano zimeelekezwa kuboresha mazingira ya kidijitali. Katika kufikia azma hii, Serikali itatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo, mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano, mradi wa Tanzania ya kidijitali na mradi wa kuendelea na ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za jamii, nikianza na elimu. Programu ya Elimu Bila Malipo, Msingi na Sekondari imeendelea kuboreshwa, ambapo Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza jambo hiolo la kihistoria kwa kuwafuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha Tano na Sita. Vilevile Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.41 kwa wanafunzi wa elimu ya juu na pia inaendelea na maboresho ya miundombinu ya vyuo ikijumuisha vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuondoa ada kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na Serikali kujiunga na vyuo vya ufundi vya Dar-es-Salaam, Mbeya pamoja na Arusha *Technical*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema pale nilipokuwa naanza kwamba, hotuba hii imebeba hisia za Mama namna anavyotaka kuwasaidia Watanzania, hasa watoto wa kimaskini. Narudia, napendekeza kuondoa ada kwa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne na kupangiwa na Serikali kujiunga na Vyuo vya Ufundi vya Dar-es-Salaam *Institute of Technology (DIT)*, Mbeya *University of Science and Technology (MUST),* Arusha *Technical College (ATC)*. Hatua hii inalenga kuongeza idadi ya wataalamu wenye ujuzi na elimu inayohitajika katika zama hizi za mapinduzi ya nne ya viwanda *(the 4$^{th}$ Industrial Revolution)*. Mama yuko Kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, toleo la Mwaka 2023, mabadiliko ya mitaala yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo Serikali inalenga kutoa elimu ya amali kwa ngazi zote kuanzia shule za awali za elimu ambayo inamwezesha kijana wa Kitanzania kujiajiri au

kuajiriwa na hivyo kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa hili. Hivyo, napendekeza kuanzisha programu ya mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa na Serikali kusoma kwenye vyuo vya kati vya elimu katika fani za kipaumbele ambazo ni sayansi, afya, ufundi na ualimu. Hatua hii itaanza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo kwa mwaka wa masomo wa 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia: Napendekeza kuanzisha programu ya mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa na Serikali kusoma kwenye vyuo vinavyotoa elimu katika fani za kipaumbele ambazo ni sayansi, afya, ufundi na ualimu. Hatua hii itaanza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo 2023/2024. Kwa wanafunzi hawa, Mama amewaona, Mama amewasikia. Mama yuko Kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upendo wa Mama yetu katika kuhuisha kwenye mikopo ya wanafunzi, pia aliamua kuongeza kiwango cha posho ya kujikimu kwa wanafunzi, maarufu kama *boom* kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka shilingi 8,500 ambayo ni ya siku nyingi sana hadi kufikia shilingi 10,000. Mafanikio mengine ni pamoja na kujengwa kwa vyumba zaidi ya 27,000 vya madarasa na kazi hiyo inaendelea. Pochi la Mama liko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afya. Katika kuboresha sekta ya afya, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali tano za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu ambapo hadi Machi 2023 jumla ya shilingi bilioni 45.3 zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kununua na kusambaza dawa, vifaa vya tiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya ambapo jumla ya shilingi bilioni 544.2 zimetolewa zikijumuisha shilingi bilioni 487.5 zilizotolewa kupitia Bohari ya Dawa *(MSD)*. Ni nia ya Serikali ya Awamu ya Sita kuona kuwa huduma za afya zinazidi kuimarika, hivyo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ikiwemo kuipatia mtaji *MSD* ili ifanye kazi kama bohari ya dawa na siyo kitengo cha

ununuzi wa dawa Serikalini. Kadhalika Serikali italipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* ili kuuwezesha kutoa huduma na mchango wake katika kuboresha huduma za afya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kuboresha miundombinu ya afya kupitia Mpango wa Kudhibiti Athari za Kiuchumi na Kijamii kutoka UVIKO-19 ambapo jumla ya shilingi bilioni 463 zimetolewa. Hizi zimetuwezesha kuwa na *EMD* 101 ambazo zimejengwa, *ICU* 70, nyumba za watumishi 150 na sasa mashine za *X-Ray* zikiwepo 169 za digitali, *CT scan* mashine 30, *MRI* 4 na magari ya kawaida 663.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuboresha huduma za afya zimeokoa kiasi kikubwa sana cha fedha za kigeni ambapo wagonjwa walikuwa wanategemea kutibiwa nje na sasa wanatibiwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maji. Katika kutekeleza dhana ya kumtua mama ndoo kichwani, Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuongeza bajeti ya sekta ya maji na kufikia shilingi bilioni 709.4. Fedha hizo zimefanikisha kufikisha miradi zaidi ya 80 ya usambazaji maji mijini na zaidi ya miradi 1,373 ya usambazaji wa maji vijijini. Serikali imesambaza seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika Mikoa 25. Sasa kila Mkoa unam tambo wake na seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Nitoe rai kwa Halmashauri, Miji, Majiji, kuchimba visima vingi kwa kadri iwezekanavyo kwa kutumia mapato ya ndani. Mmepewa mitambo ya mabilioni ya kuchimba visima na mabwawa kila Mkoa hivyo, itakuwa ni uzembe kwa kweli na ubinafsi kukosa shilingi milioni 15 kuchimba kisima. Anachokusudia Mama siyo tu kumtua mwanamke ndoo kichwani, bali ni kuiondoa kabisa ndoo, mtu atumie chombo cha maji tu kuchota na kupeleka pale anapopikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta zingine, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Serikali kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini imeendelea na jitihada za kupunguza umaskini nchini ambapo hadi Machi, 2023 jumla ya kaya 1,371,916 zilizokidhi vigezo kuingia katika Kipindi cha Pili cha Mpango kutoka

maeneo yote ulitekelezwa. Aidha, miongoni mwa ubunifu uliofanywa katika utekelezaji wa Mpango huo ni kutoa msaada kwa watu wenye ulemavu ambapo kaya yenye mtu mwenye ulemavu hupokea nyongeza ya shilingi 5,000 kwa mwezi. Hadi Mei 2023, takribani kaya 110,000 zenye wanakaya wenye ulemavu zimefanikiwa kupata katika mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kuingia kwake madarakani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonesha nia na jitihada kubwa katika kuboresha Utumishi wa Umma. Kwa upande wa utumishi wa umma baadhi ya mambo ambayo yamefanywa ni kupandisha madaraja watu 135,170 wenye sifa stahiki ambapo hadi Aprili 2023, jumla ya shilingi bilioni 177.9 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma, ambapo kima cha chini cha mishahara kiliongezwa kutoka shilingi 300,000 hadi shilingi 370,000. Mambo mengine ni kulipa madeni na malimbikizo ya mishahara kwa Watumishi wa Umma 94,293 ambapo zaidi ya shilingi bilioni 165.9 zilitumika hadi Aprili 2023. Jambo lingine ni kupunguza kodi ya mapato na ajira *Pay As You Earn* kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8, kuondoa tozo mbalimbali katika Mikopo ya Elimu ya Juu, kulipa madeni ya watumishi wa umma ambapo shilingi bilioni 42.7 zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa makato ya watumishi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, mwaka 2021/2022 Serikali ilianza kutekeleza maamuzi yake ya kukata makato yote ya kisheria kwenye chanzo ambacho Wizara ya Fedha na Mipango inawajibika kufikisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sensa ya Watu na Makazi, natoa taarifa kwamba tarehe 23 Agosti, 2022 matokeo ya awali ya sensa yalitangazwa na Mheshimiwa Rais na sensa hiyo ilifanyika kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa diplomasia ya uchumi, Serikali ya CCM, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na mashirika ya

kimataifa pamoja na majirani zetu. Kuimarika kwa ushirikiano huo ni matokeo ya jitihada za Mheshimiwa Rais katika kukuza uchumi, kufungua uchumi na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mahusiano na kuchochea uchumi na biashara katika nchi za Afrika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na utaratibu wa majadiliano ya utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mafanikio makubwa yameshajadiliwa sana katika hili na Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya Muungano, Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ni tunu ya Taifa letu na ndiyo utambulisho wetu duniani. Hivyo ni jukumu letu sote kuulinda, kuudumisha na kuuenzi. Katika kuendelea kudumisha Muungano, Serikali imekuwa ikifanya vikao mbalimbali kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa hoja za Muungano. Katika mwaka 2022/2023, Serikali ilijadili na kutoa hoja nane za Muungano na hoja nne zilipatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora, ulinzi na usalama, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ikijumuisha ujenzi wa ofisi jumuishi na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama hapa Dodoma. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa ofisi za uhamiaji katika Mkoa wa Geita na kuendelea na ujenzi katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Dodoma. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki kwa kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi na kuongeza idadi ya mahakimu na mawakili.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepeleka fedha nyingi sana kwenye Wizara, Mikoa na Wilayani kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi yetu. Natoa rai kwa Mawaziri wenzangu na watendaji wote Serikalini kufuatilia matumizi ya fedha hizi na kuchukua hatua stahiki pale fedha zinapotumika vibaya pasipo kusubiri

mbio za mwenge, ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa au Taarifa ya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa muundo wa utawala katika nchi yetu, kila ngazi ina uongozi wa Serikali ulio kamili. Tunao wa kupanga, tunao wa kufanya malipo, tunao wa kukagua, tunao wa kutathmini, tunao wa kuchunguza, tunao wa kukamata, tunao wa kupeleleza, tunayo magereza ya kuwaweka wahalifu na tunao watu wa kuhukumu. Kwa nini tunasubiri mbio za mwenge, ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa au Taarifa ya *CAG* na kila siku tunaishi huko huko? Nitoe rai kwa viongozi wetu wote Serikalini mlioko kule kwenye miradi, tusijidogoshe. Tumepewa mamlaka, tuyatumie kudhibiti rasilimali ili kazi anayoifanya Mama ya kutafuta fedha iwe na manufaa kwa wananchi aliowalenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwekezaji, viwanda na biashara, Serikali ya CCM imeendelea na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji wa kibiashara ili kuongeza ushindani wa Tanzania katika Soko la Kimataifa kwa kutunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania, kwa mfano Sheria Na. 10 ya Mwaka 2022; mafanikio mengine ni kuboresha sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania Sura 415, lengo likiwa ni kuondoa mwingiliano wa majukumu ya taasisi nyingine. Hatua hizo za Serikali zimelenga kuleta mafanikio mbalimbali ikiwemo kupunguza wastani wa siku za kupata vibali katika mamlaka za udhibiti kutoka siku 14 hadi siku tatu.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi nyingine, Serikali inakusudia kuondoa vikwazo vya kibiashara. Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kampuni, Sura 212 kwa kuongeza kifungu cha 452A ili kumpatia mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Biashara kwa kushauriana na Waziri wa Fedha, kutoa msamaha wa ulipaji wa ada ya kuwasilisha nyaraka nje ya muda.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na kutoa notisi. Notisi hiyo itaainisha kampuni zitakazohuisha taarifa zake kwenye mfumo ndani ya kipindi cha miezi 12 ambapo zitasamehewa asilimia 50 ya ada ya kuwasilisha nyaraka nje ya

muda. Marekebisho hayo yatazihusu kampuni ambazo zilisajiliwa kabla ya Mfumo wa *Online Registration* kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upatikanaji wa fedha za kigeni (Dola ya Marekani), katika mwaka 2022/2023, nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania, zilikumbwa na upungufu wa ukwasi wa Dola ya Marekani. Changamoto hii ilisababishwa na mambo makubwa mengi, yakiwemo maana, naomba niyataje. Mosi, vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambavyo vilisababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma duniani, hivyo kuongeza mahitaji ya Dola ya Marekani, ambayo ndiyo sarafu kuu katika biashara ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pili, Sera ya Fedha ya Marekani, ambayo ilijielekeza kwenye kupandisha riba, hali iliyosababisha wawekezaji wengi kuelekeza mitaji yao Marekani na kusababisha upungufu wa dola kwenye nchi nyingine. Tatu, kufunguka kwa shughuli za kiuchumi baada ya athari za UVIKO-19, jambo lililoongeza mahitaji ya Dola ya Marekani ikilinganishwa na kiasi kilichopo kwenye masoko. Sababu ya mwisho ni mabadiliko ya tabianchi, yaliyopunguza uzalishaji hasa katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa tunakabiliana na changamoto hii, Serikali imeamua kuchukua hatua mahususi za muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Miongoni mwa hatua hizo ni mkakati wa kuongeza uzalishaji ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi *(import substitution initiative)*. Katika kutekeleza hili, Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na wazalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda pamoja na utalii ili kuongeza thamani ya bidhaa na kuhakikisha kuwa tunaongeza tija katika uzalishaji wetu.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuinua sekta binafsi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara, Serikali ya CCM chini ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeamua kuhuisha mifuko ya udhamini ya mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee Scheme)* na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo

na wa Kati *(Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuboresha mazingira ya biashara, hususan katika sekta zinazoingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana pia na tatizo la upungufu wa dola, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya biashara ikiwemo kutatua changamoto katika biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nchini. Hii ni pamoja na kuchukua hatua madhubuti katika kutatua kilio cha baadhi ya wamiliki wa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni, hasusan katika Mkoa wa Arusha na maeneo mengine, ambao hawakuridhishwa na tathmini ya kodi iliyofanywa mwaka 2018/2019. Hivyo, Serikali ilipitia upya tathmini hiyo na kuwezesha baadhi ya wamiliki wa maduka kurejeshewa kiasi cha Shilingi bilioni 8.9 ambazo zilikuwa zimelipwa kama kodi kupitia tathmini ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2023, Serikali ilikuwa imetoa leseni kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni nane yenye matawi 36, ambapo matawi 24 yamefunguliwa Tanzania Bara na matawi 12 yamefunguliwa Zanzibar. Aidha, Benki Kuu inaendelea kupokea, kuchambua na kutoa leseni kwa wamiliki wanaokidhi vigezo ili kuweza kuongeza maduka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia pia kuimarisha zaidi mazingira ya biashara kwa kufanya mapitio ya Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya Mwaka 2019 ikiwemo mtaji. Lengo likiwa ni kurekebisha masharti yaliyopo kwa sasa ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23. Katika Bajeti ya Mwaka 2022/2023, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 41.48 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya Shilingi trilioni 32.43 zilipatikana kutoka vyanzo hivyo. Kwa upande wa matumizi, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya Shilingi trilioni 41.48 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka

2022/2023. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa Shilingi trilioni 32.43.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la Serikali, hadi kufikia Aprili, 2023, deni lilikuwa shilingi trilioni 79.10, sawa na ongezeko la asilimia 13.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 69.44 Aprili, 2022. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 27.94, sawa na asilimia 35.3 ya deni lote. Ongezeko la deni hili linatokana na kasi ya utekelezaji wa miradi hasa ya kimkakati, ikiwemo Reli ya Kisasa, *Standard Gauge*.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika Desemba, 2022 inaonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Matokeo ya sasa ya deni la Serikali kwa pato la Taifa ni asilimia 32.5 wakati ukomo ni asilimia 55. Tathmini kwa deni la nje ikilinganishwa na pato la Taifa ni asilimia 18.1 wakati ukomo ni asilimia 40; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 120 wakati ukomo ni asilimia 180.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye Dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Mpango huo ni mwendelezo wa dira nyingine zilizopita.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wake mikakati tuliyoiweka ya kuongeza mapato ni pamoja na kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji ikiwemo kuendelea kufanya maboresho ya sheria mbalimbali, kuongeza wigo wa mapato, kuimarisha na kuhimiza matumizi ya TEHAMA, kuendelea kusimamia Wizara na taasisi za Serikali kutumia mifumo, kusimamia matumizi sahihi ya *EFD,* kudhibiti misamaha ya kodi isiyo na ulazima, kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuimarisha ukusanyaji, kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi, kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha uwekezaji kwenye soko la ndani la dhamana za Serikali, kutumia fursa iliyopatikana kutokana na zoezi la *credit rating,* kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa vyanzo mbadala pamoja na mengine.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua migogoro na kuhakikisha haki inatendeka baina ya walipa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali ya CCM chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, imekamilisha taratibu za uanzishwaji wa Ofisi ya *Tax Ombudsman* ambaye ni Msuluhishi wa Masuala ya Kikodi, na tayari yuko kazini kwa ajili ya kutekeleza masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu ni pamoja na kutekeleza miradi ya umwagiliaji pamoja na kujenga mabwawa 100 ya kimkakati, ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *(SGR)*, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, kuzalisha umeme kwa kutumia maji kupitia Bwawa la Mwalimu Nyerere, kukamilisha ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa maji kwa upande wa Ruhudji (MW 358), ujenzi wa Daraja la J. P. Magufuli (Kigongo – Busisi), ujenzi wa barabara na madaraja makubwa, na kuendeleza kanda maalum za kiuchumi ikiwemo maeneo maalumu la uwekezaji ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sanjari na miradi ya kielelezo inayoendelea, utekelezaji wa miradi mingine kwa mwaka wa fedha 2023/2024 utazingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama ambavyo tumeuelezea.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye hatua za maboresho wa mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato, naomba nisisitize masuala mahususi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 138(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania inatoa masharti ya kutoza kodi. Hakuna aina yoyote ya kodi itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria, uliotiliwa nguvu ya kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nchi zote zilizoendelea duniani zinaendeshwa kwa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Wastani wetu wa kulipa kodi bado siyo mzuri sana ukilinganisha na ukuaji wa uchumi. Ongezeko la watu na ongezeko la mahitaji, yanakwenda kasi kuliko makusanyo yetu. Mathalani, kwa mwaka

wa fedha 2021/2022, walipakodi waliosajiliwa walikuwa 4,455,028 ambapo kati ya hao wenye *TIN* za biashara ni 1,641,173. Hata hivyo, katika kipindi hicho, takribani shilingi trilioni 16.75, sawa na asilimia 80 ya mapato ya *TRA* yalilipwa na idadi ndogo ya walipa kodi, takribani asilimia 20 tu ya walipa kodi wote. Hii inasababisha wale wanaolipa kodi wabebe mzigo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na ukweli kuwa idadi ya walipakodi walioandikishwa ni ndogo, bado kuna mwamko mdogo kwenye ulipaji Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Kodi ya Mapato *(Income Tax)* na Kodi ya Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)*. Jambo hilo linasababisha viwango vya kodi kuwa vikubwa kwa kuwa mzigo huo unabebwa na walipakodi wachache.

Mheshimiwa Spika, kwa wauzaji, kodi imekuwa ikitumika kama *discount rate* ambapo muuza duka akitaka kumpunguzia mtu bei, anamtajia kwamba aondoe kile kiasi cha kodi, ambapo muuza duka akitaka kupunguza bei kwa mteja anamwuliza kama ampe bei yenye risiti ya *TRA* au ampe bei ya bila risiti. Kwa Hiyo, kodi ya Serikali inatumiwa kama kiwango cha kupunguza bei *(discount rate)*. Hili ni kosa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine wafanyabiashara wanatoa visingizio mbalimbali ikiwemo mtandao kuwa chini, mashine kuharibika au kujizungusha hadi mnunuaji aondoke. Hili na lenyewe ni kosa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna baadhi ya wananchi, wakiwemo hata viongozi na watumishi wa umma na taasisi za Serikali kutokujali kudai risiti. Kitendo hiki kinaikosesha Serikali mapato. Kitendo hicho ni kujinyima maendeleo na kuwanufaisha wafanyabiashara wachache wasiotoa risiti na kuchukua fedha yako kwa niaba ya Serikali, huku wao wakiwa hawana wajibu wowote kwenu wa kutoa huduma au kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na wivu wa fedha tunayoitoa tunaponunua bidhaa ituletee maendeleo. Vitendo vya namna hiyo vya kuacha fedha ya Serikali ikakusanywa na anayeuza bidhaa, vinaongeza utofauti wa kipato kati ya

walionacho na wasionacho. Kwa hiyo, kila mmoja adai risiti, na anayeuza atoe risiti ili fedha ile itoe huduma ili tupunguze pengo la walionacho na wasionacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kumezuka dhana ya kuona kuwa kodi zinazotozwa na Serikali ni kubwa bila kujali majukumu makubwa ambayo nchi yetu inayo katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma za jamii. Hata kuna baadhi ya wanasiasa wanasema kodi hizi za Samia, kodi hizi za Mwigulu, kodi hizi za *TRA*.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kodi zote zinazokusanywa huwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali uliopo Benki Kuu ya Tanzania, na baadaye kupelekwa kwenye Wizara za Kisekta. Fedha hizo ndizo tunazoziona zinagharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo mijini na vijijini ikiwemo miradi ya umeme, maji, barabara, madaraja, vivuko, reli, usafiri wa anga, madarasa, zahanati, ununuzi na usambazaji wa dawa na malipo ya mishahara ya watumishi wa umma wakiwemo walimu na madaktari wanaotutibu. Kila mmoja wetu ajue kuwa kodi siyo jambo la Rais, wala siyo kodi za Rais. Kodi siyo jambo la Waziri wa Fedha, wala kodi siyo jambo la *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu, kodi ni jambo la nchi na kodi ndiyo maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani bajeti yetu tulikuwa tunajitegemea kwa asilimia 40 tu, fedha nyingine yote tulikuwa tunategemea mataifa ya nje. Sasa tumeshabadilisha, tuko zaidi ya asilimia 70. Tusirudi nyuma. Kujitegemea kuna heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania mwenye sifa ya kulipa kodi ana wajibu wa kulipa kodi stahiki, halali na kwa mujibu wa Sheria. Ni lazima tulipe kodi ili tuweze kuendelea. Ni lazima tutumie mashine za *EFD* bila udhuru na ni lazima kila anayeuza atoe risiti na anayenunua adai risiti. Mtu yeyote ambaye hataki kusumbuliwa kwenye masuala ya kodi ni vizuri akafata Sheria za kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa mamlaka ya mapato kuendelea kukusanya kodi kwa weledi, kwa kuzingatia katiba, Sheria na kanuni kama alivyoelekeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukusanya kodi kwa kutumia weledi na kwa kufata kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa mifumo ya kodi ya forodha pamoja na kodi za ndani kujenga mifumo inayosomana kikamilifu kwenye upande wa makusanyo na kwenye upande wa matumizi ili kuyapatia ufumbuzi wa kudumu malalamiko yanayojitokeza kwenye masuala, ya usimamizi wa kodi nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka nilisisitize; usimamizi na udhibiti wa fedha za umma; ambapo taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa bado kuna dosari katika matumizi ya fedha za umma hususan katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kudhibiti upotevu wa fedha za umma, hii imedhihirishwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ndio Mwenyekiti wa CCM wakati akipokea taarifa ya CAG ya kwanza tarehe 28 Mei, 2021 kwa kutoa maelekezo mahsusi kuongeza uwazi kutokuficha jambo lolote kwenye taarifa za ukaguzi alipokuwa akimwelekeza CAG.

Mheshimiwa Spika, nanukuu, "CAG naomba sana ulimi wako usiwe na utata, kama kuna shirika halifanyi vizuri tuambie hili halifanyi vizuri. Kama kuna bodi haisimamii vizuri tuambie bodi hii haisimamii vizuri. Kwa sababu tutakaposema mapungufu ndipo tutakapoweza kurekebisha na tutaweza kufanya vizuri zaidi. Tukinyamaziana kwa kutazamana sura hatutarekebisha na tutaumiza wananchi. Naomba sana ripoti yako iwe wazi zaidi, utakapo niletea ukaguzi wa mashirika naomba uwe wazi zaidi ili tujue tunachukua hatua gani". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linaloonesha nia ya dhati ya kusimamia fedha za umma kwa Serikali ya *CCM* ni pale Serikali ilipogundua mapungufu ya kwenye mfumo wa ukaguzi wa fedha na ununuzi. Niwakumbushe watanzania kwamba baada ya kuona hilo katika mwaka wa fedha 2022, Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliongeza fedha ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa ajili ya kuajiri watumishi zaidi ya 100 ili *CAG* aweze kufanya ukaguzi wa tathmini ya fedha *value for money* na ukaguzi wa wakati, *real time audit* kwenye miradi yote mikubwa na yenye matokeo makubwa na haya ndio matokeo mnayoona taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanayotokea kwenye taarifa ni jitihada za Mheshimiwa Rais za kudhibiti fedha za umma. Serikali inafanyia kazi hoja za ukaguzi za *CAG* na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale wote watakaobainika kuvunja taratibu katika matumizi ya fedha za umma bila kujali mkubwa wala mdogo kama alivyoelekeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi ndani kwa kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuwekeza kwenye mifumo ya TEHAMA na kuchukua hatua pale ambapo pana bainika. Hizi ni hatua za kulinda mali za umma na ni hatua za kukabiliana na watumishi wa umma wanao tumia vibaya fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nililotaka kulisisitiza ni masuala ya umasikini. Pamoja na utajiri tulionao na hatua kubwa ambayo nchi yetu imepiga, kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kitaifa kinapimwa kwa kuangalia wanakaya wanaoishi kwa kutumia chini ya shilingi 49,320 kwa mwezi kwa mtu mzima kwa ajili ya kupata mahitaji ya msingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kiwango cha umaskini uliokithiri unaopimwa kwa kuangalia wanakaya wanaoishi kwa kutumia chini ya shilingi 33,748 kwa mtu mzima, utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2017 ulionesha kuwa umasikini umepungua na kufika asilimia 26.4 kwa watanzania waliokuwa wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi, hali

hii imeonesha kuwa umaskini umepungua kutoka asimilia 28.2. pamoja na kuwa tumepiga hiyo hatua bado kasi hiyo hairidhishi, bado tunatakiwa tupige hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zimekuwa na mipango ya kuleta maendeleo ili kupunguza wimbi hilo la umaskini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili ni ajira kwa vijana ambapo pamoja na hatua kubwa zilizochukuliwa za kujenga uchumi kiwango cha ukosefu wa ajira bado ni kikubwa. Ukosefu wa ajira katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 au zaidi umepungua na kufikia asilimia 9.3 kutoka asilimia 10.5 lakini kiwango hicho bado kinatakiwa kipungue zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la ajira bado ni kubwa na hasa kwa vijana wa kike ambapo tuna vijana asilimia 16.7 ikiwa ni mara mbili kwa upande wa vijana wa kiume. Tatizo hili ni la kihistoria tangu uhuru wa nchi yetu ambapo wakati tunapata uhuru tulikuwa na madaktari 12, wahandisi 2, tulikuwa na chuo kikuu kimoja kilichokuwa na wanafunzi 14, shule za sekondari zilikuwa 41 na wanafunzi walikuwa 11,832, shule za msingi zilikuwa 3,270 na wanafunzi 486,470. Hii inamaanisha nini? Tulipokuwa tunapata uhuru kazi ya kwanza ilikuwa ni kujenga sekta ya utumishi wa umma ambapo viongozi wote wa Serikali na wananchi wote tulihimiza watoto waende shule ili wawe watumishi Serikalini. Kwa kipindi hicho, ilikuwa inawezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumeongeza vyuo kutoka chuo kimoja hadi 52 na wahitimu wameongezeka kutoka wale 14 hadi takribani 500,000 kutoka vyuo vya ufundi, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Shule za sekondari zimeongezeka kutoka 41 hadi 5,540 na wahitimu wameongezeka kutoka 11,000 hadi wahitimu zaidi ya 2,800,000. Aidha, shule za msingi zimeongezeka kutoka 3,000 hadi 19,000 na wanafunzi wameongezeka kutoka 480,000 hadi wanafunzi 11,420,000. Hali hii imebadili kabisa '*equation*' kutoka wahitimu kupokea barua zilizokuwa zinawaomba wachague kazi hadi kufikia kila kijiji kuwa na mhitimu ambaye hana ajira. Sasa sio ajabu kukuta familia moja yenye mzee mstaafu kuwa na

wategemezi ambao ni vijana wahitimu wanaoishi kwa kutegemea *pension* ya wastaafu kwa tatizo la ajira. *(Majira)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tulikuwa na aina ya uchumi ambao sekta ya umma ndio ilikuwa inafanya kila kitu. Hivyo, hata tulipo binafsisha mashirika ya umma na uchumi ukategemea zaidi sekta binafsi, wengi hatukuiamini na kuiheshimu sekta binafsi kama ilivyokuwa sekta ya umma pamoja na kuwa sekta binafsi ni mhimili wa uchumi. Waheshimiwa Wabunge, bado jamii yetu haiamini kuwa mtu anaweza kutajirika kupitia sekta binafsi na hata akitajirika inaaminika ni mwizi tu, hali inayoua uwekezaji wa ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa, mwekezaji wa ndani akijaribu kupiga hatua atapigwa vita na kukatishwa tamaa. Hata wamiliki wa ardhi hawapati fidia stahiki pale mwekezaji anapohitaji kumilikishwa ardhi hizo kana kwamba watanzania hawatakiwi kutajirika. Nitoe rai kwa watendaji wa Serikali, kutoa fursa kwa wamiliki wa ardhi kunufaika na maeneo wanayomiliki pale wanapihitaji kuyatoa maeneo hayo.

Mheshimiwa Rais Mama yetu amelirudia sana jambo hili kwamba tuwaache watanzania wapate hai yao pale wanapokuwa wanamiliki ardhi. Acheni watanzania walipwe pesa nyingi, acheni watanzania watajirike, acheni wapate faida na ardhi yao. Mheshimiwa Rais amewaona watanzania wanyonge wasipunjwe ardhi yao pale inapochukuliwa kwa matumizi mengine. Na hata fidia zinapotakiwa kulipwa zilipwe mapema. Nimeyasikia malalamiko ya Wabunge wengi lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaanza malipo ya fidia mmeona kule Songea Meona kule Liganga, mmeona pale Dodoma na hata yale ya Kitunguni ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Segerea amekuwa akililamikia timu ya wataalam itaenda kufanya tathmini na utekelezaji wake utafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wawekezaji wa nje, licha ya kwamba wawekezaji hao wanaleta mitaji, teknolojia, ajira, kuongeza mapato kwa Serikali na kukuza uchumi, uzoefu unaonesha kuwa, wawekezaji hao wanakumbana na vikwazo

vingi, uwezeshaji ndani ya Serikali na hata kwa wananchi. Kwa upande wa Serikali, kila ofisi anayoingia mwekezaji, wanatafuta kipengele kinachoweza kumkwamisha ili wazo lake likwame badala ya kutafuta namna nzuri ya kufanikisha uwekezaji ili tuweze kupata suluhisho la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wananchi, wanakutana na mtazamo hasi uraiani. Mwekezaji anapofika na mtaji wake anakutana na mawazo hasi. Kwa mfano mtu akitaka kuwekeza kwenye bandari ya uvuvi *deep sea fishing* mbali kabisa kule bandarini ambako hatuvui na pale ambapo tusipovua wale Samaki hawatusubiri wanaweza wakavuliwa nchi nyingine. Atakapo kuja akitaka kuwekeza anakutana na maswali haya la kwanza, utasikia ana fedha kweli, huyu sio tapeli kweli? La pili wakijiridhisha kwamba ana fedha, utasikia huyu hatatuibia kweli? Akitokea anayeshauri kwamba nadhani mwekezaji huyu ni muhimu kwa ajili ya nchi kwa ajili ya kutengeneza ajira, utasikia huyu anayesema huyu mwekezaji ni mzuri hajapewa fedha kweli? Atakuwa amelambishwa asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwekeze, ni lazima tuvutie uwekezaji, ni lazima tuvutie uwekezaji ili watoto wa kitanzania waweze kupata ajira, nani lazima watanzania na wenyewe wawekeze ili waweze kutajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jawabu la ukosefu wa ajira kwa vijana na kuondoa umaskini kwa watanzania ni kukuza uwekezaji, hususan katika sekta za uzalishaji na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Maono ya Mheshimiwa Rais wetu ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi ni maono sahihi kwa wakati sahihi. Hivyo, ni lazima watendaji wote Serikalini tuwe na nidhamu ya kuilea sekta binafsi na kuwezesha sekta binafsi kukua na kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, tunatumia nguvu kubwa sana kwenye kudhibiti kuliko tunayoitumia kwenye kuwezesha. Lazima tuheshimu sekta binafsi na kutambua mchango wake katika kutoa ajira na kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Nitoe rai tena kwa watanzania wenzangu tuwe na nidhamu katika kuiwezesha sekta binafsi na mtu yeyote anayejiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeamua kuchukua hatua mahsusi za muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Miongoni mwa hatua hizo ni kuweka mikakati wa kuongeza uzalishaji na mauzo ya bidhaa za nje ya nchi ili kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi. Katika kutekeleza haya, Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na wazalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda vinavyoongeza thamani na kuzalisha bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali kupitia Benki Kuu imehuisha Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje. Katika mwaka wa fedha huu katika kutekeleza azma hiyo Mheshimiwa Rais ameelekeza jambo hili liafnyike kwa haraka ambapo jumla ya shilingi bilioni 600 zinatarajiwa kutumika ambapo Benki Kuu ya Tanzania itatoa shilingi bilioni 280 na Benki ya Dunia itatoa mkopo wa masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 150. Hatua hii itawezesha uzalishaji na kuongeza mauzo ya bidhaa za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ndio Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, imeamua kuanza upya kuongeza mtaji kwenye benki zake yaani Benki ya Maendeleo ya Kilimo, *TAB, TADB* na Benki ya *TIB Development* na Benki ya *TCB*. Serikali inakamilisha taratibu ya kuzipatia mtaji Benki ya *TADB* na *TIB Development* ambapo jumla ya shilingi bilioni 235.9 baada ya kuzifanyia tathmini ya kina nakufahamu hali halisi ya benki hizo na kukamilisha tathmini hiyo zitapewa mtaji ili mtaji huo usiweze kupotea.

Mheshimiwa Spika, programu hiyo ya kuiwezesha mitaji benki ya *TADB* na *TIB Development* itaendelea kwa kipindi cha miaka mitano hadi kumi kwa kuzingatia mwenendo na uelekeo wa benki hizo ili hatimaye ziweze kuwa na mtaji usiopungua shilingi trilioni moja. Kwa upande *TCB* itapewa mtaji wa shilingi bilioni 30 ambayo tayari imeshapewa na kiasi kingine cha shilingi bilioni 101 kitatolewa. Lengo la hatua hizi ni kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya miradi ya kukuza sekta za uzalishaji na kuongeza wa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika katika kutekeleza azma ile ya kukuza sekta binafsi. Sote ni mashahidi wa jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anazozifanya katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara hapa nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya maboresho ya Sheria na sera mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo viwango vikubwa vya adhabu ambavyo hutumika kama vyanzo vya mapato; na uwepo wa kaguzi nyingi zisizokuwa na tija, hivyo kuongeza usumbufu katika kufanya biashara. Hali hii imesababisha Serikali kupokea malalamiko kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara kuhusu kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, uwekezaji na ufanyaji wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa: kaguzi nyingi zinafanyika kwa lengo la kutafuta makosa badala ya lengo la msingi la kuzuia kutokea kwa athari hasi. Kaguzi nyingi zinafanywa na taasisi mbalimbali na kila moja kwa wakati wake hivyo wafanyabiashara kutumia muda mwingi kupokea wageni badala ya kujihusisha na shughuli za uzalishaji na huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, adhabu kubwa zinasababisha biashara kufanyika kwa hasara; ukubwa wa adhabu unaotoa fursa ya majadiliano *(human interaction)* kati ya mwekezaji na wafanyabiashara na hivyo kuipotezea Serikali mapato na adhabu kutumika kama motisha na chanzo cha mapato ya taasisi za udhibiti; na utitiri wa tozo, ada na adhabu na kutokuwepo kwa mfumo jumuishi wa kuzilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutatua kero hizo, napendekeza kuanza matumizi ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti *(Single Window Payment System)* na taasisi za udhibiti kuweka utaratibu wa ukaguzi ambao hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo. Napendekeza hatua hizo zianze mara moja mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia ujenzi wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa

Njia ya Kielektroniki. Mfumo huo unatarajiwa kuunganisha pamoja taasisi zinazohusika na uwekezaji ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho kama ambavyo nimeziorodhesha taasisi zote ambazo tunazijua.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo huo, kutakuwa na manufaa ya kiuwekezaji ikiwemo: kuweza kusajili mradi popote ndani na nje ya nchi bila kuonana na watoa huduma wa taasisi husika; kupata kipaumbele cha kuhudumiwa kwa haraka katika taasisi zinazotoa huduma; kuweza kuingiza taarifa zake mara moja kwenye mfumo wa na kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku tatu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu unaochipukia kwa taasisi mbalimbali za Serikali na halmashauri kufunga biashara, ofisi na maeneo mengine ya uzalishaji baada ya kufanya ukaguzi na kuthibitisha ukiukwaji wa sheria kwa sababu zozote zile.

Mheshimiwa Spika, ufungaji wa biashara, kwa sababu zozote zile, una athari kubwa kwa ustawi wa uchumi wetu na una athiri ajira za wananchi, ustawi wa biashara, mapato ya kampuni na mapato ya Serikali. Aidha, utaratibu huu unakwenda kinyume na jitihada kubwa ambazo anazifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuboresha mazingira ya kufanya biashara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na athari hizo, napendekeza kuanzia tarehe 1 Julai, 2023, iwe ni marufuku kwa taasisi yoyote ya Serikali kufunga biashara, ofisi ama maeneo yoyote ya uzalishaji kwa kigezo cha kukiuka taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuboresha mazingira ya kufanya biashara hapa nchini. Ili kuondokana na matatizo yale ambayo nimeyataja napendekeza kuanzia tarehe 1 Julai, 2023 iwe ni marufuku kwa taasisi yoyote ya Serikali kufunga biashara, ofisi ama maeneo yoyote ya uzalishaji kwa kigezo cha kukiuka taratibu. Aidha, napendekeza sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zirekebishwe

ili kumchukulia hatua mwenye biashara kwa makosa ya biashara na siyo kuifunga biashara kwa makosa ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makosa ya biashara na siyo kuifunga biashara kwa makosa ya biashara. Kufunga biashara badala ya kumchukulia hatua mwenye biashara ni hatua za kikatili dhidi ya biashara, ni hatua za kikatili dhidi ya shughuli za uzalishaji. Hatua hii inalenga kulinda ajira za Watanzania, mapato ya biashara, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la ugomboaji na uondoshaji wa mizigo bandarini, upo utaratibu unaokataza mwagizaji kuondosha mizigo bandarini pale ambapo kodi inayokadiriwa inabishaniwa hadi pale kodi husika itakapolipwa. Utaratibu huu umeathiri kwa kiwango kikubwa uanzishwaji, ushamirishaji na ukuzaji wa biashara hapa nchini, umepunguza kasi ya matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kama lango la biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa sababu wakati mwingine bidhaa zile zikishikiliwa wakati wanapokubaliana bidhaa zinakuwa zimeoza. Ili kuondokana na athari hizo, napendekeza kuanzisha utaratibu utakaowezesha muagizaji wa mizigo yenye mapingamizi ya kodi aliyokuwa anakadiriwa kuweza kugomboa mizigo hiyo baada ya kulipa kodi isiyobishaniwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu maalum utawekwa chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki utakaolinda mapato ya Serikali na kuwezesha biashara kuendelea. Hata hivyo, mfanyabiashara atakayebainika kukiuka utaratibu huo atalazimika kulipa kodi iliyocheleweshwa, faini, kifungo jela au vyote kwa pamoja. Lakini mizigo ianze kutolewa kwa kulipa kodi ambayo haibishaniwi ili biashara iendelee kuliko kushikilia mizigo na biashara yote na kuua mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyinginezo za mapato. Kuanzia kipindi cha mwaka 2019/2020, Dunia imepita kwenye changamoto kubwa ya kiuchumi kufuatia kuenea kwa janga la UVIKO-19, vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vilizuka Februari 2022. Hii imeathiri si tu upatikanaji wa bidhaa muhimu katika soko la Tanzania, lakini pia imesababisha mfumuko wa bei katika nchi zote hapa duniani.

Dunia imeshuhudia hatua mpya ya mdororo wa uchumi, kupanda kwa mfumuko wa bei, na upungufu mkubwa wa bidhaa na dola za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan makaa ya mawe, jasi, chumvi, almasi, mawe ya chokaa, shaba, kuongezeka kwa shughuli za utalii kulitokana na Programu ya *Royal Tour*. Hatua ya Mapato kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 imezingatia masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho yanatarajiwa kwa mujibu wa maswali na kukidhi kiu ya shughuli mbalimbali zauzalishaji mali hapa ndani ya nchi tumeweka mkazo katika sekta za kimkakati kama vile kilimo, viwanda, ufugaji uvuvi, miundombinu ya umeme, uchukuzi na usafirishaji na sekta za kijamii kama vile elimu na afya. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

(ii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332.

(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.

(iv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438.

(v) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

(vi) Sheria ya Serikali za Mitaa na Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289, na sheria nyingine zote ambazo nimeziorodhesha katika ukurasa wa 91 na wa 92 katika hotuba hii ninayoisoma.

Mheshimiwa Spika, nikianza na kodi ya ongezeko la thamani sura namba 148 ya *VAT*. Napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo: -

(i) Kuongeza kima cha usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka

shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200. Serikali itaendelea kuongeza kima husika hadi kufikia shilingi milioni 500 ili kuepusha athari za kimapato zinazoweza kujitokeza. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Kodi ya Ongezeko la Thamani na kuchochea ulipaji kodi wa hiari. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 75,333 kwa kuwa walipakodi wenye mauzo ghafi kati ya milioni 100 hadi milioni 200 ni wengi na wamekuwa wakidai fidia *(refund)*.

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza viuatilifu vya mimea na vya mifugo zinazotambulika kwa *HS Code* 2916.32.00 na *HS Code* 2916.32.00. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa viuatilifu vya mimea na mifugo hapa nchini na kulinda viwanda vya ndani. Hatua hii inatarajia kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 6.8.

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma zinazotambulika kwa *HS Code* 9406.20.90 zitakazoagizwa na kutumiwa na wafugaji wa kuku. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa sekta ya mifugo, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Aidha, msamaha huu utatolewa baada ya mfugaji kusaini Mkataba wa Utekelezaji *(Performance Agreement)* mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 465.6.

(iv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake vinavyouzwa nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga na kuwawezesha kununua bidhaa husika hapa nchini au kuagiza kutoka nje ya nchi bila kulipa Kodi.

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini ya thamani, madini ya vito na madini mengine ya thamani yanayouzwa katika masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini vinavyoanzishwa na Tume ya Madini au vituo vya kusafishia dhahabu *(refineries)* vilivyopo hapa nchini. Lengo la hatua hii ni kuchochea uuzaji wa madini katika masoko na vituo ili

kuongeza mchango wa sekta ya madini katika ukuaji wa Pato la Taifa;

(vi) Kuruhusu ahirisho la kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Deferment)* kwa bidhaa za mtaji zinazozalishwa ndani ya nchi. Aidha, utaratibu wa ahirisho la ulipaji wa kodi husika kwa bidhaa za mtaji zinazotoka nje ya nchi utasitishwa baada ya miaka mitatu (3). Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji ndani ya nchi na kuongeza ajira, na kuhakikisha viwanda vinapata bidhaa za mtaji kwa bei nafuu;

(vii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza vifungashio vya dawa vinavyotambulika kwa *HS heading* 3902 na *heading* 3907. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio vya dawa hapa nchini na kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya kuwa shindani sokoni. Aidha, msamaha husika utatolewa baada ya mzalishaji kusaini Mkataba wa Utekelezaji *(Performance Agreement);*

(viii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye *molds* zinazotumika kutengeneza dawa za binadamu. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa dawa nchini na kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya kuwa shindani sokoni;

(ix) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa na kutumia pamba inayolimwa hapa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo hizi hasa katika kipindi cha mdororo wa uchumi;

(x) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa thamani ya kiwango cha asilimia sifuri kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima na watumiaji wa mbolea hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa kiuchumi;

(xi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyumba zinazouzwa na wajenzi wa nyumba za kibiashara zenye

gharama nafuu isiyozidi shilingi milioni 50. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wanunuaji wa nyumba hizo na kuboresha maisha ya Watanzania;

(xii) Kufanya marekebisho Kipengele cha 20 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuhusisha *gaming odds* na *gaming software* kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha;

(xiii) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Misamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 ili kuakisi mawanda ya bidhaa zinazosamehewa pamoja na kuoanisha na *H.S Codes* zilizomo kwenye kitabu cha Viwango vya Pamoja vya Ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki mambo haya yanapatikana katika Kiambatisho Namba 8;

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Kodi ya Mapato Sura namba 332. Napendekeza kusamehe Kodi ya Mapato kwenye mapato yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Mfuko wa Kitaifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* kwenye amana, hati fungani za muda mfupi, pamoja na gawio linalotokana na hisa. Lengo la hatua hii ni kufanikisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wanachama wastaafu na wenza wao ambao hawachangii kwenye mfuko baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, kwenye kifungu cha 56 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 ili miamala ya utoaji wa hisa mpya na uhamishaji wa miliki ya kampuni unaofanywa ndani ya nchi isitozwe Kodi ya Mapato. Lengo ni kuvutia uwekezaji nchini na kutoa ufafanuzi. Napendekeza kurekebisha sheria ya 82 ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kuondoa takwa la kutozwa Kodi ya zuio kwenye pango kwa wapangaji wa nyumba binafsi wasiofanya biashara. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea adha wapangaji binafsi kulipa kodi kwa niaba ya mwenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Mitaji kwenye ubadilishaji wa muundo wa ndani wa Kampuni unaofanywa kwa kuzingatia matakwa ya mikataba ya msingi iliyoainiwa baina ya Serikali na wawekezaji. Napendekeza kupunguza Kodi ya Ongezeko la thamani *(Capital Gain Tax)*

kutoka asilimia 10 kwenye faida hadi faida ya Kodi ya Mapato ya asilimia 3 ya thamani ya mauzo au thamani ya ardhi inayothaminishwa, bila kujali gharama zilizowekezwa katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha napendekeza kurekebisha Kifungu cha 65T cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kwa kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari. Nimeweka jedwali lile ambalo lina maeneo haya niliyokuwa nayataja.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini. Hatua hii inalenga kuwawekea utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wachimbaji hao na kutatua changamoto zilizokuwepo za ukusanyaji wa kodi katika sekta hiyo. Hatua hii inalenga kuongezea Serikali mapato kwa kiasi cha shilingi milioni 44.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kutoza kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo yatokanayo na uuzaji wa hewa ukaa *(verified emission reduction)*. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa wa ulipaji kodi na kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sheria ya ushuru wa bidhaa. Ushuru wa Bidhaa wa kifungu namba 124(2), marekebisho ya kiwango maalum ya ushuru wa bidhaa *(specific duty rates)* kwa bidhaa zote zisizo petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha viwango hivyo. Kwa muktadha huo, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru *(specific duty rates)* kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo petroli, na asilimia 20 kwenye bidhaa za bia na tumbaku. Lengo la hatua hii ni kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kwa kuwa utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa kutumia viwango maalum usiporekebishwa hupoteza thamani. Njia bora ya kutumika kuondoa mapungufu hayo ni kurekebisha viwango hivyo vya ushuru. Utaratibu huu hautajumuisha utozaji Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya mara ya mwisho yalifanyika mwaka 2016, bidhaa ambazo zinazozalishwa ndani na Sheria ya Fedha ya mwaka 2018. Kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi, viwanda, bidhaa za mvinyo, vinywaji vikali *(spirits)*, bidhaa za sukari zinazozalishwa nchini hazitafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kusamehe Ushuru wa Bidhaa unaotozwa kwa mujibu wa uwezo wa injini *(engine capacity)* kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme, napendekeza kusamehe ushuru wa bidhaa unaotozwa kwa mujibu wa uwezo wa injini kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme pekee inayotumika kwa *HS code* ambazo tumeziorodhesha kwenye jedwali, pamoja na magari yanayotumia Nishati Asilia *(CNG)* pekee. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya nishati ya umeme na gesi asilia nchini na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni inayotumika kuanglia nishati ya mafuta kutoka nje. Jambo hili linahusisha pia na vifaa kama ambavyo tutafafanua kwenye *Finance Bill.*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kupunguza ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 4,386 kwa lita hadi shilingi 2,466.45 kwa lita kwenye vinywaji vikali *(Ready to Drink)* vinavyozalishwa hapa nchini. Vinywaji hivyo vinatambulika kwa *Hs Code* 2208.60.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 20 kwa kila kilo moja ya Saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi. Uzalishaji wa saruji unatoa kiasi kikubwa cha hewa ya ukaa inayochafua na kuharibu mazingira. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kufidia athari hasi zinazotokana na hatua hiyo na lengo hili litaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni147,549.6.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye magari yenye uwezo wa injini wa kati ya 1000*cc* hadi 2000*cc* yaliyotokana na ukuaji wa teknolojia ili kuwianisha na magari mengine yenye ukubwa unaofanana na huo. Tumeziorodhesha *Hs Code* zinazoangukia katika eneo hilo. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye magari yenye uwezo wa injini zaidi ya 2000*cc* yanayotokana na

ukuaji wa teknolojia ili kuwianisha na magari hayo na mengine kama tulivyoainisha katika jedwali hilo *Hs Code* zake.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye magari ya abiria yanayoingizwa nchini yanayozidi umri wa miaka mitano (magari chakavu) yaliyotokana na ukuaji wa teknolojia kama tulivyoainisha katika *Hs Code* tulizoziweka katika jedwali. Kutoza ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye sigara na bidhaa za aina hiyo zinazotumika mbadala na tumbaku zinazotumika kwa *Hs code 2402.90.00;* tumbaku inayovutwa kwa kutumia bomba la maji inayotambulika kwa *Hs code 2403.11.00* na sigara za kielektroniki na bidhaa za aina hiyo zinazotambulika katika *Hs code* hizo tulizoziweka katika jedwali.

Mheshimiwa Spika, kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwenye mashine za Kamari zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa nchini. Mashine hizo zinatambulika kwa *Hs Code* kama tulizoziweka hapo, hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa zaidi ya milioni 1,365. Kuongeza ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 589.05 kwa lita hadi shilingi 600 kwa lita kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu *(Energy Drink)* zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Vinywaji hivyo vinatambulika kwa *Hs Code* ambazo tumezionesha hapo.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ili kuoanisha *Codes* zilizomo kwenye Kitabu cha Viwango vya Pamoja vya Ushuru. Hatua hizi za Ushuru wa Bidhaa kwa ujumla wake zitaongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 448,989.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura namba 438. Napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, napendekeleza kurekebisha kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili tafsiri ya neno *Primary Data Server* lijumuishe *server* halisi iliyopo nchini

Mheshimiwa Spika, napendekeleza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kushusha kiwango cha sasa cha adhabu inayotozwa kwa makosa ya kutotoa risiti au kutotumia mashine za kielektroniki, kinachoanzia *currency point* 300 (sawa na shilingi 4,500,000) hadi *currency point* 200 (sawa na shilingi 3,000,000) ili kuweka asilimia ya thamani ya kodi, ambayo ni asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi 30,000 kutegemea kiwango kilichotakiwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kushusha kiwango cha adhabu kinachotozwa kwa makosa ya kutokudai risiti au kutoa taarifa ya makosa ya kutokudai risiti kwa asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi elfu 30. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wale wenye mitaji midogo kuweza kustahimili kulipa bila kufunga biashara zao na lengo lingine ni kuwezesha kuondoa majadiliano ya faini hizo ambayo mengine yanavunja sheria.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Jedwali la viwango vya tozo chini ya Kanuni za Ada ya Mabango na Matangazo kama ambavyo tumeonyesha katika jedwali hilo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Kufanya maboresho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 290 ili jukumu la kukusanya ushuru wa mabango lihame kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura namba 290 kwa kuunganisha ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na Tozo ya Ardhi ili ziweze kulipwa kupitia namba ya malipo *(control number)* moja kwa moja. Mapato hayo yataingiizwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kubainisha kiasi cha fedha kinachokusanywa kutoka kwenye kila chanzo. Aidha, sheria ibainishe kuwa asilimia 20 ya mapato hayo yatarejeshwa Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI watasainiana Mkataba wa Makubaliano (*MoU*) wa usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi. Lengo la hatua hizi ni kuondoa kero kwa walipa kodi na kuongeza tija katika ukusanyaji wa kodi hizo. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza marekebisho ya kifungu cha 9A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura Namba 290 ili kuipa Ofisi ya Rais, TAMISEMI jukumu la kukusanya ushuru wa huduma (asilimia 0.3 ya mauzo ghafi) kwenye leseni za Huduma za Fedha Mtandaoni *(Electronic Money Issurance License)*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali za Mitaa, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura Namba 289 kama ifuatavyo: -

(a) Kurekebisha Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura Namba 289 kwa kuongeza maeneo yote ya Wilaya isipokuwa majengo yaliyosamehewa kupitia Kifungu cha 7 cha sheria hii. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika kulipa kodi; na

(b) Kuainisha zoezi la uthaminishaji wa majengo. kwenye hili kuainisha maana yake tunatoa taarifa kwamba zoezi la uthaminishaji wa majengo lianze kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kodi itozwe kwa kuzingatia thamani halisi ya jengo ifikapo mwaka 2026. Zoezi hili la majengo litasimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na ukusanyaji utafanyika kwa kwa namba ya malipo (*control number*).

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Namba 220 kwa kuongeza Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kiasi cha shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya *petrol* na *diesel*. Aidha, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 4A cha Sheria ya Ushuru wa Barabara Sura Namba, 220 kwa kuongeza kipengele ‘C’ kitakachoelekeza fedha zitakazokusanywa kutokana na ongezeko hili la ushuru wa barabara na mafuta la shilingi 100 kwa mafuta ya *petrol* na *diesel*

zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ili kupata vyanzo vya uhakika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hatua hii inatarajia kuiongezea Serikali fedha zaidi ya shilingi milioni 381,826.8.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, Sura Namba 437 na Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura Namba 306. Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza matumizi ya mifumo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Kufuta tozo kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji ili kuchochea matumizi ya kielektroniki katika miamala mbalimbali. Tunaiondoa *recharge*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Uhamiaji, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, Sura Namba 54 kwa kutoa hati ya ukaazi *(Residence Permit Class B*) kwa mwekezaji yeyote asiye mkaazi hapa nchini na atakayewekeza kununua nyumba kwa mtaji usiopungua Dola za Kimarekani 150,000. Aidha, Kibali cha Ukaazi kitatolewa baada ya mamlaka yenye dhamana ya uwekezaji kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya nyumba kujiridhisha na mtaji uliowekezwa. Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nyumba Nchini na kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Ardhi, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113, kwa kupunguza *(Premium)* ya tozo ya malipo ya kwanza kutoka asilimia 0.5 hadi asilimia 0.25. Napendekeza Kupunguza ada ya hati miliki kutoka shilingi 50,000 kwa hati hadi shilingi 25,000; Kupunguza ada ya usajili wa hati kutoka asilimia 20 hadi asilimia 10; Kupunguza ada ya maombi ya hati kutoka Sh.20,000 hadi shilingi 5,000; Kufuta ada ya mpango wa upimaji *(Deed Plan)* ambayo ilikua inatozwa shilingi 20,000; na Kurekebisha Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113 ili Mkurugenzi wa Halmashauri akasimiwe jukumu la ukusanyaji. Unaweza ukaona mama anavyojali Watanzania waweze kumiliki ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 90A(3) cha Sheria ya Madini, Sura Namba 123 ili kutoa msamaha kwa vituo vya kusafishia madini (*refineries*) wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia moja. Lengo la hatua hii ni kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya usafishaji madini nchini, kuvutia uwekezaji zaidi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napendekeza kupunguza kiwango cha tozo ya Ufundi Stadi kutoka asilimia 4.0 hadi asilimia 3.5. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia waajiri gharama za uendeshaji wa shughuli zao na kutimiza azma ya kupunguza tozo hizi hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza maboresho ya Sheria ya Kuendeleza Ujuzi ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya Fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Elimu kutoa hati ya msamaha wa tozo ya ufundi stadi baada ya kujiridhisha kuwa msamaha husika ni kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura Namba 82, ili mgao wa mapato yatokanayo na tozo ya Ufundi Stadi uwe kama ifuatavyo:-

(a) Theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa katika Wizara yenye dhamana ya Ajira;

(b) Theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na

(c) Theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa *VETA*.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa mipango ya mafunzo ya stadi za kazi yakiwemo mafunzo ya Uanagenzi na Tarakinishi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Magari ya Kigeni, napendekeza kuendelea na utaratibu wa kutoza magari ya kigeni yaliyosajiliwa nje ya Tanzania viwango sawa na vile

vinavyotozwa katika ukanda wa *EAC, SADC* na *COMESA*. Aidha, endapo itabainika kuwa kuna nchi inatoza viwango vya juu ikilinganishwa na vile vya ukanda wa *EAC, SADC* na *COMESA,* viwango hivyo vitatumika katika kutoza magari yaliyosajiliwa katika nchi husika. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa na kulinda maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kwa:-

(a) Kuanzisha michezo ya meza isiyozidi miwili katika maeneo yenye Mashine za Sloti Arobaini. Lengo la hatua hii ni kuongeza ukusanyaji;

(b) Kuongeza tozo ya michezo ya kubahatisha kutoka Sh.10,000 hadi shilingi 30,000 kwa kila mashine ya Sloti kwenye maeneo ya baa. Hatua hii inalenga kuongeza mapato ya Serikali;

(c) Kuongeza ada ya maombi ya shilingi 500,000 ya ada ya leseni Kuu ya dola za Kimarekani 10,000 kwa mwaka kwenye mashine za Sloti kwenye maduka; ada ya maombi ya shilingi 500,000 na ada ya leseni Kuu ya dola za Kimarekani 10,000 kwa mwaka kwenye mashine za Sloti katika maeneo ya baa; na

(d) Kupunguza kiwango cha kodi kutoka asilimia 25 hadi asilimia 18 kwenye mapato ghafi ya michezo ya kubahatisha kwenye maeneo ya uendeshaji wa Mashine 40 za Sloti. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika utozaji kodi katika michezo ya kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi kwa kusamehe tozo ya asilimia 80 kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa na wawekezaji waliopo kwenye Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (*EPZ)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kukufahamisha kwamba, kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichokaa kwenye *Pre-Budget Meeting,* kilichofanyika tarehe 12 Mei, 2023, Jijini Arusha, kilipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya

Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Viwango vyake vya forodha pamoja na Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mapendekezo hayo yanalenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi, kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha wa Afrika Mashariki ni kama ambavyo tumeonyesha kwenye *HS code* ambazo tumezibainisha kuanzia ukurasa wa 126 hadi ukurasa wa 135.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ushuru wa Forodha kwa viwango vya asilimia 25 badala asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba *(cotton lint)* zinazotambulika kwa *HS code* ambazo tumezibainisha katika jedwali linaloonekana katika ukurasa wa 157.

Mheshimiwa Spika, Maboresho ya ada na tozo mbalimbali za Taasisi pamoja na Taasisi za Serikali; napendekeza kufanya marekebisho ya kuanzisha kufuta na kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazisimamiwa na Wizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uwekezaji Viwanda na Biashara; kufuta adhabu ya asilimia 15 ya thamani ya bidhaa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania kwa bidhaa zinazoingia nchini bila ya kuwa na cheti cha uthibitisho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Uchukuzi; kufanya marekebisho kwenye tozo za uwekaji wa miundombinu kwenye hifadhi ya barabara (*right of way*) kwa kupunguza ada ya awali (*initial fee*) za usimikaji wa nyaya za mawasiliano kutoka dola za Kimarekani 1,000 kwa kilomita hadi dola za Kimarekani 200 kwa kilomita; na ada ya mwaka (*annual fee*) kwa kutoka dola za Kimarekani 1,000 kwa kilomita hadi dola za Kimarekani 100. Lengo la hatua hii ni kufanikisha malengo ya kusambaza miundombinu ya mawasiliano kutoka Mkoani kwenda Wilayani na kutoka Wilayani kwenda kwa wateja nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani; napendekeza kufanya maboresho ya ada na tozo mbalimbali ikiwemo:-

(a) Kuongeza tozo ya Hati ya Tabia Njema kwa Wageni kutoka dola za Kimarekani 25 hadi dola za kimarekani 50;

(b) Kuongeza tozo ya hati ya tabia njema kwa Wakazi kutoka shilingi 2,000 hadi shilingi10,000;

(c) Kuongeza tozo ya gharama ya uchunguzi wa hati zinazobishaniwa kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 75,000;

(d) Kuongeza tozo ya ada ya upotevu wa mali kutoka shilingi 500 hadi shilingi 1,000.

(e) Kutoza ada ya shilingi 10,000 za Kitanzania kwa ajili ya uchunguzi wa leseni;

(f) Kuongeza ada ya kibali cha kuhifadhi silaha katika maghala binafsi kutoka shilingi 1,000,000 hadi shilingi 1,500,000; na

(g) Kuongeza ada ya kuhuisha umiliki wa silaha za moto za kiraia kama ifuatavyo:-

(i) Bastola kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 100,000;

(ii) Shotgun kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000

(iii) Gobole kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000;

(iv) Bunduki *(Rifle)* kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, napata shida kutaja majina ya bunduki kwa sababu Watanzania hatujazoea mambo ya bunduki kwa ajili ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii; napendekeza Kufanya marekebisho ya ada na tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Utalii kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta ada ya kupanga na kurudia kupanga *(grading and regrading)* ya huduma za malazi zilizo nje na ndani ya maeneo ya hifadhi;

(b) Kupunguza viwango vya ada ya leseni za biashara ya utalii katika huduma za malazi zinazomilikiwa na Watanzania; na

(c) Kupunguza ada ya leseni ya utalii kwa huduma za malazi ambazo hazijakaguliwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii pamoja inalenga kupunguza gharama za uendeshaji na kuvutia uwekezaji zaidi katika Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Mifugo; napendekeza kufanya marekebisho mbalimbali kwenye Sekta ya Mifugo kama ilivyobainishwa katika kiambatanisho namba 10. Sekta ya Mifugo imepata nafuu nyingi kama ambavyo tumeendelea kutoa katika sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi; Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Uvuvi kama ambavyo tumeweka kwenye Jedwali Na. 2. Sekta ya Uvuvi kama ilivyo kwa Sekta ya Mifugo na yenyewe ni sekta ya uzalishaji ambazo tunaziangalia katika umakini wa kukuza sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, tunatarajia kufanya marekebisho ya ada kwa ya kufanya tafiti za kilimo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Sekta ya Kilimo na yenyewe ni sekta ya uzalishaji ni sekta ambazo tunazipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; napendekeza kufanya maboresho kwa kutoa tozo ya asilimia 1.5 kwenye *vinyl, Mini Disc, Compact Disc, DVD na SD Memory*. Hivi ni moja vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kudurufu na kutunza kazi za sanaa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wa Usajili na Udhamini (*RITA*); kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye

Sekta ya usajili, ufilisi na udhamini kama ambavyo tumeweka kwenye jedwali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wa Mbolea; kama tulivyoweka kwenye jedwali 12.

Kwa upande wa OSHA; kufuta ada ya ukaguzi ya shilingi 200,000 ya Ufungaji wa Gesi kwa kila kituo. Lengo la hatua hii ni kuchochea mazingira wezeshi ya biashara nchini hususan katika maeneo ya vituo vya gesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresho ya Sheria Mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi mbalimbali za udhibiti nchini na kufuta ama kupunguza ada na tozo kero, bado kumekuwa na changamoto za taasisi nyingi za udhibiti zinazosimamia sekta mbalimbali kuongeza kero za ufanyaji biashara. Serikali inakusudia kuanzisha mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti *(Single Window Payment System)* na kuweka utaratibu ambao utazifanya taasisi hizo kufanya kaguzi kwa namna ambayo haileti usumbufu kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na maeneo mengine. Maeneo hayo ni pamoja na hatua za kikodi ambazo zinapendekezwa katika jedwali ambalo tumelionesha.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Bajeti hii ya mwaka 2023/2024 inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 44.39 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 31.38, sawa na asilimia 70.7 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 26.73 na mapato ya Idara pamoja na Taasisi zingine yanatarajiwa kuwa trilioni 4.66.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, inatarajiwa kuwa

shilingi trilioni 5.47. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.44 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 3.54 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva na kiasi cha shilingi trilioni 1.90 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 2.10 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jedwali linaloonesha sura ya bajeti liko ukurasa wa 172 na ule wa 173. Kwa ukurasa wa 174 tumeelezea kwa kifupi baadhi ya vihatarishi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa CCM itaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 kama inavyosisitiza; itafanya mapinduzi ya uchumi kwa maendeleo ya watu; upatikanaji wa huduma bora za jamii kama ambavyo mmeona kwa sasa majengo ya madarasa na zahanati zilizoko vijijini zinapata majengo ambayo hawakuwahi kuyaona; Uwepo wa Utawala Bora, Utawala wa Sheria na Demokrasia; pamoja na kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, hususani katika Diplomasia ya Siasa pamoja na Diplomasia ya Kiuchumi, Mama yuko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Sisi sote ni mashahidi kuwa Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuwa chaguo namba moja kwa Watanzania hasa ikizingatiwa kuwa ndio chama pekee chenye nia ya dhati ya kuleta maendeleo hapa nchini. Waheshimiwa Wabunge, ukweli ni kuwa kila mtanzania anapozaliwa anakuwa mwana CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea kuwashukuru wale wote wa vyama vingine kwa kuwa na moyo wa upendo kwa kuendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020. CCM ni Baba na Mama wa demokrasia na itaendelea kuvipa fursa sawa vyama vingine na venyewe viweze kufanya siasa kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kulionesha hilo kwa vitendo, kila

mwenye chama chake amepewa fursa ya kufanya siasa bila upendeleo wala bila uoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu wakati wa hotuba yangu ya leo asubuhi, Serikali imeanza mchakato wa maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais ni muumini wa uongozi shirikishi, hivyo ameelekeza kuwa ni lazima Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ibebe maono ya wananchi wote bila ya kujali vyama vyao, bila kujali dini zao bila kujali makabila yao, bila kujali rangi zao. Kwa msingi huo, niendelee kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge kushiriki na kuwahamasisha wananchi katika Majimbo yetu kutoa ushirikiano kwa timu za wataalam zitakazokuwa zinazunguka kukusanya maoni ya kuandaa dira yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii tena kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kwa uongozi wake bora na thabiti wenye mafanikio makubwa, hususan katika kuleta mageuzi ya kiuchumi pamoja na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kikanda na Kimataifa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, hakika Mama apewe maua yake, ameelekeza kila sekta ikae na makundi ambayo wana masuala ambayo wana masuala ambayo yanahitaji Serikali ifanyie kazi yakiwepo masuala yanayohusu taasisi za kidini, masuala ya *charitable* yote yatafanyiwa kazi, masuala ya wafugaji, masuala ya wavuvi, masuuala ya kila sekta. Nitoe wito kwetu sote tuendelee kumpa ushirikiano ili aendelee kutuongoza vema na kutuheshimisha ndani na nje ya Bara la Afrika. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wao makini, weledi na jitihada zao za

kuhakikisha kuwa Watanzania wote na wanatanguliza mbele maslahi ya Taifa letu. Aidha, napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea na kuratibu shughuli za Serikali kwa umahiri mkubwa. Vilevile, kwa namna ya pekee, nimpongeze Komredi Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa utendaji wake uliotukuka katika kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kipekee kukupongeza wewe mwenyewe, Dkt. Tulia Ackson, kwa kuliongoza vyema kwa hekima na umahiri mkubwa, nimpongeze pia Mussa Azan Zungu, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa namna anavyoeendelea kukusaidia katika kushughulikia Bunge lako Tukufu. Kadhalika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuongoza Muhimili wa Mahakama. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa dhati ya moyo wangu kuwashukuru wakuu wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi. Naomba niwataje, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali John Mkunda; Inspekta Jenerali wa Polisi, Camilius Wambura; Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala; Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John William Masunga; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Said Hussein Masoro; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, *CP* Salum Hamduni na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas James Lyimo. Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wenyeviti, Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa

kuchaguliwa kusaidia katika kuliongoza Bunge hili. Nawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali na Binafsi kwa michango waliyotoa ili kukamilisha bajeti hii na kipekee nimpongeze *Chief Secretary* kwa mchango wake wa kuongoza timu ya wataalam. Kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru viongozi na waumini wa dini zote kwa kuendelea kuliombea Taifa letu. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwaomba viongozi na waumini wa dini zote kuendelea kumuombea Rais wetu pamoja na viongozi wote na Nchi yetu. Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema viongozi wetu na aendelee kuijalia amani Nchi yetu na dhamira njema ya Rais wetu iendelee kutamalaki. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Mbunge wa Jimbo la Kojani, kwa ushirikiano wake anaonipatia katika kutekelezaji majukumu hakika Mheshimiwa Chande ni Naibu Waziri wa viwango vya Wizara ya Fedha. Kipekee, nimpongeze na kumshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu, daktari mbobezi wa masuala ya uchumi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu na Makatibu Wakuu pamoja na timu yote ya wataalamu wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa ushirikiano wao mzuri wamekuwa chachu ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Washirika wote wa maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Washirika wa Maendeleo walioahidi kuchangia bajeti yetu ni pamoja na nchi wahisani; Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Mashirika ya Kimataifa yaliyoahidi kuchangia ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki za Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia

Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, Mfuko wa *OPEC* Maendeleo ya Kimataifa, Mfuko wa Mazingira Duniani, Mfuko wa *GRMF*, Umoja wa Mataifa, mashirika yote yaliyopo chini yake na Umoja wa Ulaya na Mashirikisha mengine mengi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuzipongeza timu zetu za Yanga na Simba kwa kuwakilisha vyema katika michuano ya Kimataifa, wamefanya kazi kubwa. Aidha, kwa namna ya pekee, niipongeze Timu ya Wananchi (Yanga) kwa kuweka historia ya kufika fainali za Kombe la Shirikisho Afrika. Ndugu zetu wa Simba walituwakilisha katika Mashindano ya Klabu Bingwa Afrika hadi kufika hatua ya robo fainali.

Mheshimiwa Spika, dalili ya mvua ni mawingu, Simba wamefika nusu fainali, wametolewa kwa mikwaju ya penati mara mbili hii inaonyesha siku si nyingi Kombe la Afrika litakuja Tanzania, kombe mojawapo litakuja Tanzania. Vilevile, naomba kutambua mchango na hamasa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutoa motisha kwa timu zetu za michezo pale zilipofanya vizuri Kimataifa, tunatoa rai na kwa timu zingine kama Azam, Singida, Namungo na zenyewe zifanye vizuri katika muda unaokuja. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, nitumie fursa hii ya kipekee kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuwasilisha hotuba hii. Mimi wazazi wangu hakuna hata mmoja anayejua kuandika jina langu wala jina lake, kupata fursa ya kuwasilisha Bajeti ya Nchi ni ushuhuda mbele za Mungu. Ninamshukuru sana Mungu kwa fursa hii na kwa kipekee kabisa napenda kuishukuru familia yangu, mke wangu kipenzi, Neema Mwigulu Nchemba na watoto wetu, kwa kuendelea kunitia moyo, najua yuko hapa juu, kuniombea wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza, Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kifungu cha 124(4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

2. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2023 ni sehemu ya bajeti hii.

3. **Mheshimiwa Spika**, makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo: Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 -

2025/26) ambao umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2022 - 2027; makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; na hotuba mbalimbali za Mheshimiwa Rais.

**4. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema pamoja na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi mapana ya Taifa na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani, umoja na mshikamano chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu**.

**5. Mheshimiwa Spika**, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii kubwa ya kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kuitumikia nafasi hii na kuchapa kazi kwa uadilifu, uaminifu na weledi mkubwa ili kutimiza malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

**6. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa dhati kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wake makini unaolenga mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amedhihirisha kuwa yeye** ni kiongozi makini, mwadilifu, msikivu, mchapakazi na aliye na maono thabiti ya kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo makubwa. **Ameendelea kutekeleza miradi ya zamani na miradi mipya, miradi mikubwa na miradi midogo, miradi ya kuchochea uchumi na miradi ya huduma za jamii, kusimamia deni la Serikali na kulipa madai yaliyopita kwa maslahi ya watumishi wa umma na wastaafu, kukuza demokrasia nchini na diplomasia ya uchumi.** *Hali hiyo inadhihirisha kuwa*

*hakuna kilichokwama bali vimeongezeka isivyoweza kusimuliwa kwa muda mfupi.*

**7. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Komredi Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, kwa namna anavyofuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. Ziara hizo zimekuwa na tija kubwa kwa kuchochea kasi ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo iliyokuwa imekwama. **Nawaelekeza watendaji wote wa Serikali kutekeleza maelekezo yanayotolewa wakati wa ziara hizo na muwapatie taarifa Waheshimiwa Wabunge**.

**8. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu inasonga mbele licha ya nchi zote duniani kupita kwenye misukosuko ya kiuchumi. Kwa mujibu wa jarida la uchumi la Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) la Aprili 2023, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kufikia dola za Marekani **bilioni 85.4** mwaka 2023 kutoka dola **bilioni 69.9** mwaka 2021. Tanzania imepanda hadi nafasi ya sita (6) ikilinganishwa na nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiongozwa na nchi za Kenya (dola bilioni 116.0), Ethiopia (dola bilioni 120.4), Angola (dola bilioni 121.4), Afrika Kusini (dola bilioni 405.7) na Nigeria (dola bilioni 477.4). Nchi nyingine zenye uchumi mkubwa chini ya Tanzania ni Ghana (dola bilioni 72.8), Cote d'Ivoire (dola bilioni 70.0), DRC (dola bilioni 62.8) na Uganda (dola bilioni 48.8). Hivyo, watanzania tunapotoa mifano ya wapi tunaelekea tuyajue mataifa yalioko mbele yetu. Na kwa programu hizi alizoanzisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM**, za kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji na kukuza uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi siku sio nyingi mataifa mengi tutayavuka.

**9. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ilianza mchakato wa kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni (*sovereign credit rating*) mwaka 2008 ambapo zoezi hilo halikukamilika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mdororo wa uchumi pamoja na kuyumba kwa soko la fedha duniani. Hata hivyo, **chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt.**

**Samia Suluhu Hassan, Serikali imefanikiwa kukamilisha zoezi hilo ambalo lilikuwa ni kikwazo katika utafutaji fedha na mitaji katika masoko ya kimataifa.**

**10. Mheshimiwa Spika**, mnamo Machi 2023, kampuni za *Fitch Ratings na Moody's Investors Service* zilianza zoezi la kuifanyia nchi tathmini ya kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa. Zoezi hilo lilikamilika ambapo kampuni ya Moody's Investors Service ilichapisha matokeo ya tathmini hiyo mwezi Mei 2023 na kampuni ya Fitch Ratings mwezi Juni 2023. Kwa mujibu wa matokeo hayo, **Kampuni ya Moody's Investors Service imeipa Tanzania daraja la B2 POSITIVE na Kampuni ya *Fitch Ratings* daraja la B POSITIVE, ambayo yanaashiria taswira chanya kwa nchi kimataifa.** Matokeo hayo ni bora kuliko nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi, usimamizi makini wa deni la Taifa, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa pamoja na kuleta maridhiano ya kisiasa ndani ya nchi. Kukamilika kwa zoezi hilo, kutaiwezesha nchi kutambulika katika masoko ya fedha ya kimataifa na hivyo, kuongeza sifa za kuvutia uwekezaji na kupanua wigo wa upatikanaji wa fedha kwa miradi ya Serikali na sekta binafsi.

**II. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

**11. Mheshimiwa Spika**, tunakumbuka kuwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** alishika madaraka ya kuongoza nchi katika kipindi ambacho dunia ilikuwa katika mtikisiko wa kiuchumi kutokana na janga la UVIKO-19 na baadae vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo inaendelea hadi sasa. Athari za majanga hayo zilionekana katika nyanja zote za kiuchumi na kijamii duniani ikiwemo kuongezeka kwa vifo, kuzorota kwa shughuli za uzalishaji na kuongezeka kwa gharama za utoaji huduma za jamii, hususan afya na elimu pamoja na kuongezeka kwa gharama za maisha. Kutokana na athari hizo, ukuaji wa uchumi nchini ulipungua kutoka asilimia 7.0 mwaka 2019 hadi asilimia 4.7 mwaka 2022.

**12. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kupokea kijiti cha uongozi katika kipindi cha majanga hayo, uongozi mahiri wa **Mheshimiwa**

**Dkt. Samia Suluhu Hassan** umetekeleza sera na mikakati mbalimbali iliyowezesha uchumi wa nchi yetu kuhimili majanga hayo ikiwemo utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Ni dhahiri kuwa, utekelezaji wa sera na mikakati hiyo umeleta mafanikio makubwa katika kipindi cha uongozi wa Awamu ya Sita. Mafanikio mengi yaliyopatikana katika kipindi cha Awamu ya Sita yamesemwa na Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha hotuba zao. Naomba nami nitambue baadhi ya mafanikio hayo kama ifuatavyo:

a) **Mapato**

**13**. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka na kufikia shilingi trilioni 24.40 mwaka 2021/22 ikilinganishwa na shilingi trilioni 20.59 mwaka 2020/21. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, ukusanyaji wa mapato ya ndani umefikia shilingi trilioni 21.67, ambapo mwezi Desemba 2022, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 2.63 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kukusanywa kwa mwezi tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo mwaka 1996. **Waheshimiwa Wabunge, mwenendo huu mzuri ni ishara kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ipo makini katika kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato kwa kuzingatia sheria, miongozo na taratibu pamoja na jitihada za kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.**

b) **Sekta ya Fedha**

**14.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini. Utekelezaji wa sera hizo umesababisha kushuka kwa viwango vya riba za mikopo ya benki ambapo katika kipindi cha mwaka kinachoishia Aprili 2023, viwango vya riba za mikopo vilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.91 kutoka wastani wa asilimia 16.58 Aprili 2021. Kupungua kwa viwango vya riba za mikopo kumechangia kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi ambapo mikopo hiyo imeongezeka kwa asilimia 22.5 Aprili 2023

ikilinganishwa na asilimia 4.8 Aprili 2021. Aidha, mikopo chechefu imeendelea kupungua hadi asilimia 5.5 Aprili 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.8 Aprili 2021. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ndogo ya benki ili kuongeza ufanisi katika eneo hilo.

**15.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inatambua umuhimu wa kuwezesha wananchi kiuchumi ikiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hivyo, Serikali inafanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika ugawaji na urejeshwaji wa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Utaratibu mpya wa utolewaji na urejeshaji wa mikopo hiyo utakapokamilika, Serikali itatoa taarifa kwa umma na kuendelea kutoa mikopo hiyo.

**16.** **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kuweka shilingi bilioni 1.0 kwenye mfuko wa watu wenye ulemavu kwa ajili ya kusaidia vifaa vinavyohitajika. Fedha hizo pia zitatumika kama mfuko wa wabunge wa kundi la watu wenye ulemavu na mchango kwa watoto wanaolelewa katika vituo maalumu. Nitoe rai kwa makampuni na watu binafsi kuchangia katika mfuko huo ili kuyasaidia haya makundi maalumu sambamba na programu inayotekelezwa chini ya TASAF.
**MAMA ameanzisha, sote tumuunge mkono**.

**17.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, inatarajia kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura 342. Marekebisho hayo yataiongezea Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board – DIB) majukumu ya kuweza kuongeza ukwasi kwa njia ya mkopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi. Marekebisho hayo pia yataipatia DIB nguvu na uhalali wa kisheria wa kushiriki kikamilifu, kwa kushirikiana na Benki Kuu, katika kutathmini na kuamua hatua muafaka ambayo inapaswa kuchukuliwa pindi benki au taasisi ya fedha inapokuwa katika hatari ya kufilisika. Utaratibu huu utasaidia kuokoa benki au taasisi za fedha kuingia kwenye mchakato wa ufilisi na hivyo kuepusha hasara na adha kubwa kwa wenye amana na wadai wengine.

**18. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kikosi Kazi cha Kifedha cha Kimataifa (Financial Action Task Force – FATF), ambapo ilifanikiwa yafuatayo: kufanya marekebisho ya sheria na kanuni kama sehemu ya kutekeleza viwango vya kiufundi vya FATF; kutengeneza Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi wa Mwaka 2022/23 hadi 2026/27; kufanya mapitio ya vihatarishi vya ufadhili wa ugaidi kwa Asasi za Kiraia; kufanya mafunzo na kampeni mbalimbali za kuongeza uelewa wa masuala ya utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kwa watoa taarifa na hasa taasisi teule zisizo za kifedha za biashara na taaluma; kuanzisha kituo maalumu cha kushughulikia kesi za utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; na kuandaa miongozo mbalimbali ya kusaidia taasisi zinazosimamia utekelezaji wa sheria katika kuchunguza na kuendesha mashitaka ya utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Lengo la hatua hizi ni ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa utakasishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

c) **Sekta za Uzalishaji**

**Kilimo**

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi vijijini ambapo kilimo ndiyo msingi wa ustawi wa maisha, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeendelea na dhamira yake ya kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294.0 mwaka wa fedha 2021/22 hadi shilingi bilioni 954.0 mwaka wa fedha 2022/23 na kufikia shilingi bilioni 970.8 mwaka wa fedha 2023/24.
Kuongezeka kwa bajeti ya kilimo kumewezesha: kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo; kuanzishwa kwa kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja (block farms); kuimarisha tafiti na huduma za ugani; kutolewa kwa ruzuku ya mbolea kwa wakulima; kuanza kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji na miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo; kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo; na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo.

**20. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa maghala 14 na vihenge 20 kwa ajili ya kuhifadhi nafaka. Hatua hizi zilichangia utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 114 mwaka 2022/23. **Serikali itaendelea kuiwezesha Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA) kununua mazao kutoka kwa wakulima. Katika mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya tani 400,000 zinatarajiwa kununuliwa na NFRA. Lengo la Serikali ni kuwa na akiba ya chakula inayokidhi mahitaji yasiyopungua miezi minne (4).**

**21. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea ili kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa gharama nafuu ambapo hadi Aprili 2023, shilingi bilioni 214.8 zimetolewa ikijumuisha fedha za ndani na nje. Kutolewa kwa ruzuku hiyo kuliwezesha wakulima kupata mbolea kwa bei ya kati ya shilingi 50,000 hadi 70,000 kwa mfuko wa kilo 50 badala ya bei ya soko ya wastani wa shilingi 140,000.

**22. Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya CCM chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, katika kuimarisha sekta ya kilimo, sote tumeshuhudia maendeleo mazuri ya utekelezaji wa miradi ya kilimo. Serikali itaendelea kuongeza fedha kwenye sekta hii kadri ufanisi utakavyoongezeka ikiwa ni motisha kwa utendaji mzuri. Hivyo, ninasisitiza sekta izingatie utaratibu wa *Performance for Results* (P4R). **Hatua hii inaweza kuongeza fedha zaidi za utekelezaji wa miradi ya kilimo hata kufikia shilingi trilioni 1.27. *Serikali ya Dkt. Samia iko kazini, tunataka kupiga vita umaskini kwa vitendo, tutaelewana tu!***

**Mifugo na Uvuvi**

**23. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha sekta ya mifugo, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya kuimarisha afya za mifugo, huduma za ugani, huduma za tafiti na mafunzo pamoja na masoko ya mazao ya mifugo. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii hadi Aprili 2023 ni

pamoja na: kukamilika kwa majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho 160 katika mikoa 25; kuanzisha vituo atamizi nane (8) ili kutoa ujuzi wa unenepeshaji wa mifugo kwa vijana na wanawake; na ununuzi wa pikipiki 1,200 na magari 13 kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za ugani.

**24. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha sekta ya uvuvi, Serikali imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya: ujenzi wa maabara katika Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania – TAFIRI (Dar es Salaam); kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa; kujenga na kukarabati miundombinu ya ukuzaji viumbe maji; kuendelea na ujenzi wa mialo ya Chifunfu (Sengerema) na Igabiro (Bukoba); na kukamilisha taratibu za ununuzi wa boti za uvuvi 118 ikiwa ni awamu ya kwanza ya ununuzi wa boti 160 kwa ajili ya kukopesha wavuvi. Aidha, Serikali imepunguza tozo za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi na kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha katika uagizaji wa pembejeo mbalimbali ambapo kampuni 15 za ukuzaji viumbe maji zimenufaika.

**25. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua changamoto wanazopitia wafugaji hapa nchini. Tatizo la malisho, maji, maeneo ya malisho kutumika kwa shughuli nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, tija ndogo ya shughuli za mazao ya mifugo na mengineyo. *Mifugo sio laana au umaskini katika nchi yetu, mifugo ni utajiri katika nchi yetu*. (Mimi nimesomeshwa kwa mifugo, bado nakumbuka hata rangi na majina ya ng'ombe waliouzwa). Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, itafanya tathmini ya kina kwa utaratibu ambao utakuwa shirikishi kwa kuwashirikisha wafugaji nchi nzima kupata namna bora ya kujenga na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya ufugaji na miundombinu ya mifugo sambamba na kutekeleza mapendekezo yaliyowasilishwa na wizara ya kisekta kuhusu kuboresha sekta ya mifugo. Kuna mabadiliko makubwa yanakuja kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi ili kuziwezesha sekta hizi ziweze kuchangia kwa kasi jitihada za kupunguza umaskini kwa watanzania na kukuza Pato la Taifa.

**Madini**

**26. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza thamani na kudhibiti utoroshaji wa rasilimali za madini, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya: kuanzisha vituo vya madini ambapo jumla ya vituo vipya 40 vimefunguliwa katika kipindi cha Awamu ya Sita na hivyo kufanya vituo vya madini kufikia 93; kukamilisha ujenzi wa vituo vya umahiri katika shughuli za madini vya Songea, Mpanda na Chunya; kununua madini ya Tanzanite yenye thamani ya shilingi bilioni 2.2; kununua mitambo midogo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini; na kununua mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa kwa kutumia makaa ya mawe.

**27. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha ujao, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya madini ili iweze kuchangia zaidi kwenye uchumi wa nchi yetu. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaongeza kasi ya kufanya tafiti za madini ya kimkakati na madini mengine. Aidha, Serikali itaanzisha minada ya madini nchini ili kuwezesha wachimbaji wa madini ya vito ikiwemo Tanzanite kuyafikia masoko ya kimataifa yenye bei halisi na kuvutia uongezaji thamani madini. Vilevile, hatua hiyo itasaidia kutangaza uwepo wa madini hayo hapa nchini na kuhamasisha uongezaji thamani madini katika mnyororo mzima wa uongezaji thamani.

**28. Mheshimiwa Spika**, kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vya kusafisha dhahabu nchini (refineries), Serikali inaendelea kuweka vivutio kwa viwanda hivyo ili viweze kupata malighafi za kutosha. Katika kutekeleza hilo, Serikali imepunguza mrabaha wa madini yanayouzwa kwenye *refineries* kutoka asilimia sita (6) hadi asilimia nne (4). Aidha, Serikali inaendelea kuchambua sera, sheria na taratibu za kiutawala na za kikodi ili kuwezesha dhahabu inayozalishwa kwenye migodi yetu isafishwe kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Kwa muktadha huo, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekamilisha taratibu za kununua dhahabu kupitia Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuanzisha **akiba ya dhahabu ya Taifa (Gold Reserve). Hatua hii itawapatia wachimbaji bei nzuri zaidi na kuimarisha sarafu yetu.**

**Hii ni baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia bajeti ya Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha na hotuba mbalimbali.

**29. Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kuukwamua Mradi wa Liganga na Mchuchuma, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwenye eneo la mradi ili taratibu za kuendeleza mradi huo **zianze bila kuwepo kwa mgogoro baina ya Serikali au mwekezaji na wananchi**.

**Maliasili na Utalii**

**30. Mheshimiwa Spika**, pamoja na sekta ya utalii kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na janga la UVIKO-19, hatua ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ilitangaza utalii kwa vitendo kupitia programu ya Tanzania – *the Royal Tour*, ambayo imekuwa na mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni ongezeko la idadi ya watalii wa nje kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asimilia 57.7. Aidha, watalii wa ndani waliotembelea maeneo mbalimbali ya vivutio vya utalii nchini walikuwa 2,363,260 ikilinganishwa na watalii wa ndani 788,933 waliotembelea vivutio vya utalii nchini mwaka 2021. Ongezeko hilo limeongeza mapato ya sekta ya utalii kutoka dola za Marekani milioni 1,310.0 mwaka 2021 hadi dola milioni 2,527.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 93.

**Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**31. Mheshimiwa Spika**, katika kujenga mazingira rafiki ya kuwezesha wananchi kulipa kodi, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, alitoa msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023. Msamaha huo ulilenga kuwapunguzia wananchi gharama na hivyo kuwezesha ulipaji wa deni la msingi. Katika kukabiliana na changamoto ya gharama za umilikishaji ardhi, Serikali inafanya mapitio ya tozo na

ada mbalimbali ili kutoa unafuu kwa wamiliki na pia kuongeza kasi ya umilikishaji. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi. Lengo la Mradi huo ni kuboresha milki za ardhi na utawala wa ardhi kwa kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ardhi ikiwemo kasi ndogo ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

d) **Miundombinu Wezeshi**

**Ujenzi**

**32. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya ujenzi, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ikiwemo barabara za kufungua fursa za kiuchumi na kuunganisha Tanzania na nchi jirani, madaraja na vivuko. Hadi Aprili 2023, jumla ya kilometa 1,151.37 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 1,483.74 zinaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami na kilometa 1,124.3 za barabara za mikoa zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Serikali imeendelea na upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7). Vilevile, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imetoa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa Barabara ya Kibaha – Morogoro (km 205.0) na **baadae Morogoro hadi Dodoma ili iweze kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma (km 112.3).**

**33. Mheshimiwa Spika**, kadhalika, Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 1.43 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami (km 798.1) na changarawe (km 23,251.9) pamoja na madaraja 177 na makalavati 1,002 kupitia TARURA. Hayo ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiongeza bajeti ya TARURA kwa zaidi ya mara nne. Barabara za vijijini ni maisha ya watanzania, ni uchumi wa watanzania na usalama wa watanzania. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara za vijijini, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya kujenga barabara za kudumu za mitaa na vijijini ili kuondokana na

barabara ambazo huaribika kipindi cha mvua. **Tumejifunza kutokana na utaratibu wa *Performance for Results* - P4R unaotumika na wafadhili kwenye utekelezaji wa miradi ya elimu na maji. Hivyo, ili kuboresha usimamizi wa rasilimali, eneo hili litapimwa kwa utendaji wake na kuongezewa fedha kadri ufanisi utakavyoongezeka. Hatua hii inaweza kuongeza fedha zaidi za utekelezaji wa miradi ya TARURA kwa kiasi cha shilingi bilioni 350. Ongezeko la fedha litalenga kujenga barabara ambazo ni kiungo muhimu cha kufungamanisha maeneo ya uzalishaji na masoko. MAMA yuko Kazini!**

**Uchukuzi**

**34. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza sekta ya uchukuzi, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo reli, bandari na viwanja vya ndege. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 98.14; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 93.83; na kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 31.07. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa kipande cha Makutupora - Tabora (km 371), Tabora - Isaka (km 163) na kipande cha Tabora – Kigoma (Km 506). **Mchakato wa ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa kipande cha Uvinza-MalagarasiMsongati na baadae kwenda Gitega hadi Uvira Kindu (DRC) unaendelea**.

**35. Mheshimiwa Spika**, Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kuendelea na ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa ya abiria na mizigo kwa ajili ya uendeshaji wa SGR. Serikali iko tayari kujenga reli ya kusini ya Mtwara – Mbambabay na Reli ya kaskazini (Tanga-Arusha-Mara) kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi (PPP). Katika kurahisisha shughuli za usafirishaji, Serikali imeendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya bandari zilizopo katika ukanda wa Bahari ya Hindi ikiwemo: Bandari ya Dar es Salaam awamu ya pili ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96; Bandari ya Tanga awamu ya pili (asilimia 99); na ujenzi wa Bandari Kavu - Ruvu (asilimia 90). Hatua za ujenzi wa bandari ya kisasa na yenye kina kirefu Bagamoyo zinaendelea.

**36. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu. Hadi Aprili 2023 hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa meli ya MV Mwanza *Hapa Kazi Tu* (Victoria) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83; ukarabati wa meli ya MV Umoja (Victoria) asilimia 83; na ukarabati wa meli ya MT Sangara (Tanganyika) asilimia 90.7. Aidha, Serikali inaendelea na ununuzi wa kandarasi kwa ajili ya ujenzi wa meli tatu (3) mpya za MV Liemba (Tanganyika), MT Nyangumi (Victoria) na MT Ukerewe (Victoria).

**37. Mheshimiwa Spika**, usafiri wa anga ni fursa kubwa kwa Taifa kiuchumi kwa kuwa unaunganisha nchi yetu na dunia kwa urahisi na haraka zaidi. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege nchini. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato umefikia asilimia 18, na Kiwanja cha Ndege cha Songwe asilimia 98. Aidha, Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Songea (asilimia 98), Iringa (asilimia 50) na Musoma (asilimia 47) na awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara umekamilika. Vilevile, katika kuimarisha usafiri wa anga, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza ndege nne (4) ikiwemo ndege moja (1) ya mizigo iliyowasili hivi karibuni na hivyo, kufanya Serikali kuwa na jumla ya ndege 13. Kadhalika, Serikali imefanya sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege tatu (3).

**Nishati**

**38. Mheshimiwa Spika**, mafanikio katika sekta ya nishati ni pamoja na kuendelea na ugharamiaji wa ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji wa nishati ya umeme kwa maji ikiwemo miradi ya Julius Nyerere (MW 2,115) ambao hadi Aprili 2023 umefikia asilimia 86.89 na Rusumo (MW 80) umefikia asilimia 99.0 pamoja na kukamilika kwa mradi wa uzalishaji wa nishati ya umeme kwa gesi wa Kinyerezi I *Extension* (MW 185). Aidha, Serikali inaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya usambazaji wa umeme kwa kuunganisha katika Gridi ya Taifa mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Buhigwe) pamoja na wilaya za Ngara na Biharamulo za mkoa wa Kagera. Vilevile, Serikali

inaendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme unaozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali nchini.

**39. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, inaendelea na usambazaji wa umeme vijijini ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2025, vijiji vyote viwe vimefikiwa. Katika kufikia azma hiyo, hadi Aprili 2023 kiasi cha shilingi bilioni 903.8 kimetolewa na zaidi ya asilimia 81 ya vijiji vimefikiwa na umeme. Katika mwaka wa fedha 2023/24, **Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme katika vijijini na baadhi ya ngazi za vitongoji. Hii ni ishara kwamba MAMA amedhamiria kufikisha umeme nchi nzima. MAMA yuko Kazini!**

**40. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa miradi hii ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kutaongeza uhakika wa upatikanaji wa umeme kwenye maeneo yote nchini ikiwemo maeneo ambayo hayakuwa yameunganishwa na Gridi ya Taifa kabla ya Serikali ya Awamu ya Sita kushika hatamu za uongozi. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo kutaiwezesha nchi yetu kuanza kuuza umeme nje ya nchi na kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni. Hii ni ishara tosha kuwa Serikali sikivu ya CCM ina dhamira ya dhati ya kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wake.

**Uchumi wa Kidijitali**

**41. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali itaendelea kusimamia mapinduzi ya kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndiyo yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika uchumi wa kidigitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na mwingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidijitali. Katika kufikia azma hii, Serikali itatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo: Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Project), na Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA.

e) **Huduma za jamii**

**42. Mheshimiwa Spika**, mambo mengi na makubwa yametekelezwa na **MAMA** yetu mpendwa ili kuhakikisha huduma za jamii zinaboreshwa na kuwezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kuwaletea maendeleo. Nikisema nitaje maeneo yote ambayo **MAMA** ameupiga mwingi, nadhani tutakesha hapa. Hivyo, naomba uniruhusu nigusie mafanikio machache, hususan katika elimu, afya na maji.

**Elimu**

**43. Mheshimiwa Spika**, programu ya Elimumsingi na Sekondari Bila Ada imeendelea kuboreshwa ambapo Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza jambo la kihistoria kwa kuwafutia ada wanafunzi wa kidato cha tano na sita na kuwafanya wanafunzi hao kusoma kwa utulivu. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia Programu hiyo ambapo hadi Aprili 2023 jumla ya shilingi bilioni 661.9 zimetolewa. Vilevile, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.41 kwa wanafunzi wa elimu ya juu na pia imeendelea na maboresho ya miundombinu ya vyuo ikijumuisha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi. **Napendekeza kuondoa ada kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na Serikali kujiunga na vyuo vya ufundi vya Dar es Salaam Institute of Technology – DIT, Mbeya University of Science and Technology – MUST na Arusha Technical College – ATC.** Hatua hii inalenga kuongeza idadi ya wataalamu wenye ujuzi na elimu inayohitajika katika zama hizi za mapinduzi ya nne ya viwanda (4th Industrial Revolution). **MAMA yuko Kazini!**

**44. Mheshimiwa Spika**, kufuatia mabadiliko ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, toleo la Mwaka 2023 na mabadiliko ya mitaala yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, ambapo Serikali inalenga kutoa elimu ya amali kwa ngazi zote kuanzia shule za awali, elimu ambayo itamuwezesha kijana wa kitanzania kujiajiri au kuajiriwa na hivyo, kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa.

Hivyo, **napendekeza kuanzisha programu ya mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa na Serikali kusoma kwenye vyuo vinavyotoa elimu katika fani za kipaumbele ambazo ni sayansi, afya, ufundi na ualimu. Hatua hii itaanza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo wa 2023/24. MAMA yuko Kazini!**

**45. Mheshimiwa Spika**, kwa upendo wa **MAMA** yetu hakuishia kwenye mikopo ya wanafunzi tu, pia aliamua kuongeza kiwango cha posho ya kujikimu maarufu kama ***Boom*** kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka shilingi 8,500 hadi shilingi 10,000 kwa siku. Mafanikio mengine ni pamoja na kujengwa kwa vyumba vipya 27,235 vya madarasa ya msingi na sekondari ikijumuisha madarasa 15,000 ya UVIKO-19. Aidha, madarasa hayo pia yanajumuisha madarasa 8,000 ya shule za sekondari yaliyojengwa kwa shilingi bilioni 160 iliyotolewa kupitia ***Pochi la MAMA*** ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wa kidato cha kwanza. Vilevile, Serikali imekamilisha: ukarabati wa shule kongwe 89; utoaji wa ajira kwa walimu 16,749 wa shule za msingi na sekondari; na ujenzi wa vyuo vya VETA ngazi za mikoa kwenye mikoa ya Rukwa, Njombe, Geita na Simiyu ambayo haikuwa na vyuo.

**Afya**

**46. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha sekta ya afya, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali tano (5) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu ambapo hadi Machi 2023 jumla ya shilingi bilioni 45.3 zilitolewa. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali imeendelea na ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri, ukarabati wa hospitali kongwe 19 na ukamilishaji wa zahanati 300 ambapo jumla ya shilingi bilioni 246.4 zimetolewa na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Aidha, Serikali imeendelea kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya ambapo jumla ya shilingi bilioni 544.2 zimetolewa zikijumuisha shilingi bilioni 487.5 zilizotolewa kupitia Bohari ya Dawa - MSD. **Ni nia ya Serikali ya Awamu ya Sita kuona kuwa huduma za afya zinazidi kuimarika, hivyo katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ikiwemo kuipatia mtaji MSD ili ifanye kazi kama bohari ya dawa**

**na sio kitengo cha ununuzi ya dawa serikalini. Kadhalika Serikali italipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuuwezesha kutoa huduma na mchango wake katika kuboresha huduma za afya hapa nchini**.

**47. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeendelea kuboresha miundombinu ya huduma za afya kupitia Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na UVIKO19 ambapo jumla ya shilingi bilioni 463 zimetolewa. Kiasi hicho cha fedha kilitumika katika ujenzi na ukarabati wa vyumba vya huduma za dharura - EMD (101), vyumba vya wagonjwa mahututi - ICU (70) na nyumba za watumishi (150). Aidha, kiasi hicho pia kiliwezesha ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ikiwemo mashine 169 za digitali za *X – Rays*, *CT - Scan* (30), *MRI* (4) *Echocardiograph* (7), magari ya kawaida na ya kubebea wagonjwa (ambulance) 663 kwenye kila Halmashauri na maboresho ya miundombinu mbalimbali. Vilevile, uwekezaji huo umebadili kabisa taswira ya afya kwenye teknolojia na miundombinu ambapo rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi zimepungua kwa asilimia 97.

**48. Mheshimiwa Spika**, kwa mara ya kwanza Tanzania tumeweza kumtibu mtoto mwenye ugonjwa wa seli mundu (sickle cell) na kupona kabisa. Mtoto huyo aliletwa hapa bungeni na Waheshimiwa Wabunge mlimuona. Tiba ya seli mundu ilikuwa haipatikani nchini na hivyo kulazimu kutibiwa nje ya nchi kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 250 kwa mtu mmoja. Katika kuhakikisha huduma hiyo inanufaisha watoto wengi zaidi, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ametoa shilingi bilioni tano (5) kwa ajili ya matibabu hayo. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na: kutoa uvimbe chini ya sakafu ya ubongo bila kupasua kichwa ambapo matibabu hayo nje ya nchi yalikuwa yakigharimu shilingi milioni 80 kwa mtu mmoja; na kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha mionzi tiba ambayo imeifanya Tanzania kuwa nchi ya 5 Afrika kuwa na kiwanda hicho na kuokoa zaidi ya bilioni 11 zilizokuwa zinaenda nje kununua mionzi hiyo.

**49.** **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla jitihada za Mheshimiwa Rais katika kuboresha huduma za afya kumewezesha kuokoa kiasi kikubwa cha fedha zetu za kigeni zilizokuwa zinatumika kwa matibabu nje ya nchi. Jitihada hizo siyo tu zimesaidia Tanzania bali zimevuka mipaka ya nchi kwani majirani zetu tuliokuwa tunapanga nao foleni nje kutafuta tiba leo kimbilio lao ni Tanzania.

**Maji**

**50.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza dhana ya kumtua mama ndoo kichwani, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeendelea kuongeza bajeti ya sekta ya maji ambapo kwa mwaka 2022/23, ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 709.4. Fedha hizo zimefanikisha kukamilika kwa miradi 80 ya usambazaji maji mijini na miradi 1,373 vijijini. Miradi hiyo inajumuisha miradi 218 kupitia fedha za Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kiuchumi na Kijamii zitokanazo na UVIKO–19. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji maji vijijini na kufikia asilimia 77.0 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 70.1 mwaka 2020. Vilevile, upatikanaji wa huduma za maji mijini ulifikia asilimia 88.0 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 84.0 mwaka 2020.

**51.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imesambaza seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika mikoa 25 na seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa katika kila kanda. **Nitoe rai kwa Halmashauri, Miji na Majiji kuchimba visima vingi kwa kadri iwezekanavyo kwa kutumia mapato ya ndani.** ***Mmepewa mitambo ya mabilioni ya kuchimba visima na mabwawa kila mkoa hivyo, itakuwa ni uzembe na ubinafsi kukosa shilingi milioni 15 za kuchimba kisima. Anachokusudia MAMA sio tu kumtua mwanamke ndoo kichwani bali kuiondoa kabisa ndoo, mtu achote maji hapohapo anapoishi kwa sufuria ya kupikia.***

f) **Sekta Nyingine**

**Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

**52. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini imeendelea na jitihada za kupunguza umaskini nchini ambapo hadi Machi 2023 jumla ya kaya 1,371,916 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika Kipindi cha Pili cha Mpango kutoka maeneo yote ya utekelezaji 186 kwa Tanzania Bara, Pemba na Unguja kwa Zanzibar ambapo jumla ya shilingi bilioni 218 zilitumika. Aidha, miongoni mwa ubunifu uliofanywa katika utekelezaji wa Mpango huo ni kutoa msaada kwa watu wenye ulemavu ambapo kaya yenye mtu mwenye ulemavu hupokea nyongeza ya shilingi 5,000 kwa mwezi. Hadi Mei 2023, takribani kaya 110,000 zenye wanakaya wenye ulemavu zimenufaika na mpango huo.

**Maslahi ya Watumishi na Wastaafu**

**53. Mheshimiwa Spika**, tangu kuingia kwake madarakani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia na jitihada kubwa katika kuboresha Utumishi wa Umma nchini kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Kutokana na jitihada hizo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

(i) Kupandisha madaraja watumishi 135,170 wenye sifa stahiki ambapo hadi Aprili 2023, jumla ya shilingi bilioni 177.9 zimetumika;

(ii) Kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, ambapo kima cha chini cha mishahara kiliongezeka kutoka shilingi 300,000 hadi shilingi 370,000;

(iii) Kulipa madeni ya malimbikizo ya mishahara kwa Watumishi wa Umma 94,290 yenye thamani ya shilingi bilioni 165.9 hadi Aprili 2023;

(iv) Kupunguza kodi ya mapato ya ajira (PAYE) kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8;

(v) Kuondoa tozo ya limbikizo la Mkopo wa Elimu ya Juu, ambapo takribani kiasi cha shilingi trilioni 1.1 kilisamehewa; na

(vi) Kulipa madeni ya watumishi (yasiyo ya kimshahara) shilingi bilioni 42.7 hadi Aprili 2023.

**54. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa makato ya watumishi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, mwaka 2021/22 Serikali ilianza kutekeleza maamuzi yake ya kukata makato yote ya kisheria kwenye chanzo kimoja ambacho ni Wizara ya Fedha na Mipango na kuwasilisha moja kwa moja kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Utaratibu huu umewezesha kuondoa tatizo la malimbikizo ya michango ya watumishi kwenda kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Nawaelekeza Maafisa Masuuli kuhakiki na kulipa malimbikizo ya michango ambayo haikuwasilishwa kwenye mifuko hiyo ili kuondoa usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu.

**Sensa ya Watu na Makazi**

**55. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa Serikali iliendesha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti 2022 na matokeo ya awali yalizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Oktoba, 2022. Matokeo ya sensa yalionesha kuwa Tanzania ina jumla ya watu takribani milioni 61.7, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka. Takwimu za sensa hiyo ni muhimu kwa ajili ya mipango jumuishi na maendeleo endelevu ya nchi na yataongeza ufanisi katika kugawa rasilimali zilizopo kuendana na uwiano wa idadi ya watu katika ngazi zote za utawala. Aidha, matokeo yatatumika na Serikali na wadau wengine katika maandalizi, ufuatiliaji na tathmini ya mipango mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

**Diplomasia ya Uchumi**

**56. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha uhusiano na

ushirikiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Kuimarika kwa ushirikiano huo ni matokeo ya jitihada za Mheshimiwa Rais za kuifungua nchi kiuchumi kwa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika kutekeleza diplomasia ya uchumi.

**57. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uhusiano na kuchochea uchumi na biashara kwa nchi za Afrika, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuratibu majadiliano yanayohusu utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA). Kupitia utekelezaji wa mkataba huo, Tanzania itaweza kushiriki kwa ufanisi katika biashara kwenye soko huru la ukanda wa Afrika na kujenga uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa kupitia sera bora za kukuza teknolojia, ubunifu na ushindani.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kufungua uchumi kupitia ushirikiano na mataifa mengine duniani, Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuimarisha uhusiano kati ya Taifa letu na washirika wetu wa maendeleo ambao umetujengea heshima na kuaminika kimataifa. Sisi sote ni mashahidi kuwa, katika kipindi cha miaka miwili ya **MAMA**, Serikali ilipokea misaada na mikopo nafuu yenye thamani ya shilingi trilioni 8.54 ikiwemo mkopo usiokuwa na riba wa kiasi cha shilingi trilioni 1.29 uliotolewa na IMF kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 na matokeo yake tumeyaona katika majimbo yetu. **Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matunda ya kuboresha ushirikiano!** Aidha, Mheshimiwa Rais ameendelea kusimamia utekelezaji madhubuti wa programu ya Extended Credit Facility (ECF) inayosimamiwa na Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF na Programu ya Development Policy Operation (DPO) inayoratibiwa na Benki ya Dunia katika mkakati wa kufufua, kuchochea na kuimarisha uchumi. Napenda kuwahakikishia kuwa fedha hizo zimewekezwa katika shughuli mbalimbali za kuchachua uchumi ikiwemo sekta za uzalishaji, miundombinu na huduma za jamii. Niwaombe wote tumuunge mkono **MAMA** yetu katika kufanikisha maono mazuri aliyonayo kwa Taifa letu.

**Masuala ya Muungano**

**59. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ni Tunu ya Taifa letu na ndio utambulisho wetu duniani, hivyo ni jukumu letu sote kuulinda, kuudumisha na kuuenzi. Katika kuendelea kudumisha Muungano, Serikali imekuwa ikifanya vikao mbalimbali kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa hoja za Muungano. Katika mwaka 2022/23, Serikali ilijadili hoja nane (8) za Muungano ambapo hoja nne (4) zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni: malalamiko ya wafanyabiashara wa zanzibar kutozwa kodi mara mbili; kodi ya mapato (Pay As You Earn - PAYE) na kodi ya zuio (Withholding Tax); mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III); na ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO).

**60. Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa wakati ili kuulinda na kuudumisha Muungano wetu adhimu.

**Utawala Bora, Ulinzi na Usalama**

**61. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ikijumuisha ujenzi wa ofisi jumuishi na ujenzi wa jengo la makao makuu ya mahakama Jijini Dodoma. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa ofisi za uhamiaji katika mkoa wa Geita na kuendelea na ujenzi katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Dodoma. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki kwa kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi na kuongeza idadi ya majaji, mahakimu na mawakili.

**62. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuiimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili ziende sambamba na mwendo wa Mahakama. Serikali itaendelea kuviimarisha vyombo vya Ulinzi na Usalama ili viweze

kufanya kazi vizuri ya kuimarisha ulinzi na usalama kama alivyoweka Amri Jeshi Mkuu ambaye pia ni **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuwa ulinzi na usalama ni kipaumbele cha juu kinachowezesha vipaumbele vingine kutekelezwa.

**63. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, inapeleka fedha nyingi Wizarani, Mikoani na Wilayani kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi yetu. Natoa rai kwa mawaziri wenzangu na watendaji wote wa Serikali kufuatilia matumizi ya fedha hizi na kuchukua hatua stahiki pale fedha zinapotumika vibaya pasipo kusubiri mbio za mwenge, ziara za viongozi wa kitaifa au taarifa ya CAG. **Kwa mujibu wa muundo wa utawala katika nchi yetu, kila ngazi ina uongozi kamili wa Serikali, *tunao wa kupanga, tunao wa kufanya malipo, tunao wa kukagua, tunao wa kutathmini, tunao wa kuchunguza, tunao wa kukamata, tunao wa kupeleleza, tunayo magereza ya kuwaweka wahalifu na tunao wa kuhukumu*.** Kwa nini tunasubiri mbio za mwenge, ziara za viongozi wa kitaifa au taarifa ya CAG na kila siku tunaishi huko inakotekelezwa miradi. **Viongozi wa Serikali tusijidogoshe, tumepewa mamlaka.**

**Uwekezaji, Viwanda na Biashara**

**64. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeendelea na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara ili kuongeza ushindani wa Tanzania katika soko la kimataifa kwa: kutunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania Namba 10 ya Mwaka 2022; kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Sura 415 kwa lengo la kuondoa mwingiliano wa majukumu ya taasisi za udhibiti na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi; na kuunganisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji **Mahali Pamoja na mifumo ya taasisi za NIDA, TRA, BRELA, TIC, Idara ya Kazi, Idara ya Uhamiaji na Idara ya Ardhi**.

**65. Mheshimiwa Spika**, hatua hizo za Serikali zimeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo: kupunguza wastani wa siku za kupata vibali katika mamlaka za udhibiti kutoka siku 14 hadi siku tatu (3);

kurekebishwa kwa ada na tozo 39; kutoa huduma za uwekezaji katika kituo cha Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (OSC); na kuongeza ushindani na ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali ikiwemo biashara ya uondoshaji na ugomboaji wa shehena za bidhaa mbalimbali zinazosafirishwa kwa njia ya maji.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuondoa vikwazo vya kibiashara, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kampuni, Sura 212 kwa kuongeza kifungu cha 452A ili kumpatia mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Biashara kwa kushauriana na Waziri wa Fedha, kutoa msamaha wa ulipaji wa ada ya kuwasilisha nyaraka nje ya muda (late filing fee).

**67. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa sheria hii, kumekuwepo na changamoto ya kukosekana kwa utaratibu wa kutoa msamaha huo, hivyo, Serikali imefanya uchambuzi na kutoa mapendekezo ya namna ya kutekeleza msamaha tajwa. Kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Waziri mwenye dhamana ya Biashara baada ya kujiridhisha atatoa Notisi kupitia Gazeti la Serikali kufuta sehemu ya ada ya adhabu kwa kutumia asilimia katika ada ya ucheleweshwaji kwa kuzingatia vigezo vitakavyoainishwa kwenye Notisi hiyo. **Notisi hiyo pia itaainisha kampuni zitakazohuisha taarifa zake kwenye mfumo ndani ya kipindi cha miezi 12 ambapo zitasamehewa asilimia 50 ya ada ya kuwasilisha nyaraka nje ya muda. Marekebisho hayo yatazihusu kampuni ambazo zilisajiliwa kabla ya mfumo wa *Online Registration System* – ORS kuanza kutumika (kabla ya mwaka 2017).**

**68. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali imekamilisha mapitio ya Sheria ya PPP, Sura 103 na kuwasilisha muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ambayo yamepitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 13 Juni 2023. Kuridhiwa kwa marekebisho hayo kutawezesha kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa utaratibu wa PPP. Rai yangu kwa Mawaziri wenzangu na watendaji wa Serikali kutumia fursa hiyo kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo. Utaratibu huo unatumika na mataifa mengi duniani ikiwa ni njia mbadala ya

kugharamia miradi iliyopaswa kutekelezwa na Serikali na kuchochea maendeleo.

## III. TATHMINI YA CHANGAMOTO ZA UCHUMI WA DUNIA

### UVIKO-19 na Vita kati ya Urusi na Ukraine

**69. Mheshimiwa Spika**, uchumi wa dunia umekumbwa na athari kubwa zinazotokana na majanga ya UVIKO-19 na vita kati ya Urusi na Ukraine. Changamoto hizo zimesababisha kuvurugika kwa mfumo wa uzalishaji, mnyororo wa usambazaji na uhitaji wa huduma na bidhaa. Mathalan, athari za UVIKO-19 zilisababisha ukuaji hasi wa uchumi wa dunia wa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 2.9 mwaka 2019. Aidha, ukuaji wa uchumi wa dunia uliimarika hadi asilimia 6.3 mwaka 2021 na kushuka hadi asilimia 3.4 mwaka 2022, hali iliyochangiwa na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine. **Athari nyingine ni kuongezeka kwa mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2019 hadi asilimia 8.7 mwaka 2022, kulikochangiwa na kupanda kwa bei za bidhaa za petroli na chakula. Kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii duniani, changamoto hizo zimekuwa na athari katika uchumi wa mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania.**

**70. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na athari za UVIKO-19 nchini, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na UVIKO-19. Utekelezaji wa Mpango huo umesaidia: kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama; kusogeza huduma za afya karibu na wananchi; kuongeza miundombinu ya elimu ili kupunguza msongamano wa wanafunzi; kuboresha miundombinu na huduma za utalii; na kuwezesha kaya maskini 51,290 zilizoathiriwa na UVIKO-19 kwa kuzipatia fedha taslimu ili kumudu mahitaji yao ya msingi. Aidha, Mpango huo umewezesha uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogo ikiwemo wamachinga.

**71. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) Kutoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 479.4 katika mafuta ya petroli na dizeli ili kupunguza makali ya bei na kuleta nafuu kwa walaji; Hatua hii imesaidia kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa pamoja na usafirishaji wa bidhaa na abiria;

(ii) Kutoa unafuu wa kodi kwenye mafuta ya kula na mbolea ili kuongeza uzalishaji, kupunguza bei na kuzalisha ajira;

(iii) Kuimarisha miundombinu wezeshi na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi; na

(iv) Kuongeza bajeti kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na utalii ili kuongeza ajira, kuchochea uzalishaji na kuongeza mauzo nje ya nchi.

**72. Mheshimiwa Spika**, pamoja na athari zitokanazo na UVIKO–19, fursa mbalimbali zimejitokeza ikiwemo: kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya ndani wa vifaa vya kujikinga na UVIKO - 19 ikiwemo barakoa, vipukusa na dawa ambapo hapo awali vilikuwa vikiagizwa kutoka nje; kuongezeka kwa ajira, hususan katika sekta ya afya; na kuongezeka kwa ubunifu na utafiti wa dawa asili. Kwa upande wa sekta ya habari na mawasiliano, fursa zilizotokana na UVIKO-19 ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya habari katika kutoa habari na kufanya biashara mtandao kupitia *mobile applications*. Aidha, Serikali imeweza kupunguza gharama za vikao kazi na mikutano kwa kutumia njia ya mtandao (virtual meetings) ili kuwezesha majadiliano pasipo kuhitaji mikusanyiko.

**73. Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto za vita kati ya Urusi na Ukraine, Serikali inalenga kutumia fursa ambazo hazijatumika kikamilifu ili kuongeza uzalishaji wa ndani na kupunguza utegemezi. Fursa hizo ni pamoja na uwepo wa: gesi asilia nchini itakayoweza kupunguza utegemezi wa mafuta yanayoagizwa kutoka nje; eneo kubwa la bandari ambalo linafaa kujenga hifadhi ya mafuta ya kimkakati (strategic oil reserve); maeneo yanayoweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa ngano, alizeti na chikichi nchini; uwepo wa maeneo yanayoweza

kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji; na malighafi za kuzalisha mbolea nchini.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kutumia fursa hizo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo: ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam; kuanza kwa taratibu za ujenzi wa *petroleum hubs* katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Tanga; kuendelea kuimarisha miundombinu ya utafiti na kufanya tafiti zitakazozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo cha mazao ya ngano, alizeti na chikichi; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji wa viwanda nchini, hususan viwanda vya mbolea.

**Upatikanaji wa Dola ya Marekani**

**75. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania zilikumbwa na upungufu wa ukwasi wa dola ya Marekani. Changamoto hii ilisababishwa na mambo manne makubwa. **Mosi**, vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambavyo vilisababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma duniani, hivyo kuongeza mahitaji ya dola ya Marekani, ambayo ndiyo sarafu kuu katika biashara ya kimataifa. **Pili**, sera ya fedha ya Marekani, ambayo ilijielekeza kwenye kupandisha riba, hali iliyosababisha wawekezaji wengi kuelekeza mitaji yao Marekani na kusababisha upungufu wa dola kwenye nchi nyingine. **Tatu**, kufunguka kwa shughuli za kiuchumi baada ya athari za UVIKO-19, jambo lililoongeza mahitaji ya dola za Marekani ikilinganishwa na kiasi kilichopo kwenye masoko ya fedha. Sababu ya mwisho ni mabadiliko ya tabianchi, yaliyopunguza uzalishaji hasa kwa nchi zinazoendelea na kuongeza mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kutumia dola ya Marekani.

**76. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa tunakabiliana na changamoto hii, Serikali imeamua kuchukua hatua mahususi za muda mfupi, wa kati na mrefu. Miongoni mwa hatua hizo ni mkakati wa kuongeza uzalishaji ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya

nchi (import substitution initiative). Katika kutekeleza hili, Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na wazalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda vinavyoongeza thamani na kuzalisha bidhaa, ili kuhakikisha kuwa tunaongeza tija katika uzalishaji.

**77.** **Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuinua sekta binafsi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeamua kuhuisha mifuko ya udhamini wa mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme - ECGS) na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (Small and Medium Entreprises Credit Guarantee Scheme - SMECGS). Hatua hii itawezesha wazalishaji na wajasiriamali wanaoomba mikopo kupitia kwenye benki za hapa nchini kupata mitaji, mitambo na malighafi kwa urahisi zaidi na kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa bei inayokidhi ushindani wa soko la nje.

**78.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, hususan katika sekta zinazoingiza fedha nyingi za kigeni ikiwemo utalii na madini ili kuongeza uwekezaji na tija kwenye sekta hizo. Kipekee, Serikali inaangalia uwezekano wa kuuza makaa ya mawe kwa wingi zaidi nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni, kwani mahitaji ya bidhaa hii kwa sasa ni dhahiri. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza sera ya fedha ili kuhakikisha utulivu wa bei, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza ushindani na hivyo kuwa na ufanisi katika soko la jumla la fedha za kigeni (Interbank Foreign Exchange Market). Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu inakamilisha mchakato wa kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na wa kati nchini kuanzia mwaka wa fedha 2023/24. Mafanikio ya zoezi hili yatasaidia kuongeza akiba ya fedha za kigeni nchini na kukuza sekta ya madini.

**Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni**

**79. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya biashara ikiwemo kutatua changamoto katika biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nchini. Hii ni pamoja na kuchukua hatua madhubuti katika kutatua kilio cha baadhi ya wamiliki wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hasusan katika Mkoa wa Arusha, ambao hawakuridhishwa na tathmini ya kodi iliyofanywa mwaka 2018/19. Hivyo, Serikali ilipitia upya tathmini hiyo na kuwezesha baadhi ya wamiliki wa maduka kurejeshewa kiasi cha shilingi bilioni 8.9 ambazo zilikuwa zimemelipwa kama kodi kupitia tathmini ya awali.

**80. Mheshimiwa Spika**, hadi Mei 2023, Serikali ilikuwa imetoa leseni kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni nane (8) yenye matawi 36, ambapo matawi 24 yamefunguliwa Tanzania Bara na matawi 12 yamefunguliwa Zanzibar. Aidha, Benki Kuu inaendelea kupokea, kuchambua na kutoa leseni kwa wamiliki wanaokidhi vigezo vilivyopo. Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuhamasisha mabenki kuingiza mashine za kubadilishia fedha (Forex ATM).

**81. Mheshimiwa Spika**, **Serikali inakusudia kuimarisha zaidi mazingira ya biashara kwa kufanya mapitio ya Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya Mwaka 2019 ikiwemo mtaji**, kwa lengo la kurekebisha masharti yaliyopo kwa sasa ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni. Pamoja na masuala mengine, mapitio hayo yanatarajia kuanzisha madaraja ya maduka hayo kulingana na kiwango cha mtaji ambacho kinaweza kukidhi maeneo yenye wateja wengi na wachache. Mapitio hayo yanalenga pia kuweka utaratibu utakaowezesha hoteli za kitalii nchini kutoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wao, ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma hii na hivyo kuchangia kutatua changamoto ya soko lisilo rasmi la kubadilisha fedha za kigeni nchini (black-market). Nitoe rai kwa umma kuendelea kutoa ushirikiano katika kupambana na soko haramu la kubadilisha fedha za kigeni.

## Mabadiliko ya Tabianchi

**82. Mheshimiwa Spika**, Tanzania kama zilivyo nchi nyingine inakabiliwa na vihatarishi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazosababishwa na uzalishaji wa hewa ukaa.
Ikumbukwe kuwa sehemu kubwa ya uchumi wa Tanzania hutegemea shughuli za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na utalii ambazo kwa kiasi kikubwa huathirika na mabadiliko ya tabianchi. Ni dhahiri kuwa madhara ya mabadiliko ya tabianchi ni hatarishi kwa ukuaji wa uchumi, usalama wa chakula, uzalishaji na maendeleo ya viwanda. Hivyo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) unaojumuisha kilimo cha umwagiliaji.

**83. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mwanachama wa mfuko wa *Global Environmental Facility* ambapo kwa kipindi cha miaka minne (2022/23 - 2025/26), Tanzania imetengewa jumla ya dola za Marekani milioni 33.59 kwa ajili ya miradi ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Ili kuweza kunufaika na fedha hizo, natoa rai kwa Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta na watendaji kuandaa miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ili kuongeza fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## IV. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

### Mapato ya Serikali

**84. Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2022/23, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 41.48 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi Aprili 2023, jumla ya shilingi trilioni 32.43 zilipatikana kutoka vyanzo hivyo. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania yalikuwa ni shilingi trilioni 18.81, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 23.65;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali yalifikia shilingi trilioni 2.07, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 3.35;

(iii) Mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 788.8, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 1.01;

(iv) Misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trilioni 4.61, ambapo lengo la mwaka ni shillingi trilioni 4.65;

(v) Mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani ilifikia shilingi trilioni 4.68, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 5.78; na

(vi) Mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka vyanzo vya nje ilifikia shilingi trilioni 1.47, ambapo lengo la mwaka ni shilingi trilioni 3.03.

**Matumizi ya Serikali**

**85. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 41.48 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mwaka 2022/23. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 32.43. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 20.94 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 11.49 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Sehemu kubwa ya fedha za maendeleo zimeelekezwa katika utekelezaji wa: mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) unaojumuisha ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa; mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Julius Nyerere (MW 2,115); ujenzi wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi); miradi ya ujenzi wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji; ujenzi wa mindombinu ya Mji wa Serikali –

Mtumba; miradi ya barabara; na miradi ya kuimarisha huduma za jamii (maji, afya na elimu).

**Ulipaji wa Malimbikizo ya Madai**

**86. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kulipa malimbikizo ya madai na madeni ya wakandarasi, wazabuni, watoa huduma na watumishi. Hadi Aprili 2023, Serikali imelipa madeni na madai mbalimbali yenye jumla ya shilingi trilioni 1.20. Hatua hiyo ni utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Madai na Madeni ya Serikali wa Mwaka 2022 wenye lengo la kuifanya Serikali ifikapo mwaka 2025/26 kuwa na kiwango kinachokubalika kimataifa cha malimbikizo ya madai na madeni kisichozidi asilimia mbili (2) ya bajeti. Niwaelekeze Maafisa Masuuli kufanya uhakiki wa malimbikizo ya madai na madeni katika mafungu yao pamoja na kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410.

**Deni la Serikali**

**87. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2023, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 79.10, sawa na ongezeko la asilimia 13.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 69.44 Aprili 2022. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 27.94, sawa na asilimia 35.3 na deni la nje ni shilingi trilioni 51.16, sawa na asilimia 64.7. Kati ya deni la nje, deni lenye masharti nafuu ni shilingi trilioni 37.69, sawa na asilimia 73.6, hivyo, sehemu kubwa ya deni la nje ni mikopo yenye masharti nafuu.

**Uhimilivu wa Deni**

**88. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika Desemba 2022 ilionesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa: uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 32.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la

Taifa ni asilimia 18.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 120 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180. Aidha, uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ni asilimia 13.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15. Matokeo haya yanawiana na matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa na Shirika la Fedha la Kimataifa na kuchapishwa Aprili 2023.

**89. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza hatua zifuatazo:

(i) Kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu kadri inavyopatikana. Hali hiyo inajidhihirisha katika bajeti inayopendekezwa ambapo mikopo nafuu imeongezeka kwa asilimia 22.8 na yenye masharti ya kibiashara imepungua kwa asilimia 14.4;

(ii) Kuelekeza mikopo yenye masharti ya kibiashara katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi; na

(iii) Kuboresha mikakati ya kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali.

## V. BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**90. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2023/24 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Mpango huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayotekelezwa kupitia Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26). Aidha, dhima kuu ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni "***Kuchochea Kasi ya Ukuaji wa Uchumi, Kuhimili na***

***Kukabili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji ili Kuboresha Hali ya Maisha***".

**Shabaha za Uchumi Jumla**

**91. Mheshimiwa Spika**, kutokana na nyaraka na miongozo iliyozingatiwa katika uandaaji wa Bajeti hii, shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 – 7.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 11.5 ya mwaka wa fedha 2022/23;

(iv) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka wa fedha 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 14.4 mwaka wa fedha 2022/23;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**Misingi ya Bajeti**

**92. Mheshimiwa Spika**, misingi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(iii) Kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kushuka kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini;

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani; na

(vi) Kuendelea kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii.

**Mikakati ya Kuongeza Mapato ya Serikali**

**93. Mheshimiwa Spika**, mikakati ya kuongeza mapato katika mwaka wa fedha 2023/24 inajumuisha:

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo kuendelea kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;

(ii) Kuongeza wigo wa mapato kwa kusajili biashara na walipakodi wapya pamoja na kuendelea na jitihada mbalimbali za kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kutoa elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi wa hiari;

(iii) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(iv) Kuendelea kusimamia wizara na taasisi za Serikali kutumia Mfumo wa Serikali wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuhakikisha malipo yote ya Serikali yanafanyika kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number);

(v) Kusimamia matumizi sahihi ya EFD ili kudhibiti upotevu wa mapato na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi;

(vi) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa kwa: kufanya tathmini ya mfumo wa kisheria unaotumika kutoa na kusimamia motisha za kikodi ili kubaini ufanisi katika kufikia malengo tarajiwa; na kuboresha pamoja

na kuhamasisha uwekezaji kwa kutumia vivutio visivyo vya kikodi kama vile ardhi, miundombinu ya maji, barabara na nishati;

(vii) Kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi;

(viii) Kuendelea kuimarisha mifumo na usimamizi wa mashirika, taasisi za umma na wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa wakati;

(ix) Kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha uwekezaji kwenye soko la ndani la dhamana za Serikali;

(x) Kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na kutekeleza makubaliano ya kimkataba ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo kama ilivyopangwa;

(xi) Kutumia fursa iliyopatikana kutokana na zoezi la *credit rating* ili kuongeza mitaji ya uwekezaji kutoka kwenye soko la fedha la kimataifa kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo; na

(xii) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Vyanzo Mbadala (Alternative Project Financing - APF) ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**94. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua migogoro na kuhakikisha haki inatendeka baina ya walipakodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali ya CCM chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imekamilisha taratibu za uanzishwaji wa ofisi huru ya *Tax Ombudsman* ambayo imeanza majukumu yake Februari 2023.

**Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi ya Serikali**

**95. Mheshimiwa Spika**, mikakati ya kusimamia matumizi inalenga kuongeza tija na ufanisi pamoja na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo;

(ii) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kuendesha vikao kwa njia ya mtandao na kupunguza matumizi ya karatasi (paperless);

(iii) Kuimarisha usimamizi wa mashirika, wakala na taasisi za Serikali ili yajiendeshe kwa ufanisi na kuipunguzia mzigo Serikali;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwa wakati ili kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi; na

(v) Kufanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ili kuufanya mfumo wa ununuzi wa umma kuwa wa kimkakati pamoja na kuziba mianya ya ubadhirifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali.

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na zoezi la kujenga mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi kwa kutumia wataalamu wa ndani. Lengo la mfumo huo ni kuongeza ufanisi katika ununuzi wa umma na kuwezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha. Aidha, pamoja na mambo mengine, mfumo huo utaweka bei ya ukomo kwa ununuzi wa baadhi ya bidhaa na huduma ili kuiwezesha Serikali kununua kwa bei ya soko. Mfumo huo unatarajiwa kuanza kutumika ifikapo Julai 2023.

**Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2023/24**

**97. Mheshimiwa Spika**, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24, maeneo ya vipaumbele ni pamoja na kuendelea

kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati ikiwemo miradi ya: ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR); kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115); kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG); kuzalisha umeme wa maji wa Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222); ujenzi wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi); ujenzi wa barabara na madaraja makubwa; na kuendeleza kanda maalumu za kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo. Aidha, Serikali itaendelea na uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa makubwa 100. Miradi hiyo inatarajiwa kuwa na matokeo makubwa na ya haraka katika uchumi, ikiwemo kuzalisha ajira na kuongeza kipato.

**98. Mheshimiwa Spika**, sanjari na miradi ya kielelezo inayoendelea, utekelezaji wa miradi mingine kwa mwaka wa fedha 2023/24 utazingatia maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na uwekezaji; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Waheshimiwa Wabunge, miradi mahususi katika maeneo haya ambayo itatekelezwa katika majimbo yetu ni kama nilivyowasilisha kwenye hotuba yangu leo asubuhi kuhusu *Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24*.

**99. Mheshimiwa Spika**, upangaji wa vipaumbele vya Taifa umezingatia fursa na faida zilizopo Tanzania ambazo ni pamoja na:

(i) Upatikanaji wa rasilimali za kutosha ikiwemo ardhi, misitu, madini, gesi asilia, vituo vya utalii pamoja na uwepo wa vyanzo vya maji (bahari, mito na maziwa);

(ii) Uwepo wa nguvukazi kubwa ya Taifa ambayo ni vijana;

(iii) Ukuaji wa miji ambao umekuwa ukifungua fursa nyingi za kiuchumi;

(iv) Uwepo wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ambao unaweza kutumika nchini na nchi jirani;

(v) Faida ya kijiografia ambayo huwezesha Tanzania kutumika kama lango la biashara na uchumi kwa nchi za EAC, SADC na COMESA; na

(vi) Amani, umoja na utulivu wa uchumi.

**Mambo Mahususi ya Kuzingatia**

**100. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuwasilisha maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua zingine za mapato naomba nisisitize mambo mahususi kama ifuatavyo:

**101. Mheshimiwa Spika**, **jambo la kwanza**, Ibara ya 138(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania inatoa masharti ya kutoza kodi. Hakuna kodi ya aina yeyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu ya kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge. Nchi zote zilizoendelea duniani zinaendeshwa kwa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Wastani wetu wa kulipa kodi sio mzuri sana ukilinganisha na ukuaji wa uchumi, ongezeko la watu na ongezeko la mahitaji. Mathalan, kwa mwaka 2021/22, walipakodi waliosajiliwa walikuwa 4,455,028 ambapo kati ya hao wenye TIN za biashara ni 1,641,173. Hata hivyo, katika kipindi hicho, takriban shilingi trilioni 16.75, sawa na asilimia 80 ya mapato ya TRA yalilipwa na idadi ndogo (asilimia 20) ya walipa kodi wenye TIN za biashara.

**102. Mheshimiwa Spika**, mbali na ukweli kuwa idadi ya walipakodi walioandikishwa ni ndogo, bado kuna mwamko mdogo kwenye ulipaji Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Kodi ya Mapato (Income Tax) na kodi ya Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty). Jambo hilo linasababisha viwango vya kodi kuwa vikubwa kwa kuwa mzigo huo unabebwa na walipakodi wachache. Kwa wauzaji, kodi imekuwa ikitumika kama *discount rate* ambapo muuza duka akitaka kumpunguzia bei mteja anamuuliza kama ampe bei yenye risiti ya

TRA au bei ya bila risiti. **Hili ni kosa kisheria!** Wakati mwingine wafanya biashara wanatoa visingizio mbalimbali ikiwemo mtandao kuwa chini na mashine kuharibika au kujizungusha hadi mnunuaji aondoke. **Hili ni kosa kisheria! Aidha, kuna baadhi ya wananchi tukiwemo viongozi na watumishi wa umma na taasisi za Serikali hatujali kudai risiti. Kitendo hiki kinaikosesha Serikali mapato, kujinyima maendeleo na kuwanufaisha wafanyabiashara wachache wasiotoa risiti kuchukua fedha yako kwa niaba ya Serikali huku wakiwa hawana wajibu wowote kwenu wa kutoa huduma au kutekeleza miradi ya maendeleo.** Vitendo vya namna hii vinaongeza utofauti wa kipato kati ya walio nacho na wasio nacho.

**103. Mheshimiwa Spika**, kumezuka dhana ya kuona kuwa kodi zinazotozwa ni kubwa bila kujali mzigo mkubwa wa Serikali kwa nchi yetu katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma za jamii. ***Kuna baadhi ya wanasiasa wanasema kodi hizi ni za Samia, kodi hizi za Mwigulu, kodi hizi za TRA.*** Waheshimiwa Wabunge, kodi zote zinazokusanywa huwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali uliopo Benki kuu ya Tanzania, na baadae kupelekwa kwenye Wizara za Kisekta. Fedha hizo ndizo zinazotumika kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo mijini na vijijini ikiwemo miradi ya umeme, maji, barabara, madaraja, vivuko, reli, usafiri wa anga, madarasa, zahanati, ununuzi na usambazaji wa dawa na malipo ya mishahara ya watumishi kama walimu, wauguzi na madaktari. *Kila mmoja wetu ajue kuwa, Kodi sio jambo la Rais, kodi sio jambo la Waziri wa Fedha, kodi sio jambo la TRA,* **KODI NI JAMBO LA NCHI, KODI NDIO MAENDELEO YA NCHI YETU**.

**104. Mheshimiwa Spika**, kila Mtanzania mwenye sifa za kulipa kodi ana wajibu wa kulipa kodi stahiki na halali kwa mujibu wa sheria. **NI LAZIMA KULIPA KODI!** Ni lazima tutumie mashine za EFD bila udhuru wowote, ni lazima kila anayeuza atoe risiti na anayenunua adai risiti. Mtu yeyote ambaye hataki kusumbuliwa kwenye masuala ya kodi na masuala ya risiti, ni sharti atii sheria za kodi, vinginevyo utakutana na mkono wa sheria. Nawaelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendelea kukusanya kodi kwa weledi na kwa kuzingatia Katiba, sheria na kanuni kama alivyoelekeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Serikali inaendelea na ujenzi wa mifumo ya kodi za forodha na kodi za ndani na kujenga mifumo inayosomana kikamilifu kwenye upande wa makusanyo na upande wa matumizi ili kuyapatia ufumbuzi wa kudumu malalamiko yanayojitokeza kwenye masuala ya usimamizi kodi hapa nchini.

**105. Mheshimiwa Spika**, **jambo la pili** ni usimamizi na udhibiti wa fedha za umma ambapo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - CAG ilionesha kuwa bado kuna dosari katika matumizi ya fedha za umma, hususan katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kudhibiti upotevu wa fedha za umma. Hii imedhihirishwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM**, wakati akipokea taarifa ya CAG tarehe 28.03.2021 kwa kutoa maelekezo mahususi ya kuongeza uwazi na kutoficha jambo lolote kwenye taarifa za ukaguzi. Nanukuu "**CAG naomba sana ulimi wako usiwe na utata, kama kuna shirika halifanyi vizuri tuambie hili halifanyi vizuri. Kama kuna bodi haisimamii vizuri tuambie bodi hii haisimamii vizuri, kwa sababu tutakaposema mapungufu ndipo tutakapoweza kurekebisha na tutaweza kufanya vizuri zaidi, tukinyamaziana kwa kutizamana sura hatutarekebisha na tutaumiza wananchi. Naomba sana *report* yako iwe wazi zaidi, utakaponiletea ukaguzi wa mashirika naomba uwe wazi zaidi ili tujue tunachukua hatua gani**".

**106. Mheshimiwa Spika**, jambo lingine linaloonesha nia ya dhati ya kusimamia fedha za umma, Serikali ilifuatilia na kugundua upungufu katika mifumo ya ukaguzi wa kifedha na taratibu za ununuzi. Niwakumbushe watanzania kwamba baada ya kuona hilo, katika mwaka 2022/23, Serikali ya CCM chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, iliiongezea fedha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa ajili ya kuajiri watumishi zaidi ya 100 ili CAG aweze kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha (Value for Money) na ukaguzi kwa wakati (Real Time Audit) kwenye miradi yote mikubwa na matokeo yake ndio yanaonekana.

**107. Mheshimiwa Spika**, Serikali inafanyia kazi hoja za ukaguzi zilizotolewa na CAG na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale watakaothibitika kuwa ni wavunjifu wa sheria na kusababisha upotevu wa fedha za umma bila kujali mkubwa wala mdogo kama alivyoelekeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuwekeza kwenye mifumo ya TEHAMA pamoja na kuchukua hatua kali pale panapothibitika uwepo wa uvunjifu wa sheria. **Hizi ni hatua za kulinda mali za umma na ni hatua za kukabiliana na watumishi wa umma wanaotumia vibaya fedha za walipa kodi**.

**108. Mheshimiwa Spika, jambo la tatu** ni hali ya umaskini ambapo pamoja na utajiri tulionao na hatua kubwa iliyopigwa, nchi yetu bado ina wananchi maskini. Kiwango cha umaskini cha mahitaji ya msingi kitaifa kinapimwa kwa kuangalia wanakaya wanaoishi kwa kutumia **chini ya shilingi 49,320** kwa mwezi kwa mtu mzima kwa ajili ya kupata mahitaji ya msingi. Vilevile, kiwango cha umaskini uliokithiri (umaskini wa chakula) unapimwa kwa kuangalia wanakaya wanaoishi kwa kutumia **chini ya shilingi 33,748** kwa mwezi kwa mtu mzima hivyo kushindwa kumudu kupata chakula chenye kalori 2,200 zinazotakiwa kwa mtu mzima kwa siku.

**109. Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2017/18 ulionesha kuwa **asilimia 26.4** ya watanzania walikuwa wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi, hali hii imepungua kutoka **asimilia 28.2** kwa mwaka 2012. Tanzania imefanikiwa kupunguza kiwango cha umaskini uliokithiri kutoka **asilimia 9.7** kwa mwaka 2011/12 hadi **asilimia 8.0** mwaka 2017/18. Hata hivyo, kiwango cha umaskini kimeendelea kupungua lakini siyo kwa kasi ya kuridhisha hivyo bado kuna watanzania maskini.

**110. Mheshimiwa Spika**, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zimekuwa zikitekeleza mipango mbalimbali inayolenga kupunguza wimbi la umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini uliokithiri. Ukanda wa Afrika Mashariki umekuwa na viwango vya juu vya umaskini vikitofautiana miongoni mwa nchi wanachama.

Hata hivyo, nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kupambana na umaskini japokuwa kasi ya upunguaji wa umaskini ni ndogo.

**111. Mheshimiwa Spika, jambo la nne** ni tatizo la ajira kwa vijana ambapo pamoja na hatua kubwa zilizochukuliwa za kujenga uchumi wa Nchi yetu bado vijana wengi hawana ajira. Kiwango cha ukosefu wa ajira nchini Tanzania kimekuwa kikipungua katika miaka ya hivi karibuni. Utafiti wa Nguvukazi wa mwaka 2020/21 ulibaini kuwa **ukosefu wa ajira katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 au zaidi ulipungua hadi asilimia 9.3 kutoka asilimia 10.5 mwaka 2014.** Kupungua kwa kiwango hiki ni matokeo ya juhudi mbalimbali zilizotekelezwa na Serikali, ingawa viwango vya ukosefu wa ajira bado ni vya juu na vinahitaji juhudi zaidi kuvipunguza. Aidha, hali ya ukosefu wa ajira **kwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35 nchini Tanzania imekuwa ikiongezeka kutoka asilimia 12.1 kwa mwaka 2014 hadi aslimia 12.6 kwa mwaka 2020/21**.

**112. Mheshimiwa Spika,** tatizo hili la ajira ni kubwa zaidi hasa kwa vijana wa kike (asilimia 16.7) ikiwa ni mara mbili ya kiwango kwa vijana wa kiume (asilimia 8.3). Tatizo hili ni la kihistoria tangu uhuru wa nchi yetu ambapo wakati tunapata uhuru tulikuwa na madakitari 12, wahandisi 2, tulikuwa na chuo kikuu kimoja kilichodahili wanafunzi 14, shule za sekondari zilikuwa 41 na wanafunzi 11,832, shule za msingi zilikuwa 3,270 na wanafunzi 486,470. *Hii inamaanisha nini?* Tulipopata uhuru kazi ya kwanza ilikuwa ni kujenga sekta ya utumishi wa umma ambapo viongozi wote wa Serikali na wananchi wote walihamasisha watoto waende shule ili wawe watumishi wa Serikali. Kwa kipindi hicho, iliwezekana kuajiri wahitimu wote serikalini kwa nafasi ambayo muhitimu ataipendelea hata bila uwepo wa sekta binafsi.

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa sasa vyuo vimeongezeka kutoka **kimoja (1) hadi 52** na wahitimu kutoka 14 hadi takribani **500,323** kutoka vyuo vya ufundi, vyuo vya kati, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Shule za sekondari zimeongezeka kutoka **41** hadi **5,540** na wahitimu kutoka **11,832** hadi **2,823,588**. Aidha, shule za msingi zimeongezeka kutoka **3,270** hadi **19,261** na wanafunzi wakiongezeka kutoka **486,470** hadi wanafunzi **11,420,973**. Hali hii imebadili kabisa 'equation' kutoka wahitimu kupokea barua

zikimwomba achague kazi hadi kufikia uwezekano wa kila kijiji kuwa na mhitimu wa ngazi fulani ambaye hana ajira. *Sasa sio ajabu kukuta familia mmoja yenye mzee mstaafu kuwa na wategemezi ambao ni vijana wahitimu wanaoishi kwa kutegemea pension ya mstaafu.*

**114. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine tulikuwa na aina ya uchumi ambao sekta ya umma ndio inafanya kila kitu ikiwemo biashara na umiliki wa vitu vyote. Hivyo, hata tulipo binafsisha mashirika ya umma na uchumi kutegemea zaidi sekta binafsi, wengi hatujaiamini na kuiheshimu sekta binafsi kama ilivyo sekta ya umma pamoja na kuwa sekta binafsi ni mhimili wa uchumi. Waheshimiwa Wabunge, bado jamii yetu haiamini kuwa mtu anaweza kutajirika kupitia sekta binafsi na hata akitajirika inaaminika ni mwizi, hali inayoua uwekezaji wa ndani na nje.

**115. Mheshimiwa Spika**, **hali ilivyo sasa,** wawekezaji wa ndani wakijaribu kupiga hatua wanapigwa vita na kukatishwa tamaa. Hata wamiliki wa ardhi hawapati fidia stahiki pale wawekezaji wanapohitaji kumilikishwa ardhi hizo kana kwamba watanzania hawatakiwi kutajirika. Nitoe rai kwa watendaji wa Serikali, kutoa fursa kwa wamiliki wa ardhi kunufaika na maeneo wanayomiliki pale wawekezaji wanapihitaji ardhi kwa ajili ya kuwekeza nchini. **Acheni watanzania walipwe pesa nyingi, acheni watanzania watajirike!**

**116. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa wawekezaji wa nje, licha ya kwamba wawekezaji hao wanaleta mtaji, teknolojia, ajira, kuongeza mapato kwa Serikali na kukuza uchumi, uzoefu unaonesha kuwa, wawekezaji hao wanakumbana na vikwazo kuliko uwezeshaji ndani ya Serikali na hata kwa wananchi. Kwa upande wa Serikali, kila ofisi anayoingia mwekezaji, wanatafuta kipengele kinachoweza kumkwamisha ili wazo lake likwame badala ya kutafuta namna nzuri ya kufanikisha uwekezaji. Kwa upande wa wananchi, atakutana na mtazamo wa uraiani mathalani mwekezaji anapofika na mtaji wa kuwekeza kwenye meli na bandari ya uvuvi wa samaki kwenye kina kirefu ambao hata wasipovuliwa watahama na kuvuliwa sehemu nyingine, ***mosi utasikia ana fedha kweli, huyu sio tapeli kweli? Pili wakijiridhisha ana fedha, utasikia huyu hatatuibia kweli? Tatu akitokea***

***anayeshauri kwamba nadhani uwekezaji huu ni muhimu kwa ajili ya nchi utasikia huyu lazima ameshapewa fedha, amelambishwa asali huyu*. Ni lazima tukubali uwekezaji ikiwemo kuwapa majina mazuri wanaobeba hatima za wengine.**

**117. Mheshimiwa Spika**, jawabu la ukosefu wa ajira kwa vijana na kuondoa umaskini kwa watanzania ni kukuza uwekezaji, hususan katika sekta za uzalishaji na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Maono ya Mheshimiwa Rais wetu ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi ni maono sahihi na kwa wakati sahihi. Hivyo, ni lazima watendaji wote serikalini wawe na nidhamu ya kuilea na kuiwezesha sekta binafsi kukua na kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi. **Tunatumia nguvu kubwa sana kwenye kudhibiti kuliko nguvu tunayoitumia kuwezesha. Lazima tuheshimu sekta binafsi na kutambua mchango wake katika kutoa ajira, kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Nitoe rai kwa watanzania wenzangu tuwe na nidhamu katika kuiwezesha sekta binafsi kukua.**

**Kuimarisha Sekta za Uzalishaji**

**118. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeamua kuchukua hatua mahususi za muda mfupi, wa kati na mrefu. Miongoni mwa hatua hizo ni mkakati wa kuongeza uzalishaji ili kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Katika kutekeleza hili, Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na wazalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda vinavyoongeza thamani na kuzalisha bidhaa ili kuhakikisha kuwa tunaongeza tija katika uzalishaji wetu. Aidha, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itahuisha Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme). Katika kutekeleza mkakati huo, jumla ya shilingi bilioni 600 zinatarajiwa kutumika ambapo Benki Kuu ya Tanzania itatoa shilingi bilioni 280 na Benki ya Dunia itatoa mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 150. Hatua hii itawezesha uzalishaji na kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi.

**119. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi**, imeamua kuanza upya kuziongezea mtaji benki zake za kimkakati yaani Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB, Benki ya Maendeleo TIB (TIB Development Bank) na Benki ya Biashara Tanzania – TCB. Serikali inakamilisha taratibu za kuzipatia mtaji TADB na TIB Development Bank jumla ya shilingi bilioni 235.9 baada ya kuzifanyia tathmini ya kina ili kufahamu hali halisi ya benki hizo na kuhakikisha mtaji unaowekwa haupotei. Programu hiyo ya kuziongezea mitaji benki za TADB na TIB Development Bank itaendelea kwa kipindi cha miaka mitano hadi kumi kwa kuzingatia mwenendo na uelekeo wa benki hizo ili hatimaye ziweze kuwa na mtaji usiopungua shilingi trilioni moja kwa kila benki. Aidha, benki ya TCB imepewa mtaji wa shilingi bilioni 30 na kiasi kingine cha shilingi bilioni 101 kitatolewa. Lengo la hatua hizi ni kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya miradi ya kukuza sekta za uzalishaji na uongezaji wa thamani.

**Utendaji wa Taasisi za Udhibiti**

**120. Mheshimiwa Spika**, sisi sote ni mashahidi wa jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, katika kuendelea na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi mbalimbali za udhibiti nchini na kufuta au kupunguza ada na tozo kero. Hata hivyo, pamoja na maboresho hayo, bado kumekuwa na changamoto ya taasisi nyingi za udhibiti zinazosimamia sekta mbalimbali kuongeza kero za ufanyaji wa biashara na uwekezaji kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo: kukosekana kwa mfumo mmoja wa ulipaji ada na tozo; **kuwepo kwa viwango vikubwa vya adhabu ambavyo hutumika kama vyanzo vya mapato; na uwepo wa kaguzi nyingi zisizokuwa na tija, hivyo kuongeza usumbufu katika kufanya biashara. Hali hii imesababisha Serikali kuendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara kuhusu kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, uwekezaji na ufanyaji wa biashara nchini.**

**121. Mheshimiwa Spika**, uzoefu umeonesha kuwa: kaguzi nyingi zinafanyika kwa lengo la kutafuta makosa badala ya lengo la msingi la kuzuia kutokea kwa athari hasi; kaguzi nyingi kufanywa na taasisi mbalimbali na kila moja kwa wakati wake hivyo wafanyabiashara kutumia muda mwingi kupokea wageni badala ya kujihusisha na shughuli za uzalishaji na huduma; adhabu kubwa zinasababisha biashara kufanyika kwa hasara; ukubwa wa adhabu unaotoa fursa ya majadiliano (human interaction) kati ya watendaji na wafanyabiashara na hivyo kuipotezea Serikali mapato; adhabu kutumika kama motisha na chanzo cha mapato ya taasisi za udhibiti; na utitiri wa tozo, ada na adhabu na kutokuwepo kwa mfumo jumuishi wa kuzilipa.

**122. Mheshimiwa Spika**, **katika kutatua kero hizo, napendekeza kuanza matumizi ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (Single Window Payment System) na taasisi za udhibiti kuweka utaratibu mzuri wa ukaguzi ambao hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo. Napendekeza hatua hizo zianze mwaka wa fedha 2023/24**.

**123. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kusimamia ujenzi wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa Njia ya Kielektroniki (Tanzania Electronic Investment Single Window - TeIW). Mfumo huo unatarajiwa kuunganisha pamoja taasisi zinazohusika na kuwezesha uwekezaji ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC); Shirika la Viwango Tanzania (TBS); Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA); Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC); Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO); na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

**124. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo huo, kutakuwa na manufaa kwa wawekezaji ikiwemo: kuweza kusajili mradi popote ndani na nje ya nchi bila kuonana na watoa huduma wa taasisi husika; kupata kipaumbele cha kuhudumiwa kwa haraka katika taasisi zinazotoa huduma; kuweza kuingiza

taarifa zake mara moja kwenye mfumo wa TeIW; na kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku tatu (3).

**125. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na utaratibu unaochipukia kwa kasi wa taasisi mbalimbali za Serikali na Halmashauri **kufunga biashara, ofisi na maeneo mengine ya uzalishaji** baada ya kufanya kaguzi na kuthibitisha ukiukwaji wa sheria mbalimbali tunazosimamia. Ufungaji wa biashara, kwa sababu zozote zile, una athari kubwa kwa ustawi wa uchumi wetu kwa kuathiri ajira za wananchi, ustawi wa biashara, mapato ya kampuni na mapato ya Serikali. Aidha, utaratibu huu unakwenda kinyume na juhudi kubwa za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

**126. Mheshimiwa Spika**, ili kuondokana na athari hizo, napendekeza kuanzia tarehe 1 Julai 2023, iwe ni marufuku kwa taasisi yoyote ya Serikali kufunga biashara, ofisi ama maeneo yoyote ya uzalishaji kwa kigezo cha kukiuka taratibu mbalimbali. Aidha, napendekeza sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zirekebishwe ili kumchukulia hatua mwenye biashara kwa makosa ya biashara na siyo kuifunga biashara yenyewe. Hatua hii inalenga kulinda ajira za watanzania, mapato ya biashara, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

**127. Mheshimiwa Spika**, kwenye eneo la ugomboaji na uondoshaji wa mizigo bandarini, upo utaratibu unaokataza mwagizaji kuondosha mizigo bandarini pale ambapo kodi iliyokadiriwa inabishaniwa hadi pale kodi husika itakapolipwa yote. Utaratibu huu umeathiri kwa kiwango kikubwa uanzishwaji, ushamirishaji na ukuzaji wa biashara nchini na umepunguza kasi ya matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kama lango la biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Ili kuondokana na athari hizo, **napendekeza kuanzisha utaratibu utakaow ezesha waagizaji wa mizigo wenye mapingamizi ya kodi iliyokadiriwa kuweza kugomboa mizigo hiyo baada ya kulipa kodi isiyobishaniwa.** Aidha, utaratibu maalum utawekwa chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki utakaolinda mapato ya Serikali na kuwezesha biashara kuendelea. **Hata hivyo, mfanyabiashara atakayebainika kukiuka utaratibu huo**

**atalazimika kulipa kodi iliyocheleweshwa, faini, kifungo jela au vyote kwa pamoja**.

**VI. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO**

**128. Mheshimiwa Spika**, kuanzia kipindi cha mwaka 2019/20, Dunia imepita kwenye changamoto kubwa ya kiuchumi kufuatia kuenea kwa janga la uviko-19 na baadaye kuzuka kwa vita ya Urusi na Ukraine Februari 2022. Hii imeathiri si tu upatikanaji wa bidhaa muhimu katika soko la Tanzania lakini pia imesababisha mfumuko wa bei, kupanda kwa gharama za maisha na kuathiri ukuaji wa uchumi nchini. Vilevile, katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, Dunia imeshuhudia hatua mpya za mdororo wa uchumi, kupanda kwa mfumuko wa bei, na upungufu mkubwa wa fedha za kigeni (Dola ya Marekani).

**129. Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, Serikali imeendelea na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan makaa ya mawe, jasi, chumvi, almasi, mawe ya chokaa na shaba; kuongezeka kwa shughuli za utalii kutokana na Programu maalumu ya Tanzania - *The Royal Tour*. Hatua za Mapato kwa mwaka wa Fedha 2023/24 zinalenga Kuongeza kasi ya Kufufua Uchumi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji kwa ajili ya Kuboresha Maisha ya Watanzania.

**130. Mheshimiwa Spika**, Marekebisho yanatarajiwa pia kujibu maswali na kukidhi kiu ya jamii ya Watanzania yakilenga kuchachua shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi kwa kuweka mkazo katika sekta za kimkakati kama vile viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, miundombinu ya umeme, uchukuzi na usafirishaji na sekta za kijamii za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji, kukuza uchumi jumla, kukuza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi ("Macro economic objectives for economic growth"). Aidha, Hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali ("Domestic Revenue Mobilization and Improvements in Tax Administration"). Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo:

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;

(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;

(d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;

(e) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;

(f) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289;

(g) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;

(h) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, 2015 na Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306;

(i) Sheria ya Uhamiaji, SURA 54;

(j) Sheria ya Ardhi, SURA 113;

(k) Sheria ya Madini, SURA 123;

(l) Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82;

(m) Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84;

(n) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;

(o) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196

(p) Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

(q) Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint); na

(r) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

**(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**131**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kima cha usajili kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200. Serikali itaendelea kuongeza kima husika hadi kufikia shilingi milioni 500 ili kuepusha athari za kimapato zinazoweza kujitokeza. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Kodi ya Ongezeko la Thamani na kuchochea ulipaji kodi wa hiari. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 75,333** kwa kuwa walipakodi wenye mauzo ghafi kati ya milioni 100 hadi milioni 200 ni wengi lakini wamekuwa na madai zaidi kuliko kiasi kinacholipwa kutokana na udanganyifu. Hivyo, walipakodi hawa wataacha kudai Serikali kodi itokanayo na manunuzi yao, sambamba na kupunguza gharama za usimamizi;

ii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza viuatilifu vya mimea (insecticides) na vya mifugo (acaricides) zinazotambulika kwa *HS Code* 2916.32.00 (Benzalkonium Chloride) na *HS Code* 2916.32.00 (Glutaraldehyde). Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa viuatilifu vya mimea na mifugo nchini na kulinda viwanda vya ndani. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 6.8;**

iii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye hema za chuma (prefabricated structures) zinazotambulika kwa *HS Code* 9406.20.90 zitakazoagizwa na kutumiwa na wafugaji wa kuku. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye sekta ya mifugo, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Aidha, msamaha husika utatolewa baada ya mfugaji kusaini Mkataba wa Utekelezaji (Performance

Agreement) na Serikali. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 465.6**;

iv. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake vinavyouzwa nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga kwa kuwawezesha kununua bidhaa husika nchini au kuagiza kutoka nje ya nchi bila kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hatua hii itafuta uamuzi uliochukuliwa mwaka 2022/23 ili kuendana na dhamira ya kukuza sekta ya utalii sambamba na hatua ya Mheshimiwa Rais ya kuhamasisha Sekta hii kupitia filamu yake ya "Royal Tour";

v. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini ya thamani, madini ya vito na madini mengine ya thamani yanayouzwa katika masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini vilivyoanzishwa na Tume ya Madini au vituo vya kusafishia dhahabu (refineries) vilivyopo nchini. Lengo la hatua hii ni kuchochea uuzaji wa madini katika masoko na vituo hivyo na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika ukuaji wa Pato la Taifa;

vi. Kuruhusu ahirisho la kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Deferment) kwa bidhaa za mtaji zinazozalishwa ndani ya nchi. Aidha, utaratibu wa ahirisho la ulipaji wa kodi husika kwa bidhaa za mtaji zinazotoka nje ya nchi utasitishwa baada ya miaka mitatu (3). Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji ndani ya nchi, kuongeza ajira, na kuhakikisha viwanda vinapata bidhaa za mtaji kwa bei nafuu;

vii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza vifungashio vya madawa zinazotambulika kwa *heading* 3902 (Polypropylene USP - Medical Grade); na *heading* 3907 (Polyethylene Terephthalate USP). Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio vya dawa nchini, kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya kuwa shindani sokoni. Aidha, msamaha husika utatolewa baada ya mzalishaji kusaini Mkataba wa Utekelezaji (Performance Agreement) na Serikali;

viii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye *moulds* zinazotumika kutengeneza madawa ya binadamu. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa dawa nchini, kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya kuwa shindani sokoni;

ix. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka 1. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani uliotokana na athari za UVIKO na vita vya Urusi na Ukraine;

x. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka 1. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani;

xi. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyumba zinazouzwa na wajenzi wa nyumba za kibiashara zenye gharama nafuu isiyozidi shilingi milioni 50. Lengo ni kutoa unafuu kwa wanunuaji wa nyumba hizo na kuboresha maisha ya watanzania;

xii. Kufanya marekebisho kwenye Kipengele cha 20 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuhusisha *gaming odds* na *gaming software* kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi. Hatua hii inalenga kuongeza mchango wa tasnia ya michezo ya kubahatisha kwenye ukuaji wa Pato la Taifa pamoja na kutoa ufafanuzi wa neno *gaming supply* kwa upana zaidi;

xiii. Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 ili kuakisi mawanda ya bidhaa zilizosamehewa pamoja na kuoanisha *H.S Codes* zilizomo kwenye kitabu cha Viwango vya Pamoja vya Ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African

Community Common External Tariff) cha mwaka 2017 na zile zilizomo kwenye kitabu cha mwaka 2022 kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho Namba 8**; na

xiv. Serikali itaendelea kutoa misamaha ya kodi inayotolewa sasa kwenye Sekta za uzalishaji kama vile kilimo, mifugo na uvuvi. Hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 71,262.4**.

**(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**132**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:

i. Kusamehe Kodi ya Mapato kwenye mapato yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Mfuko wa Kitaifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwenye amana (fixed deposit), hati fungani za muda mfupi (treasury bonds and treasury bills) pamoja na gawio linalotokana na hisa. Lengo la hatua hii ni kufanikisha utoaji huduma za matibabu kwa wanachama wastaafu na wenza wao ambao hawachangii kwenye mfuko baada ya kustaafu;

ii. Kurekebisha kifungu cha 56 cha Sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332 ili miamala ya utoaji wa hisa mpya na uhamishaji wa miliki ya kampuni unaofanyika ndani ya nchi isitozwe Kodi ya Mapato. Lengo ni kuvutia uwekezaji nchini na kutoa ufafanuzi;

iii. Kurekebisha kifungu cha 82 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 ili kuondoa takwa la kutoza Kodi ya Zuio kwenye pango kwa wapangaji wa nyumba binafsi wasiofanya biashara. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea adha wapangaji binafsi kulipa kodi kwa niaba ya mwenye nyumba;

iv. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Mtaji kwenye ubadilishaji wa muundo wa ndani wa Kampuni (internal restructuring) unaofanywa kwa kuzingatia matakwa ya Mikataba ya

Msingi iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji kwa lengo la kutekeleza miradi ya ubia ya uchimbaji wa madini baina ya Serikali na wawekezaji. Lengo la hatua hii ni kuharakisha utekelezaji wa Miradi ya Ubia na kutimiza jukumu la Serikali la kimkataba kwa wakati;

v. Kupunguza Kodi ya Ongezeko la Mtaji (Capital Gain Tax) kutoka asilimia 10 kwenye faida hadi Kodi ya Mapato ya asilimia 3 ya thamani ya mauzo au thamani ya ardhi iliyothaminishwa, (thamani yoyote kubwa kati ya hizo) bila kujali gharama zilizowekezwa katika maeneo husika (investment costs) kwa walipakodi wasiotunza kumbukumbu za manunuzi au uendelezaji wa mali husika. Aidha, kwa mlipakodi anayetunza kumbukumbu za gharama za ununuzi na uendelezaji mtaji ataendelea na utaratibu wa sasa wa kulipa kodi ya asilimia 10 kwenye faida ya mtaji (Capital Gain). Lengo la hatua hii ni kuweka utaratibu rahisi wa ukokotoaji wa kodi kwa mauzo ya mali mtaji kwa wasiotunza kumbukumbu za gharama na hatimaye kuongeza ukuaji wa sekta ya ardhi kwa kurahisisha uhamishaji miliki;

vi. Kurekebisha Kifungu cha 65T cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332, kwa kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari. Utaratibu huu utahusisha walipakodi binafsi (Individuals) pekee ambao hawana wajibu wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi. Lengo la hatua hii ni kutatua changamoto za utekelezaji wa utaratibu uliopitishwa hapo awali wa kuwataka walipakodi wanaoandaa na wasioandaa hesabu za kodi kulipa kodi za awali kulingana na viwango elekezi vya kodi kwa kila gari. Viwango elekezi vya kodi vinavyopendekezwa sasa vitatumika kwa walipakodi binafsi pekee ambao mauzo ghafi yao hayazidi kiasi cha shilingi milioni mia moja na ambao hawawajibiki kuandaa hesabu kisheria. Aidha, maboresho ya viwango vya kodi elekezi kwa kila gari yanalenga kutoa unafuu wa kodi kwa kundi husika na hivyo, kurahisisha utekelezaji wa takwa la kisheria. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 72,211.5;**

**Jedwali Na. 1. Utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato unaopendekezwa kwa wasafirishaji wa Abiria na Mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila Gari**

| **A** | **Daraja A: Magari ya Abiria** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Utaratibu wa Sasa** | | **Utaratibu Unaopendekezwa** | |
| | ***Idadi ya Abiria*** | ***Kiwango*** | ***Idadi ya Abiria*** | ***Kiwango*** |
| 1 | Wasiozidi 10 | 180,000 | Wasiozidi 15 | 250,000 |
| 2 | 11 hadi 15 | 450,000 | 16 hadi 25 | 550,000 |
| 3 | 16 hadi 30 | 720,000 | 26 hadi 45 | 1,100,000 |
| 4 | Abiria hadi 32 | 1,710,000 | 46 hadi 65 | 1,600,000 |
| 5 | Basi la Kawaida | 2,430,000 | Zaidi ya 65 | 2,200,000 |
| 6 | *Semi-Luxury* | 2,610,000 | | |
| 7 | *Luxury* | 2,790,000 | | |
| | | | | |
| **B** | **Daraja B: Magari ya Utalii** | | | |
| | **Utaratibu wa Sasa** | | **Utaratibu Unaopendekezwa** | |
| | ***Idadi ya Watalii*** | ***Kiwango*** | ***Idadi ya Watalii*** | ***Kiwango*** |
| | Haikuwepo | Haikuwepo | Wasiozidi 15 | 650,000 |
| | - | - | 16 hadi 25 | 900,000 |
| | - | - | 26 hadi 45 | 1,300,000 |
| | - | - | 46 hadi 65 | 1,800,000 |
| | - | - | Zaidi ya 65 | 2,400,000 |
| | | | | |
| **C** | **Daraja C: Magari ya Mizigo** | | | |
| | **Viwango vya Sasa** | | **Viwango Vinavyopendekezwa** | |
| | ***Uwezo wa Gari (tani)*** | ***Kiwango*** | ***Uwezo wa Gari (tani)*** | ***Kiwango*** |
| 1 | Chini ya tani 1 | 180,000 | Chini ya tani 1 | 250,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | 1 hadi 5 | 450,000 | 1 hadi 5 | 500,000 |
| 3 | 6 hadi 10 | 720,000 | 6 hadi 10 | 750,000 |
| 4 | 11 hadi 15 | 1,710,000 | 11 hadi 15 | 1,100,000 |
| 5 | 16 hadi 20 | 2,430,000 | 16 hadi 20 | 1,300,000 |
| 6 | 21 hadi 25 | 2,610,000 | 21 hadi 25 | 1,650,000 |
| 7 | 26 hadi 30 | 2,790,000 | 26 hadi 30 | 1,900,000 |
| 8 | Zaidi ya 31 | 2,790,000 | Zaidi ya 31 | 2,200,000 |
| | | | | |
| **D** | **Daraja D: Magari Binafsi ya Kukodisha** | | | |
| | **Viwango vya Sasa** | | **Viwango Vinavyopendekezwa** | |
| | | | | |
| | ***Aina ya Chombo*** | ***Kiwango*** | ***Aina ya Chombo*** | ***Kiwango*** |
| 1 | Pikipiki ya miguu miwili | Haikuwepo | Pikipiki ya miguu miwili | 65,000 |
| 2 | Pikipiki ya miguu mitatu | - | Pikipiki ya miguu mitatu | 120,000 |
| 3 | Teksi | - | Teksi | 180,000 |
| 4 | *Ride Hailling* | - | *Ride Hailling* | 350,000 |
| 5 | *Ride Sharing* | - | *Ride Sharing* | 450,000 |
| 6 | *Special Hire* | - | *Special Hire* | 750,000 |

vii. Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (Artisanal and SmallScale Miners). Hatua hii inalenga kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wachimbaji hao na kutatua changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji kodi katika Sekta hiyo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 44,712.4;**

viii. Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo yatokanayo na uuzaji wa hewa ukaa (Verified

Emmission Reduction). Lengo la hatua hii ni kuleta usawa wa ulipaji kodi na kupanua wigo wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 638.2; na**

ix. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania itasimamia utolewaji wa vyeti vya msamaha wa kodi kwa taasisi za huduma ya jamii kama vile taasisi za dini na kupitia mifumo ya kielektoniki ambapo sasa ndani ya siku 14 vyeti hivyo vitakuwa vinapatikana.

Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 51,960.1**

**(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**133. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124(2), marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa *bidhaa (specific duty rates)* kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla.

**134. Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru (specific duty rates) kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo za petroli, na asilimia 20 ya bei kwenye bidhaa za bia na tumbaku. Lengo la hatua hii ni kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kwa kuwa utozaji wa Ushuru wa Bidhaa kwa kutumia viwango maalum (specific rates) usiporekebishwa hupoteza thamani ya fedha na hivyo kupunguza mapato ya Serikali. Njia bora inayotumika kuondoa mapungufu hayo ni kurekebisha viwango maalum vya ushuru ili kuendana na thamani ya fedha kulingana na mfumuko wa bei. Utaratibu huu hautajumuisha utozaji Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa (advalorem rates) kwa kuwa thamani ya bidhaa inazingatia mfumuko wa bei.

**135. Mheshimiwa Spika**, aidha, marekebisho haya mara ya mwisho yalifanyika katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kwa bidhaa zinazozalishwa ndani na Sheria ya Fedha ya mwaka 2018

kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kutokana na hali ya kiuchumi kutetereka kufuatia mabadiliko ya tabia ya walaji na athari za UVIKO 19. Kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa kukuza uchumi wa viwanda, bidhaa za mvinyo, vinywaji vikali (spirits) na bidhaa za sukari (confectionary) zinazozalishwa nchini hazitafanyiwa marekebisho hayo. Hatua hii kwa ujumla inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kiasi cha shilingi **milioni 299,662.4.**

**136. Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147, kwa kuanzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kila baada ya miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, napendekeza pia kufanya marekebisho kwa bidhaa nyingine kama ifuatavyo:

i. Kusamehe Ushuru wa Bidhaa unaotozwa kwa mujibu wa uwezo wa injini (engine capacity) kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme pekee yanayotambulika kwa *HS Code* 8702.40.11; 8702.40.19; 8703.80.10; na 8703.80.90 pamoja na magari yanayotumia Nishati ya Gesi Asilia (CNG) pekee. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya nishati ya umeme na gesi asilia nchini na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni inayotumika kuagiza nishati ya mafuta kutoka nje ya nchi;

ii. Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kutoka shilingi 4,386 kwa lita hadi shilingi 2,466.45 kwa lita kwenye vinywaji vikali (Ready to Drink) vinavyozalishwa nchini. Vinywaji hivyo vinatambulika kwa *Hs Code* 2208.60.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya viwe shindani. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 779.1;**

iii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 20 kwa kila kilo moja ya Saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi. Uzalishaji wa Saruji unatoa kiasi kikubwa cha hewa ya ukaa inayochafua na kuharibu mazingira. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za fidia ya athari hasi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 147,549.6**;

iv. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye magari yenye uwezo wa injini (Engine Capacity) wa kati ya 1000cc hadi 2000cc yaliyotokana na ukuaji wa teknolojia ili kuwianisha na magari mengine yenye ukubwa unaofanana yanayotozwa ushuru huo. Magari hayo ni yale yanayotambuliwa kwenye *H.S Codes* 8703.40.00, 8703.50.00, 8703.60.00 na 8703.70.00;

v. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye magari yenye uwezo wa injini (Engine Capacity) wa zaidi ya 2000cc yaliyotokana na ukuaji wa teknolojia ili kuwianisha na magari mengine yenye ukubwa unaofanana yanayotozwa ushuru huo. Magari hayo ni yale yanayotambuliwa kwa *H.S Codes* 8702.10.11, 8702.10.19, 8702.20.11, 8702.20.19, 8702.30.11, 8702.30.19, 8702.90.11, 8702.90.19, 8703.40.00, 8703.50.00, 8703.60.00, 8703.70.00, na 8703.90.90;

vi. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye magari ya abiria yanayoingizwa nchini yanayozidi umri wa miaka mitano (magari chakavu) yaliyotokana na ukuaji wa teknolojia ili kuwianisha na magari mengine yanayofanana yanayotozwa ushuru huo. Magari hayo ni yale yanayotambuliwa kwa *H.S Codes* 8702.20.22, 8702.20.29, 8702.20.99, 8702.30.22, 8702.30.29, 8702.30.99, 8702.40.22, 8702.40.29 na 8702.40.99;

vii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye sigara na bidhaa za aina hiyo zinazotumia mbadala wa tumbaku zinazotambulika kwa *Hs code* 2402.90.00; tumbaku inayovutwa kwa kutumia bomba la maji inayotambulika kwa *Hs code* 2403.11.00; na sigara za kielektroniki, shisha na bidhaa za aina hiyo zinazotambulika kwa *Hs codes* 8543.40.10, 8543.40.90 na 9614.00.00. Lengo la hatua hii ni kujumuisha bidhaa mpya zinazotumika kama mbadala wa tumbaku ambazo pia zina athari sawa na tumbaku;

viii. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwenye mashine za Kamari zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa nchini. Mashine hizo zinatambulika kwa *Hs Code* 9504.30.00. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,365.4**;

ix. Kuongeza Ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 589.05 kwa lita hadi shilingi 600 kwa lita kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu (Energy Drink) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Vinywaji hivyo vinatambulika kwa *Hs Code* 2202.99.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuvifanya viwe shindani. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 36.9**; na

x. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ili kuoanisha H.S Codes zilizomo kwenye kitabu cha Viwango vya Pamoja vya Ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Common External Tariff) cha mwaka 2017 na zile zilizomo kwenye kitabu cha mwaka 2022 kama ilivyobainishwa kwenye **Kiambatisho Namba 9**.

Hatua hizi za Ushuru wa Bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 448,989.9**

**(d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

**137**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 kama ifuatavyo: -

i. Kurekebisha kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili tafsiri ya neno *Primary Data Server* lijumuishe seva halisi iliyopo nchini, Seva Mtandao (virtual) au aina yoyote ya kifaa maalum kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za kielektroniki za mlipakodi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za usimikaji wa seva hapa nchini na kuwezesha upatikanaji wa taarifa mara zinapohitajika. Hatua hii itaanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2024; na

ii. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kushusha kiwango cha sasa cha adhabu inayotozwa kwa makosa ya kutotoa risiti au kutotumia mashine za kielektroniki (EFD) kinachoanzia *currency point* 300 (sawa na shilingi 4,500,000) hadi *currency point* 200 (sawa na shilingi

3,000,000) kwenda asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi 3,000,000 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Vilevile, napendekeza kushusha kiwango cha adhabu inayotozwa kwa makosa ya kutodai risiti au kutotoa taarifa ya makosa ya kutotoa risiti cha *currency point* 2 (sawa na shilingi 30,000) hadi *currency point* 100 (sawa na shilingi 1,500,000) kwenda asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi 30,000 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Viwango husika viliwekwa kwa lengo la kuchochea utii wa matakwa ya Sheria za kodi zilizopo. Hata hivyo, imebainika kuwa viwango vikubwa vya adhabu vinachochea mazingira ya rushwa. Sambamba na hatua hizi, napendekeza kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazotoza adhabu ili kushusha viwango hivyo na kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kabla ya kuanza kutumia viwango vipya vya adhabu. Lengo la hatua hii ni kupunguza mianya ya rushwa, kulinda mapato ya Serikali na kuchochea utii wa sheria. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilifanya jaribio la mchezo wa bahati nasibu kwenye Mkoa wa Kikodi wa Tegeta jijini Dar es Salaam kwa kuwajumuisha wananchi waliodai risiti za EFD katika manunuzi ya bidhaa kwenye shindano la bahati nasibu kupitia risiti za hizo. Washindi wa bahati nasibu walipewa zawadi nono. Hatua hii ilisaidia kuongeza uhiari wa wananchi kudai risiti katika manunuzi yao. Aidha, mwaka wa Fedha 2023/24 Serikali inakusudia kufanya mchezo wa kubahatisha kwa nchi nzima ili kuhamasisha wananchi kudai risiti halali za EFD.

**(e) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290.**

**138. Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukuaji wa teknolojia, Dunia inashuhudia mabadiliko makubwa katika tasnia ya matangazo ya kibiashara (Advertisment) ambapo sasa matangazo mengi yamekua yakifanyika kupitia mitandao (online advertisement) hasa mitandao ya kijamii kama vile Instagram, Facebook, twiter na Blogs mbalimbali. Kwa kushirikiana na Sekta binafsi, Serikali inatarajia kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kufuatilia na kuhakikisha kodi husika za Serikali zinalipwa kwa wakati. Hii itajumuisha matangazo ya Biashara ambayo huwekwa na watu maarufu (digital influencers) na biashara za mtandaoni zinazofanyika nchini.

**139. Mheshimiwa Spika**, napendekea kufanya marekebisho kwenye Jedwali la viwango vya tozo chini ya Kanuni za Ada ya Mabango na Matangazo ili kupunguza kiwango cha tozo ya mabango yasiyowaka ya matangazo (non-illuminated) kutoka shilingi kwenye 10,000 hadi shilingi 7,000 na mbango yanayowaka ya matangazo (illuminated) kutoka shilingi 13,000 hadi shilingi 10,000. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwenye matangazo ya biashara. Hatua hii inatarajia **kupunguza** Mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 3,773.8.** Vilevile, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290 kama ifuatavyo:

i. Kufanya maboresho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili jukumu la kukusanya ushuru wa mabango lihame kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa mabango kwa kutumia Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambao muundo wake wa kiutawala umefika hadi ngazi za chini za Kata, Mitaa na vijiji, na hivyo kurahisisha masuala ya ufuatiliaji na usimamizi;

ii. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kwa kuunganisha ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na Tozo ya Ardhi ili ziweze kulipwa kupitia namba ya malipo (control number) moja. Mapato hayo yataingiizwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kubainisha kiasi cha fedha kilichokusanywa kutoka kwenye kila chanzo. Aidha, sheria ibainishe kuwa asilimia 20 ya mapato hayo yatarejeshwa Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi hizo. Wizara ya Ardhi na Ofisi ya Rais- TAMISEMI zitaingia Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) wa usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi. Lengo la hatua hizi ni kuondoa kero kwa walipa kodi na kuongeza tija katika ukusanyaji wa kodi hizo;

iii. Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 9A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kuipa Ofisi ya Rais TAMISEMI jukumu la kukusanya ushuru wa huduma (asilimia 0.3 ya mauzo ghafi) kwenye leseni za Huduma za Fedha Mtandaoni (Electronic Money Issuance License – EMI na kuzigawanya kwa halmashauri

husika. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za usimamizi na ulipaji kodi kwa Kampuni za Simu na Halmashauri husika.

**(f) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289**

**140**. **Mheshimiwa Spika**, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289 kama ifuatavyo:

i. Kurekebisha Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289 kwa kuongeza maeneo yote ya Wilaya isipokuwa majengo yaliyosamehewa kupitia Kifungu cha 7 cha sheria hii. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika kulipa kodi; na

ii. Kuainisha zoezi la uthaminishaji wa majengo lianze mwaka wa fedha 2023/24 ili kodi itozwe kwa kuzingatia thamani halisi ya jengo ifikapo mwaka 2026. Zoezi la uthaminishaji na ukusanyaji wa kodi ya majengo litasimamiwa na Ofisi ya RaisTAMISEMI na ukusanyaji utafanyika kwa kupitia namba ya malipo (control number) kuanzia mwezi Januari, 2024. Aidha, katika kipindi cha mpito, utaratibu wa kutumia LUKU kukusanya kodi husika utaendelea kutumika. Lengo la hatua hii ni kutoa nafasi kwa Serikali kuanza maandalizi ya uthaminishaji na kuondoa jukumu hilo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambalo jukumu lake la msingi ni kuzalisha na kusambaza nishati ya umeme nchini.

**(g) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**

**141**. **Mheshimiwa Spika**, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220 kwa kuongeza Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kiasi cha shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya Petroli na Dizeli. Aidha, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 4A cha Sheria ya Ushuru wa Barabara SURA, 220 kwa kuongeza kipengele ‘c’ kitakachoelekeza fedha zitakazokusanywa kutokana na ongezeko hili la ushuru wa barabara na mafuta la shilingi 100 kwa mafuta ya petroli na dizeli zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ili kupata vyanzo vya uhakika

kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** Mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 381,826.8**

**(h) Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, SURA 437 na Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306**

**142**. **Mheshimiwa Spika**, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kufanya miamala. Hatua hizo ni pamoja na usasishaji wa Mifumo ya Malipo ya Taifa (upgrading), ikiwemo kukamilika na kuanza kutumika kwa Mfumo wa Malipo wa papo kwa papo (Tanzania Instant Payment System – TIPS), na usimamizi thabiti wa mifumo ya malipo nchini. Uboreshaji wa miundombinu hii ni hatua muhimu ya kufikia malengo ya ujumuishwaji wa wananchi wengi kwenye mfumo rasmi wa fedha na pia kwa nchi yetu kuelekea kwenye uchumi wa kidijitali. Kwa kuzingatia hayo, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, 2015 kama ifuatavyo: -

i. Kufuta tozo kwa siku kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji ili kuchochea matumizi ya kielektroniki katika miamala mbalimbali.

**(i) Sheria ya Uhamiaji, SURA 54**

143. **Mheshimiwa Spika**, Kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji SURA 54 kwa kutoa hati ya ukaazi (Residence Permit Class B) kwa mwekezaji yeyote asiye mkaazi hapa nchini na atakayewekeza kununua nyumba kwa mtaji usiopungua dola za Kimarekani 150,000. Aidha, Kibali cha Ukaazi kitatolewa baada ya mamlaka yenye dhamana ya uwekezaji kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya nyumba na kujiridhisha kuwa mtaji husika umetoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika sekta ya nyumba nchini na kuongeza fedha za kigeni.

**(j) Sheria ya Ardhi, SURA 113**

**144**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, SURA 113 kama ifuatavyo:

i. Kupunguza tozo ya Malipo ya mbele (Premium) kutoka asilimia 0.5 ya thamani ya ardhi hadi asilimia 0.25;

ii. Kupunguza ada ya hati miliki kutoka shilingi 50,000 kwa hati hadi shilingi 25,000 kwa hati;

iii. Kupunguza ada ya usajili wa hati kutoka asilimia 20 hadi asilimia 10;

iv. Kupunguza ada ya maombi ya hati kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 5,000;

v. Kufuta ada ya mpango wa upimaji (Deed Plan) ambayo ilikua inatozwa shilingi 20,000; na

vi. Kurekebisha Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili Mkurugenzi wa Halmashauri akasimiwe jukumu la kukusanya Kodi ya Pango la Ardhi kwa niaba ya Wizara ya Ardhi. Aidha, asilimia 20 ya mapato hayo yatarejeshwa Halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi hizo.

Lengo la hatua hizi ni kupunguza gharama za upangaji, urasimishaji na umilikishaji wa ardhi nchini ili kuhamasisha eneo kubwa zaidi la nchi kupangwa, kurasimishwa na kumilikishwa kwa wananchi. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 115,500.**

**(k) Sheria ya Madini, SURA 123**

**145**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 90A (3) cha Sheria ya Madini, SURA 123 ili kutoa msamaha kwa vituo vya kusafishia madini (refineries) wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia 1. Lengo la hatua hii ni kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya usafishaji madini

nchini na kuvutia uwekezaji zaidi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.

**(l) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82**

**146**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82 kama ifuatavyo:

i. Kupunguza kiwango cha tozo ya Ufundi Stadi kutoka asilimia 4 hadi asilimia 3.5. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia waajiri gharama za uendeshaji wa shughuli zao na kutimiza azma ya kupunguza tozo hizi hatua kwa hatua bila kuathiri mapato ya serikali kwa kiasi kikubwa. Hatua hii **itapunguza** Mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 58,889.7;**

ii. Kufanya maboresho ya Sheria ya Kuendeleza Ujuzi ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na Elimu kutoa Hati ya msamaha wa tozo ya ufundi stadi baada ya kujiridhisha kuwa msamaha husika ni kwa maslahi ya Taifa;

iii. Kurekebisha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82, ili mgao wa mapato yatokanayo na tozo ya Ufundi Stadi uwe kama ifuatavyo: - theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa katika Wizara yenye dhamana ya Ajira; theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, na theluthi moja (1/3) ya mapato itapelekwa VETA. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa mipango ya mafunzo ya stadi za kazi yakiwemo mafunzo ya Uanagenzi na Tarakinishi.

**(m) Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84**

**147**. **Mheshimiwa Spika**, Napendekeza kuendelea na utaratibu wa kutoza magari ya kigeni yaliyosajiliwa nje ya Tanzania viwango sawa na vile vinavyotozwa katika ukanda wa EAC, SADC na COMESA. Aidha, endapo itabainika kuwa kuna nchi inatoza viwango vya juu ikilinganishwa na vile vya ukanda wa EAC, SADC na COMESA, viwango hivyo vitatumika katika kutoza magari

yaliyosajiliwa katika nchi husika. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa na kulinda maslahi ya nchi.

**(n) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41**

**148. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kama ifuatavyo:

i. Kuanzisha michezo ya meza isiyozidi miwili (2) katika maeneo yenye Mashine za Sloti Arobaini (Forty Machine Site). Lengo la hatua hii ni kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha kutoka kwenye uendeshaji wa Mashine Arobaini za Sloti. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 4,223** kwa mwaka wa Fedha 2023/24;

ii. Kuongeza tozo ya michezo ya kubahatisha kutoka shilingi 10,000 hadi Shilingi 30,000 kwa kila mashine ya Sloti kwenye maeneo ya baa (sehemu za kuuzia pombe). Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 4,738** mwaka 2023/24;

iii. Kuanzisha ada ya maombi ya shilingi 500,000 na ada ya leseni Kuu ya dola za Kimarekani 10,000 kwa mwaka kwenye mashine za Sloti kwenye maduka; ada ya maombi ya shilingi 500,000 na ada ya leseni Kuu ya dola za Kimarekani 10,000 kwa mwaka kwenye mashine za Sloti katika maeneo ya baa; (sehemu za kuuzia pombe); ada ya maombi ya shilingi 500,000 na ada ya leseni Kuu dola za Kimarekani 5,000 kwa mwaka kwenye mashine Arobaini za Sloti. Lengo la hatua hii ni kuweka utofauti kati ya shughuli za mashine za Sloti katika maeneo ya baa (sehemu za kuuza pombe), maduka na shughuli za mashine arobaini za sloti pamoja na kuwezesha ufanisi na udhibiti bora wa michezo ya kubahatisha; na

iv. Kupunguza kiwango cha kodi kutoka asilimia 25 hadi asilimia 18 kwenye mapato ghafi ya michezo ya kubahatisha kwenye maeneo ya uendeshaji wa Mashine Arobaini za Sloti. Lengo la hatua hii ni kuleta usawa katika utozaji kodi katika michezo ya kubahatisha inayoshabiana.

**149. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaufufua Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) uliopo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kuweka utaratibu wa kuuwekea fedha ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ardhi nchini ikiwemo kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Mfuko huu utasaidia kuongeza wananchi wenye milki salama, kudhibiti makazi holela, kupunguza migogoro ya ardhi, kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza wigo wa mapato.

**(o) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

150. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi kwa kusamehe tozo ya asilimia 80 kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa na wawekezaji waliopo kwenye Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji nchini (EPZ) kwenda nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uwekezaji ambapo kwa sasa gharama kubwa zinatumika katika kuharibu ngozi hizo kutokana na ukosefu wa soko hapa nchini.

**(p) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**151. Mheshimiwa Spika**, Napenda kukufahamisha kwamba, kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (EAC Pre-Budget Consultative Meeting of Ministers of Finance) kilichofanyika tarehe 12 Mei 2023 jijini Arusha, kilipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 pamoja na Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC-Common External Tariff) kwa mwaka wa Fedha 2023/24. Mapendekezo hayo yanalenga kuongeza kasi ya kufufua uchumi, kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha Sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi.

**152. Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo

zimekuwa zikitekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

i. Mapendekezo ya hatua mpya za Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo: -

a. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye karatasi za kutolea risiti za kielektroniki zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 kwa mwaka mmoja. Aidha, wazalishaji wanaotumia bidhaa hii kama malighafi watapata unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii pamoja na kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hii;

b. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 50 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vitenge vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.51.10; 5208.52.10; 5209.51.10; 5210.51.10; 5211.51.10; 5212.15.10; 5212.25.10; 5513.41.10; na 5514.41.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye uagizaji wa vitenge ili kulinda walaji. Sambamba na hatua hii, uthaminishaji wa bidhaa hizi utakuwa dola za Kimarekani 0.4 kwa vitenge vya pamba na dola za Kimarekani 0.36 kwa vitenge vya polyester;

c. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 0.25 kwa kila mita moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja kwenye vitambaa vya pamba (cotton grey fabric) vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.11.00; 5208.12.00; 5208.13.00; 5208.19.00; 5209.11.00; 5209.12.00; 5209.19.00; 5210.11.00; 5210.19.00; 5211.11.00; 5211.12.00; 5211.19.00; 5212.11.00; na 5212.21.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uzalishaji wa vitambaa hivyo kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini pamoja na kuongeza ajira;

d. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye kadi janja (smart cards) zinazotambulika kwa HS Code 8523.52.00 zitakazoingizwa nchini

na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa kadi hizo ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi;

e. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye kamba zinazotengenezwa kwa nyuzi zenye asili ya plastiki (Twine of other synthetic fibers) zinazotambulika kwa HS Code 5607.50.00 kwa mwaka mmoja. Lengo ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa mbadala hapa nchini pamoja na kuongeza ajira;

f. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 2.0 kwa kila mita moja ya mraba (square meter) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye marumaru zinazotambulika kwa HS Codes 6907.21.00; 6907.22.00; na 6907.23.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha marumaru, pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

g. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye misumari zinazotambulika kwa HS code 7317.00.00 *(nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, and staples other than those of heading* 83.05). Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo nchini pamoja na kuongeza ajira;

h. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kutoka asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuzalisha bidhaa mtaji (capital goods) zinazotumika viwandani zinazotambulika kwa *headings* 72.14; 72.15; 72.16; 32.08; 73.07; 83.11; 85.44; 68.06; 74.19; 72.08; 73.06; 73.12; 73.15; 73.18; 84.82; 84.83; 72.22; 73.04; 84.81; 84.84; 7325; 40.10; na 76.06. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji wa bidhaa mtaji hapa nchini ili bidhaa hizo ziweze kupatikana kwa unafuu kwa viwanda vya ndani pamoja na kuchochea uwekezaji wa kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini;

i. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye malighafi za kutengeneza bidhaa za waya za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7213.91.10; na 7213.91.90. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji wa bidhaa za waya za chuma ndani ya Jumuiya pamoja na kuongeza ajira;

j. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi aina ya *base oil* inayotambulika kwa HS Code 2710.19.59 inayotumika kutengeneza vilainishi (lubricants). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vilainishi ndani ya Jumuiya;

k. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza *wiring harnesses* za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 8538.90.00; 4016.99.00; 8205.59.00; 8536.10.00; 8536.69.00; 8536.90.00; 8547.20.00; 3926.90.90; 3917.32.00; na 8544.30.00. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hizo nchini;

l. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza rejeta (radiators) za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 7409.11.00; 7409.19.00; 7410.11.00; 7410.12.00; 7409.21.00; 8001.10.00; 3810.90.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hiyo hapa nchini;

m. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwenye viatu, nafaka na mbogamboga kama vile matango na Macadamia,

Wanyama hai kama vile mbuzi, ng'ombe na kondoo, majeneza, samaki, mihogo na asali zinazotambulika kwa HS Codes 4421.20.00; 6402.19.00; 6403.19.00; 6403.51.00; 6404.19.00; 6404.20.00; 6405.20.00; 6405.90.00; 0802.11.00; 0802.22.00; 0802.61.00; 2001.10.00; 0102.29.00; 0102.39.00; 0102.90.90; 0103.91.00; 0103.92.00; 0104.10.90; 0104.20.90; 0407.21.00; 0409.00.00; 0714.10.00 na Chapter 3. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa bidhaa hizo kwa kuwa zinapatikana kwa wingi ndani ya Jumuiya;

n. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa HS Codes 8702.10.99 na 8702.20.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi;

o. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya kiwango cha asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayotambulika kwa HS Code 1701.14.90 inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap) la uzalishaji hapa nchini;

p. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kufanya marekebisho kwenye Kipengele cha 27 cha sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutanua wigo wa msamaha kwenye ''*Biogas Digesters*'' zinazotengenezwa na malighafi nyingine mbali na plastiki;

q. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kubadilisha muundo wa *Heading* 17.01 kwa kuongeza *subheading* 1701.99.20 ili kukidhi hitaji la kuwa na bidhaa inayojitegemea ambayo ni sukari isiyokuwa nyeupe kwa ajili ya matumizi ya viwandani.

r. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kubadilisha muundo wa *Heading* 76.12 ili

kuoanisha na muundo wa *Heading* 73.10 kwa kuongeza *subheading* 7612.90.10 itakayotozwa ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25. Lengo ni kutoa unafuu kwenye mikebe ya kuhifadhia viuatilifu (Aerosol cans) vinavyotengenezwa kwa *base metal*.

s. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 0 au asilimia 10 kwenye waya za chuma zinazotambulika kwa *Heading* 72.17. Aidha, wazalishaji wanaotumia bidhaa hii kama malighafi watapata unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 au asilimia 10 badala ya asilimia 25 kulingana na aina ya bidhaa wanayozalisha. Lengo la hatua hii ni kuwianisha na viwango vya ushuru wa forodha vinavyotozwa kwenye *Heading* 72.13 pamoja na kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwenye viwanda vinavyotumia
malighafi hii;

t. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kugawanya (split) HS Code 8703.80.00 ili kuwezesha waunganishaji (assemblers) wa magari anayotumia nishati ya umeme nchini kuingiza magari ambayo hayajaunganishwa (unassembled) kwa ushuru wa forodha wa asilimia 0. Hatua hii inalenga kutoa unafuu ili kuhamasisha uwekezaji katika uunganishaji wa magari hayo nchini;

ii. Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

a. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwenye malighafi zinazotumika kuzalisha vifaa maalum vinavyotumika katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu (UVIKO-19) vikiwemo Barakoa (Masks), kipukusi (sanitizer), mashine za kusaidia kupumua (ventilators), na mavazi maalum ya kujikinga yanayotumiwa na madaktari na wahudumu wa afya (PPE). Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji

wa vifaa hivyo ndani ya Jumuiya ili kuongeza kasi katika kupambana na ugonjwa huo;

b. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali *(Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS)* machines) zinazotambulika kwa HS Codes 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika kuhasibu mapato ya Serikali;

c. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (UHT Milk) vinavyotambulika kwa HS code 4819.50.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini;

d. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye vifuniko vya chupa za mvinyo (corks and stoppers) vinavyotambulika kwa HS Code 4503.10.00. Hatua hii inalenga kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mvinyo ili kuhamasisha na kuendeleza kilimo cha zao la zabibu nchini pamoja na kuongeza ajira;

e. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa HS Code 1805.00.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha kilimo cha zao la kakao nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

f. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotambulika kwa HS codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90 na 3920.30.90 vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Hatua hii inalenga kuongeza thamani

kwenye zao la kahawa na kutoa unafuu wa gharama kwenye viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini;

g. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho vinavyotambulika kwa HS code 3923.21.00. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwenye zao la korosho na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyochakata korosho hapa nchini;

h. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba (cotton lint) vinavyotambulika kwa HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00. Hatua hii inalenga kuvutia uwekezaji ili kuongeza thamani ya zao la pamba nchini;

i. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwenye malighafi za kutengeneza taulo za watoto (Baby Diapers) zinazotumbulika kwa HS code 3506.91.00 Hot Melt Adhesive; PE film HS Code 3920.10.90, Empty bag for Baby Diapers HS Code 6305.33.00, Plastic cask HS Code 3926.90.90; Super Absorbent Polymer HS Code 3906.90.00, Wet strength paper HS Code 4803.00.00, Non-woven HS Code 5603.11.00, Polyethylene laminated Nonwovens HS Code 5903.90.00, Spandex HS Code 5402.44.00 na Dust free paper HS Code 4803.00.00. Hatua hii inalenga kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji na kuongeza ajira;

j. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika kwa HS codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90 na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini;

k. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kwenye bidhaa za chuma kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya

ushuru wa asilimia 10 pekee kwa mwaka mmoja. Bidhaa hizo ni "*Flat -rolled products of iron or Non-alloy steel and other alloy steel*." Bidhaa hizi zinatambulika kwa HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hizo pamoja na kukuza ajira;

l. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS codes 7210.30.00; 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00; 7210.90.00; na 7212.30.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

m. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS Code 7212.60.00 badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

n. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma *(Iron and Steel reinforment bars and hallow profile)* kwa mwaka mmoja. Hatua hii inahusu bidhaa zinazotambulika kwa HS Codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00;7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

o. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango

cha asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma *(Flat-rolled products of other alloy steel, of a width of 600 mm or more)* zinazotambulika kwa HS Codes 7225.91.00; 7225.92.00; na 7225.99.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali,

p. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* zinazotambulika kwa HS Codes 3916.10.00; 3916.20.00; na 3916.90.00 zinazotumika kutengenezea fremu za milango, adirisha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

q. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS code 4804.29.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

r. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa HS Codes 1001.99.10 na 1001.99.90. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa Viwanda vinavyozalisha unga wa ngano;

s. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ijulikanayo kama "Printed Alluminium Barrier Laminates" (ABL) inayotambulika kwa HS Code 3920.10.90 ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio vya dawa ya meno. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama kwa viwanda vinavyozalisha dawa ya meno nchini;

t. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD Palm Stearin* zinazotambulika kwa HS Code 1511.90.40 kwa viwanda vinavyotengeneza sabuni nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vya kuzalisha sabuni nchini;

u. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja ya viberiti *(safety match boxes)* vinavyotambuliwa kwenye HS code 3605.00.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

v. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa *(mineral water)* yanayotambulika kwa HS code 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavozalisha maji ya kunywa nchini;

w. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *Gypsum Powder* inayotambulika kwa HS code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa *Gypsum Powder* nchini;

x. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 35 au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayotambulika kwa HS Codes 6309.00.10; 6309.00.20; na 6309.00.90 inayoingia kutoka nje. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa watumiaji wa bidhaa hii hapa nchini;

y. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na viatu vya ngozi nchini;

z. Kutoza ushuru wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha;

aa. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mikebe ya kubebea maziwa (milk cans) inayotambulika kwa HS Codes 7310.10.00 na

7310.29.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa vifungashio vya kuhifadhia maziwa ili kuwalinda walaji nchini;

bb. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (Organic surface-active agents) zinazotambulika kwa HS Codes 3402.31.00; 3402.39.00; 3402.49.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na maji nchini;

cc. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Codes 3208.20.10; 3208.20.20; 3208.90.20 na 3210.00.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

dd. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 mwaka mmoja kwenye malighafi za utengeneza mbolea zinazotambulika kwa HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00 na 3505.20.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea nchini;

ee. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Code 5310.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa tumbaku nchini;

ff. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90, 5407.44.00 na 3923.29.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini;

gg. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu

bila kujumuisha fremu ili ziweze kutengenezwa na kuunganishwa hapa nchini (CKD for three-wheel motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo;

hh. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mabomba ya plastiki (glass reinforced plastic pipes) zinazotambulika kwa HS Codes 3920.61.10, 7019.39.00, 7019.31.00, 6006.90.00, 7019.12.00, 3920.10.10, 4016.93.00, na 3907.91.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji;

ii. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo (metric tone) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye sukari ya matumizi ya viwandani (sugar for industrial use) inayotambulika kwa HS Codes 1701.99.10 na 1701.99.20. Lengo la hatua hii ni kuwezesha na kutoa unafuu kwenye viwanda vinavyotumia bidhaa hii kama malighafi;

jj. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma na mabati zinazotambulika kwa HS Code 7212.20.00; na 7226.99.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

kk. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto *(Baby* Diapers) zinazotumbulika kwa HS code 9619.00.90. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

ll. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn) zinazotambulika kwa *Headings* 52.05, 52.06 na 52.07 isipokuwa nyuzi za pamba zinazotambulika kwa HS Code 5205.23.00. Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba (value addition) nchini;

mm. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa za mbogamboga na matunda zinazotambulika kwa HS code 0604.20.00; 0604.90.00; 0808.10.00; 0808.30.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kilinda wazalishaji wa bidhaa za mbogamboga na matunda hapa nchini;

nn. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza viongeza ladha kwenye vyakula na vinywaji (food flavors) zinazotambulika kwa HS Code 1901.90.10; 3302.10.00; na 3505.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa bidhaa hizo nchini;

oo. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Codes 4804.39.00; 4805.11.00; 4805.19.00; 4805.24.00; 4805.25.00; zinazotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (corrugated boxes). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa bei nafuu;

pp. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza vioo vizito (toughened glass) zinazotambulika kwa HS Codes 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; na 7005.30.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vioo hivyo nchini;

qq. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 35 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja

kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (toilet soap) zinazotambulika kwa HS Code 3401.20.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini, kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

rr. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (electrical cables) zinazotambulika kwa HS Codes 7312.10.00; 7217.20.00; 7408.19.00; 7409.11.00; 7605.21.00; 2710.19.56; 3815.90.00; 5402.19.00; 5903.90.00; 7217.20.00; 7907.00.00; 7312.10.00; na 2712.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji nchini;

ss. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja badala ya asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi, mnyonyo, mahindi n.k yanayotambulika kwa HS codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1513.11.00; 1513.21.00; 1514.11.00; 1514.91.00; na 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni kuoanisha viwango vya mafuta haya ghafi vifanane na viwango vya mafuta ghafi ya alizeti, pamba na mafuta ghafi mengineyo ambayo viwango vyake ni asilimia 10. Aidha, hatua hii pia inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

tt. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (refined) yanayotambulika kwa HS codes 1507.90.00; 1508.90.00; 1509; 1510.10.00; 510.90.00; 90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 1514.19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 1515.29.00; 1515.50.00; na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda na kuhamasisha uchakataji wa mbegu na mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini ili kuongeza thamani ya bidhaa (value addition), kukuza ajira, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,258.3**

**(q) Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint)**

**153**. **Mheshimiwa Spika**, Napendekeza kufanya maboresho ya kurekebisha, kuanzisha, kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuleta usimamizi bora wa sekta mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara nchini. Hatua hizi pia ni moja ya sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment). Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

i. **Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara.**

Kufuta adhabu ya asilimia 15 ya thamani ya bidhaa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania kwa bidhaa zinazoingia nchini bila ya kuwa na cheti cha uthibitisho wa ukaguzi wa ubora (Certificate of Conformity - COC). Aidha, bidhaa hizo zisizo na Cheti cha uthibitisho wa ubora zitafanyiwa ukaguzi wa ubora zinapofika nchini na kulipiwa gharama za ukaguzi pekee.

ii. **Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**

Kufanya marekebisho kwenye tozo za uwekaji wa miundombinu kwenye hifadhi ya barabara (Right of Way) kwa kupunguza ada ya awali (initial fee) za usimikaji wa nyaya za mawasiliano kutoka dola za Kimarekani 1,000 kwa Kilomita hadi dola za Kimarekani 200 kwa kilomita; na ada ya mwaka (annual fee) kwa kutoka dola za Kimarekani 1,000 kwa kilomita hadi dola za Kimarekani 100 kwa kilomita. Lengo la hatua hii ni kufanikisha malengo ya kusambaza miundombinu ya mawasiliano kutoka Mkoani kwenda Wilayani na kutoka Wilayani kwenda kwa wateja na hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora;

iii. **Wizara ya Mambo ya Ndani**

Kufanya marekebisho ya ada na tozo mbalimbali kama ifuatavyo:

a. Kuongeza tozo ya hati ya tabia njema kwa Wageni kutoka dola za kimarekani 25 hadi dola za kimarekani 50;

b. Kuongeza tozo ya hati ya tabia njema kwa Wakazi kutoka Sh. 2,000 hadi Sh.10,000;

c. Kuongeza tozo ya gharama ya uchunguzi wa hati zinazobishaniwa kutoka Sh. 50,000 hadi Sh. 75,000;

d. Kuongeza tozo ya ada ya upotevu wa mali kutoka Shilingi 500.00 hadi Shilingi 1,000.00;

e. Kutoza ada ya Shilingi 10,000.00 ya uchunguzi wa leseni za udereva kwa madereva kutoka nchi za kigeni wanaokuja kufanya kazi hapa nchini/walioajiriwa na makampuni yaliyopo nchini. Lengo ni kujua uhalali wao katika umiliki wa leseni hizo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

f. Kuongeza ada ya kibali cha kuhifadhi silaha katika maghala binafsi kutoka Shilingi. 1,000,000 hadi Shilingi 1,500,000 kwa mwaka;

g. Kuongeza ada ya usajili wa mkufunzi mpya wa shule ya udereva kutoka Shilingi 10,000.00 hadi Shilingi 20,000.00; na

h. Kuongeza ada ya kuhuisha umiliki wa silaha za moto za kiraia kama ifuatavyo;-(i) Bastola (Pistol) kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 100,000; (ii) Bunduki (Shotgun) kutoka Shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000 (iii) Gobole (Muzzle loading gun) kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000; (iv) Bunduki (Rifle) kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000 na (v) na silaha nyingine za moto kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000.

Viwango vilivyopo sasa havijahuishwa kwa mda yaani miaka 8 hadi 20, hivyo vimepitwa na wakati.

iv. **Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kufanya marekebisho ya ada na tozo mbalimbali kwenye sekta ya utalii kama ifuatavyo:

a. Kufuta ada ya kupanga na kurudia kupanga (grading and regrading) huduma za malazi zilizo nje na ndani ya maeneo ya hifadhi;

b. Kupunguza viwango vya Ada ya leseni ya biashara ya utalii katika huduma za malazi zinazomilikiwa na Watanzania kutoka dola za kimarekani 2,500 hadi dola za kimarekani 1,500 kwa hoteli za nyota tano; dola za kimarekani 2,000 hadi dola za kimarekani 1,000 kwa hotel za nyota nne; dola za kimarekani 1,500 hadi dola za kimarekani 500 kwa hotel za nyota tatu; dola za kimarekani 1,300 hadi dola za kimarekani 300 kwa hoteli za nyota mbili; na kutoka dola za kimarekani 1,000 hadi dola za kimarekani 200 kwa hoteli za nyota 1; na

c. Kupunguza Ada ya Leseni ya Utalii kwa huduma za malazi ambazo hazijakaguliwa na kupangwa katika viwango vya ubora (ungraded accommodation) nje ya maeneo ya hifadhi kutoka dola za kimarekani 1000 hadi dola za kimarekani 300; huduma ya malazi zinazopatikana katika makazi ya mtoa huduma (homestay) kutoka dola za Kimarekani 400 had dola za kimarekani 100; na hosteli kutoka dola za kimarekani 400 hadi dola za kimarekani 200.

Hatua hizi kwa pamoja zinalenga kupunguza gharama za uendeshaji na kuvutia uwekezaji kwenye Sekta ya Utalii.

v. **Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

a. **Sekta ya Mifugo**

Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Mifugo kama ilivyoanishwa kwenye **Kiambatisho Namba 10**;

b. **Sekta ya Uvuvi**

Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Uvuvi kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 2**;

**Jedwali Na. 2: Maboresho ya kanuni za uvuvi kwa ada za leseni, ushuru wa kusafirisha nje ya nchi na kuingiza nchini mazao ya uvuvi kwa mwaka 2023/2024**

| Na | Aina ya ada ya leseni/ushuru wa kuuza nje na kuingiza nchini mazao ya uvuvi | Viwango vinavyotozwa Sasa | Viwango vinavyopendekezwa Kutozwa. |
|---|---|---|---|
| 1. | Leseni ya ukusanyaji wa samaki wa mapambo | Dola za Kimarekani 12.60 | Dola za Kimarekani 100 |
| | | Dola za Kimarekani 18.96 | |
| | | Raia wa Kigeni hawaruhusiwi | Raia wa Kigeni hawaruhusiwi |
| 2. | Leseni ya kuuza nje ya nchi samaki aliyetolewa matumbo | | Hairuhusiwi |
| 3. | Ushuru/Mrahaba wa kuuza nje ya nchi samaki wa mapambo | 5% ya thamani ya soko | Dola za Kimarekani 0.65 kwa kila samaki |
| 4. | Ushuru wa kuingiza mabondo mabichi, yaliyokaushwa, na yaliyogandishwa | Dola za Kimarekani 2.5 kwa kilo | Kuondoa gharama ya tozo yakuingiza mabondo nchini |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Mwani | | Dola za Kimarekani 500 | | Dola za Kimarekani 300 kwa wafanyabiashara wadogo | |
| | | | Dola za Kimarekani 600 | | Dola za Kimarekani 400 kwa wafanyabiashara wakubwa | |
| | | | Dola za Kimarekani 1000 | | Dola za Kimarekani 800 kwa Kampuni ya Kigeni | |
| 6 | Kibali cha kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi (dagaa, furu) samaki wakavu, wabichi na waliogandi-shwa | Samaki na mazao ya uvuvi yaliyokaushwa | Kilo 0 – 500 | Bure | Kilo 0-20 | Bure |
| | | | Kilo 501 na zaidi | Shilingi 10 kwa kila kilo moja | Kilo 21 na zaidi | Shilingi 100 kwa kila kilo |
| | | | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 100 kwa kila kilo | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 200 kwa kila kilo |
| | | Samaki na mazao ya uvuvi mabichi na yaliyogandishwa | Kilo 0 – 1,000 | Bure | Chini ya kilo 30 | Bure |
| | | | Kilo 1,001 na zaidi | Shilingi 10 kwa kila kilo | Kilo 31 na zaidi | Shilingi 100 kwa kila kilo |
| | | | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 200 kwa kila kilo | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 200 kwa kila kilo |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Pweza, | Kilo 0 – | Bure | Chini ya | Bure |
| **Na** | **Aina ya ada ya leseni/ushuru wa kuuza nje na kuingiza nchini mazao ya uvuvi** | | **Viwango vinavyotozwa Sasa** | | **Viwango vinavyopendekezwa Kutozwa.** | |
| | | Ngizi na Kamba miti wabichi au waliogandishwa | 1,000 | | kilo 30 | |
| | | | Kilo 1,001 na zaidi | Shilingi 10 kwa kila kilo | Zaidi ya kilo 31 | Shilingi 100 kwa kila kilo |
| | | | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 200 kwa kila kilo | Uzito uliozidi na haujatolewa taarifa | Shilingi 200 kwa kila kilo |
| 7 | Kibali cha kusafirisha mazao ya mabondo mabichi na makavu | Mabo ndo mabichi | | | | Shilingi 2,500 kwa kilo |
| | | Mabondo Makavu | | | | Shilingi 3,500 kwa kilo |

vi. **Wizara ya Kilimo**

Kuanzisha ada kwa ajili ya kufanya tafiti za kilimo kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na.3**.

**Jedwali Na. 3: Maboresho ya Kanuni za Tafiti za Kilimo mwaka 2023/2024**

| Na. | Aina ya Adaya Leseni | Awamu za Malipo | Ada ya Watafiti wa Ndani (TZS) | Ada ya Watafiti wa Nje (USD) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya usajili wa mtoa huduma ya utafiti wa kilimo | Mara moja | 20,000 | 100 |
| 2. | Usajili wa mtoa huduma ya utafiti wa kilimo | Mara moja | 300,000 | 300 |
| 3. | Ada ya kuhuisha matumizi ya cheti cha mtoa huduma | Kila baada ya miaka mitatu | 100,000 | 150 |
| 4. | Ada ya maombi ya usajili wa mradi wa utafiti | Mara moja | 20,000 | 100 |
| 5. | Usajili wa mradi wa utafiti wa kilimo | Kwa mradi | 2% ya bajeti ya mradi | 2% ya bajeti ya mradi |
| 6. | Ada ya nyongeza ya muda wa mradi wa utafiti | Kwa mradi | 20,000 | 100 |
| 7. | Upatikanaji wa taarifa | Mara moja | 500,000 | 1000 |

Aidha, napendekeza kuanzisha utaratibu wa kutoa vibali vya uagizaji wa mafuta ghafi ya kula (Crude oil na Semi refined) baada ya kupata uthibitisho wa uzalishaji na uchakataji wa bidhaa bakaa (by-products). Waziri mwenye dhamana ya Kilimo, Fedha na Viwanda wataweka utaratibu wa kupata vibali hivyo.

vii. **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo** Kufanya maboresho kwa kuanza kutoza tozo ya asilimia 1.5 kwenye vinyl, Mini Disc, Compact Disc, DVD na SD Memory. Hivi ni moja vifaa

vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kudurufu na kutunza kazi za Sanaa, uandishi na ubunifu mwingine kama vile muziki, filamu, vitabu, picha na aina nyingine za kazi za ubunifu.

viii. **Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)**
Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya usajili, ufilisi na udhamini kama ilivyoanishwa kwenye
**Kiambatisho Namba 11**;

ix. **Wakala wa Mbolea Tanzania (TFRA)** Kuanzisha ada za Maabara katika uchambuzi wa mbolea kama ilivyoanishwa kwenye **Kiambatisho Namba 12**; na

x. **Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**
Kufuta ada ya ukaguzi ya shilingi 200,000 ya Ufungaji wa Gesi kwa kila kituo. Lengo la hatua hii ni kuchochea mazingira wezeshi ya biashara nchini hususan katika maeneo ya vituo vya gesi.

**154**. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na maboresho ya sheria mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi mbalimbali za udhibiti nchini na kufuta/kupunguza ada na tozo kero, bado kumekuwa na changamoto ya taasisi nyingi za udhibiti zinazosimamia sekta mbalimbali kuongeza kero za ufanyaji biashara na uwekezaji kutokana na ada, tozo na adhabu mbalimbali wanazotoza, kaguzi nyingi na zisizokuwa na tija. Ili kuondoa kero hizo, Serikali inakusudia kuanzisha mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (Single Window Payment System) na kuweka utaratibu kwa taasisi hizo kufanya kaguzi kwa namna ambayo haileti usumbufu na bila kuathiri majukumu ya msingi yanayofanywa na taasisi husika.

**(r) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.**

**155**. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo

yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2023** na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)*.

**(s) Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi.**

**156**. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2023, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

**VII. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2023/24**

**157. Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 44.39 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 31.38, sawa na asilimia 70.7 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 26.73 na mapato yasiyo ya kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 4.66.

**158. Mheshimiwa Spika**, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 5.47. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 5.44 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 3.54 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi trilioni 1.90 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 2.10 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwakawa fedha 2023/24, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 44.39 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 30.31 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha: shilingi trilioni 12.77 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu; shilingi trilioni 10.88 kwa ajili ya mishahara ikiwemo nyongeza ya mshahara, upandishaji wa madaraja na ajira mpya; na shilingi trilioni 1.14 ni ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya kugharamia elimumsingi na sekondari bila ada pamoja na

mikopo ya wanafunzi elimu ya juu; shilingi trilioni 5.52 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 14.08. Kiasi hicho kinajumuisha gharama za utekelezaji wa miradi mbalimbali katika ngazi ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**160. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza hapo awali, sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.4** na mgawanyo wa bajeti kisekta ni **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 4: Sura ya Bajeti ya Mwaka 2023/24**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Shilingi Milioni** |
| | **Mapato** | **2023/24** | |
| **A.** | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | | **30,237,128** |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 26,725,409 | |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | 3,511,719 | |
| **B.** | **Mapato ya Halmashauri** | | **1,143,883** |
| **C.** | **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | | **5,466,215** |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | 2,184,134 | |
| | (ii) Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | 3,151,958 | |
| | (iii) Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | 130,123 | |
| **D.** | **Mikopo ya Kibiashara Ndani na Nje** | | **7,540,840** |
| | (i) Mikopo ya Nje | 2,100,464 | |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | 1,898,316 | |
| | (iii) Mikopo ya Ndani- Rollover | 3,542,061 | |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | | **44,388,067** |
| | | | |
| | **Matumizi** | | |
| **E.** | **Matumizi ya Kawaida** | | **30,310,847** |
| | (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | | 12,771,533 |
| | -Malipo ya Riba Ndani | 2,799,374 | |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | 3,542,061 | |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | 2,763,947 | |
| | -Malipo ya Riba Nje | 1,364,377 | |
| | -Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | 1,710,608 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | 591,167 | |
| | (ii) Mishahara | | 10,882,126 |
| | (iii) Matumizi Mengineyo (OC) | | 5,518,819 |
| | -Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | 200,000 | |
| | -Matumizi ya Halmashauri (own source) | 689,468 | |
| | -Matumizi mengineyo | 4,629,351 | |
| | (iv) Ruzuku ya Maendeleo | | 1,138,369 |
| | -Elimu Msingi na Sekondari Bila Ada | 399,642 | |
| | -Mikopo ya Wanafunzi Elimu ya Juu | 738,727 | |
| | | | |
| **F.** | **Matumizi ya Maendeleo** | | **14,077,220** |
| | (i) Fedha za Ndani | | 10,795,139 |
| | -Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | 528,000 | |
| | -Ugharamiaji wa SGR | 1,113,000 | |
| | -Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere | 1,500,000 | |
| | -Matumizi ya Halmashauri | 454,415 | |
| | -Miradi mingine | 7,199,724 | |
| | (ii) Fedha za Nje | | 3,282,081 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | | **44,388,067** |
| | **NAKISI YA BAJETI (kama asilimia ya Pato la Taifa)** | | **2.7%** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Jedwali Na. 5: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta kwa Mwaka 2023/24**

| **SEKTA** | | **2022/23** | **2023/24** |
|---|---|---|---|
| | | **Shilingi Bilioni** | |
| Elimu | | 5,684.7 | 5,951.6 |
| Afya | | 2,149.1 | 2,435.5 |
| Maendeleo ya Uchumi | Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano | 3,929.2 | 3,843.2 |
| | Kilimo | 1,216.2 | 1,465.2 |
| | Viwanda na Biashara | 282.9 | 324.2 |
| | Nishati | 2,905.9 | 3,048.6 |
| | Madini | 83.3 | 89.3 |
| | Maliasili, Utalii na Mazingira | 615.4 | 637.1 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Vijana, Kazi na Maendeleo ya Kukuza Ujuzi | 31.2 | 20.3 |
| Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii | Maji | 723.9 | 766.2 |
| | Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 118.6 | 173.3 |
| | Maendeleo ya Jamii | 455.2 | 369.8 |
| | Habari, Michezo na Utamaduni | 35.4 | 35.4 |
| Hifadhi ya Jamii | | 2,244.2 | 2,345.5 |
| Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama | | 4,208.0 | 4,682.3 |
| Huduma za Utawala | Mihimili ya Utawala, Usimamizi wa Mapato na Matumizi, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 10,581.4 | 11,894.6 |
| | Deni la Taifa | 6,216.0 | 6,306.0 |
| **JUMLA** | | **41,480.6** | **44,388.1** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti**

**161. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2023/24 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali ikiwemo: mabadiliko ya kiwango cha mfumuko wa bei; mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha na riba katika masoko ya fedha ndani na nje ya nchi; madeni sanjari; na mabadiliko ya sera za kibajeti, misaada na mikopo. Vihatarishi vingine ni pamoja na: mabadiliko ya tabianchi; na majanga asilia kama vile matetemeko ya ardhi na magonjwa ya mlipuko.

**162. Mheshimiwa Spika**, athari zinazoweza kujitokeza endapo vihatarishi vya mwenendo wa uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti vitatokea ni pamoja na: kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato; kasi ndogo ya

utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za bidhaa, malighafi, huduma na utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali; kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha; kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; uharibifu wa miundombinu; na kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma.

**163. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24, Serikali itaendelea na mikakati na afua za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na: kusimamia miongozo ya kubaini vihatarishi serikalini katika utekelezaji wa mipango, mikakati na sera mbalimbali; kuimarisha ulinzi, usalama na utawala bora; kuimarisha mikakati ya Serikali katika kuongeza mapato; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuongeza uzalishaji pamoja na uuzaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali; kusimamia sera za fedha na bajeti kwa weledi; na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na nchi rafiki pamoja na Washirika wa Maendeleo.

## VIII. HITIMISHO

**164. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 inayosisitiza: mapinduzi ya uchumi kwa maendeleo ya watu; upatikanaji wa huduma bora za jamii; uwepo wa utawala bora, utawala wa sheria na demokrasia; pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, hususan katika diplomasia ya siasa na uchumi.

**165. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24, itaendeleza juhudi za Serikali katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Katika kufikia malengo hayo, kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zilizopo na kufanya kazi kwa bidii. Ni matumaini yangu kuwa,

utekelezaji madhubuti wa bajeti hii utachochea ukuaji wa uchumi pamoja na kuwaletea wananchi maendeleo yaliyokusudiwa. Hivyo, niwaombe wananchi wenzangu kutekeleza wajibu wetu wa kulipa kodi stahiki kwa hiari pamoja na kutoa na kudai risiti ya EFD pindi tunapofanya mauzo/ununuzi wa bidhaa na huduma ili kuhakikisha kuwa Serikali inaongeza mapato kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti.

**166. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Sisi sote ni mashahidi kuwa Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuwa chaguo namba moja kwa watanzania hasa ikizingatiwa kuwa ndio chama pekee chenye nia ya dhati ya kuleta maendeleo nchini. Waheshimiwa Wabunge, ukweli ni kuwa kila mtanzania anapozaliwa anakuwa mwana CCM. Aidha, tunaendelea kuwashuruku wale wote wa vyama vingine kwa mioyo yao ya upendo kwa kuendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020.

**167. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu wakati wa Hotuba yangu leo asubuhi, Serikali imeanza mchakato wa maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais ni muumini wa uongozi shirikishi, hivyo ameelekeza kuwa ni lazima Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ibebe maono ya wananchi wote. Kwa msingi huo, niendelee kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge kushiriki na kuwahamasisha wananchi katika majimbo yetu kutoa ushirikiano kwa timu za wataalamu zitakazokuwa zinazunguka kukusanya maoni.

**168. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii tena kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kwa uongozi wake bora na thabiti wenye mafanikio makubwa, hususan katika kuleta mageuzi ya kiuchumi pamoja na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kikanda na kimataifa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. **HAKIKA MAMA APEWE MAUA YAKE!** Nitoe wito kwetu sote tuendelee kumpa ushirikiano ili aendelee

kutuongoza vema na kutuheshimisha ndani na nje ya Bara la Afrika.

**169. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi makini, weledi na jitihada zao za kuhakikisha wakati wote wanatanguliza mbele maslahi ya Taifa letu. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali kwa umahiri mkubwa. Vilevile, kwa namna ya pekee, nimpongeze Komredi Daniel Godfrey Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa utendaji wake uliotukuka katika kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi CCM ya Mwaka 2020.

**170. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii ya kipekee kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa kuliongoza Bunge kwa hekima na umahiri mkubwa. Nimpongeze pia Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa namna ambavyo ameendelea kukusaidia katika kusimamia shughuli za Bunge. Kadhalika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jaji Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuongoza Muhimili wa Mahakama.

**171. Mheshimiwa Spika**, kipekee niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa uzalendo na utumishi wao uliotukuka. Naomba niwataje, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Jacob John Mkunda; Inspekta Jenerali wa Polisi, Camilius Wambura; Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John William Masunga; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Said Hussein Masoro; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, CP Salum R. Hamduni na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas James Lyimo. Aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende kwa kazi zao nzuri za kuwatumikia wananchi katika maeneo yao.

**172. Mheshimiwa Spika**, niwapongeze Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge lako Tukufu. Nawapongeza sana na kuwatakia majukumu mema ya kuliongoza Bunge. Aidha, niipongeze Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa umakini mkubwa wa kupitia, kuchambua na kushauri wakati wote wa maandalizi ya Bajeti hii.

**173. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali na sekta binafsi kwa michango waliyotoa ili kukamilisha Bajeti hii. Kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru viongozi na waumini wa dini zote kwa kuendelea kuliombea Taifa letu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi na waumini wa dini zote kuendelea kumuombea Rais wetu pamoja na viongozi wote wa Serikali ya Awamu ya Sita. Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema, hekima, unyenyekevu na dhamira njema katika utekelezaji wa majukumu yao.

**174. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Mbunge wa Jimbo la Kojani, kwa ushirikiano anaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kipekee, nimpongeze na kumshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu, kwa usimamizi wa kazi za kila siku za Wizara na uratibu mzuri wa maandalizi ya Bajeti. Ninawashukuru pia wakuu wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango; Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara; pamoja na watumishi wote wa wizara na

taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalamu na umahiri na hivyo, kuwezesha Wizara ya Fedha na Mipango kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

**175. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali, nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa ushirikiano mzuri na kuwa chachu katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kusaidia Taifa kuendelea kurejea katika hali ya uchumi himilivu kutokana na athari za UVIKO -19, mabadiliko ya tabianchi na vita kati ya Urusi na Ukraine.

**176. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/24, Washirika wa Maendeleo walioahidi kuchangia Bajeti ya Serikali ni pamoja na nchi wahisani za: Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Mashirika ya Kimataifa yaliyoahidi kuchangia ni pamoja na: Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Katika Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa, Mfuko wa Mazingira Duniani, Mfuko wa GRMF, Umoja wa Mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake, Umoja wa Ulaya na Shirikisho la GAVI.

**177. Mheshimiwa Spika**, ni matarajio yetu kuwa, fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 zitapatikana kama zilivyoahidiwa na zitatumika kwa kuzingatia vipaumbele na miongozo ya Serikali pamoja na mila, desturi na tamaduni za nchi yetu. Aidha, nitoe rai kwa sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo.

**178. Mheshimiwa Spika**, nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuzipongeza timu zetu za mpira wa miguu za Yanga na Simba kwa kutuwakilisha vema katika michuano ya kimataifa. Ndugu zetu wa Simba walituwakilisha kwenye mashindano ya Klabu Bingwa Afrika hadi kufikia hatua ya robo

fainali ya mashindano hayo, hongera sana!! Aidha, kwa namna ya pekee, niipongeze Timu ya Wananchi (Yanga) kwa kuweka historia ya kufanikiwa kufika fainali za Kombe la Shirikisho Afrika. Kwa hakika, timu hizi zimeliheshimisha Taifa letu katika nyanja za kimataifa. Mafanikio hayo ya timu za Yanga na Simba yamepandisha hadhi ya Taifa letu katika viwango vya mpira wa miguu vinavyosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika – CAF. Timu nyingine pia ziige kutoka Yanga kwani katika mwaka huu na mwaka jana timu ya Yanga imechukua vikombe vyote vilivyoandaliwa hapa nchini. Vilevile, naomba kutambua mchango na hamasa ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa kuendelea kutoa motisha kwa timu zetu za michezo pale zinapofanya vizuri kimataifa.

**179. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuwasilisha hotuba hii. Kwa moyo wa dhati napenda kuishukuru familia yangu, mke wangu kipenzi **Bi. Neema Nchemba** na watoto wetu, kwa kuendelea kunitia moyo na kuniombea wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya ubunge. Nawashukuru wote kwa kunisikiliza. ***Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania!***

**180. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa wasilisho hili. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi hizo kwa Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho alilolifanya la makadirio ya mapato na matumizi kwa Serikali kwa Mwaka wa Fedha

2023/2024. Sasa pamoja na kwamba hoja imeungwa mkono mnafahamu utaratibu wetu hili jambo mtahojiwa baadaye siku zinazokuja huko mbele baada ya kumaliza hatua zote kama tunavyotakiwa Kikanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengi ambao wamekuja siku ya leo kutuunga mkono kama Bunge kwa ajili ya kusikiliza hotuba hii muhimu sana katika mwaka wa fedha unaokuja. Nitumie fursa hii kumpongeza Waziri kwa wasilisho zuri lakini pia na Wasaidizi wake Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na tunawatakia kwa kweli kila la kheri huko mbele kadri Wabunge watakavyokuwa wanawashauri na kuwaambia mambo kadhaa wa kadha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siku ya leo makofi yalikuwa ya tofauti kidogo na mimi niliyaruhusu kwa sababu ya mambo mazuri yalikuwa yanasomwa kwenye hotuba hii, lakini nadhani tulishakubaliana ushangiliaji wetu wa Kibunge ni upi. Huu mwingine kidogo huwa unaleta shida inapotokea Waziri anaendelea kusoma ukiwa unashangilia. Mkienda kusikiliza ni kwamba unakuwa unaingiliana kwa sababu inatoka sauti kwa ukali ni tofauti na meza. Kwa hiyo, kwa leo hilo tuliache lipite lakini huko mbele kwa sababu mambo mengi sana ya kushangilia niwaombe tuzingatie ule utaratibu ili tuache yule anayekuwa anatoa hoja aendelee kusikika kama akiendelea bila kusimama kusubiri makofi yaishe. Kwa hiyo, yale makofi ya kupiga mwenyewe, yale kidogo na yenyewe yanatoa sauti inaenda mbali sana, kwa hiyo inaingiliana na yule anayekuwa anazungumza na vivyo hivyo kigelegele kinaingilia yule anayekuwa anazungumza. Kwa hiyo, kama tulivyokuwa tumekubaliana tupige kigelegele cha makofi yale tuliokubaliana ya Kibunge ya kupiga meza.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na tangazo la wageni ambao wapo hapa na tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika. Kwanza tutaanza na Dkt. James Andilile ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *EWURA*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo ninao wageni wengi sana kwa hiyo tutajitahidi kwenda kwa haraka. Ninao wageni

wengine watano kutoka Kanisa la *TAG* wakimwakilisha Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Dkt. Barnabas Mtokambali na hawa ni Mchungaji Joseph Gabriel Marwa ambaye ni Katibu Mkuu wa Kanisa la *TAG*, karibu sana. Yupo pia Mchungaji Samson Simon Mkuyu ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Kanisa la *TAG*, karibu sana. Yupo pia Mchungaji Sadiki Herzon ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Vijana *CASFETA* Taifa Makao Makuu ya Kanisa la *TAG*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni Ndugu Patricia Mhando ambaye ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Kampuni ya Sigara Tanzania *(TCC);* yupo Ndugu Spencer Lameck ambaye ni mwakilishi kutoka *Wasafi Media;* na pia yupo Ndugu Ally Abdallah, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Bunge. Kwanza ni Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, karibu sana. Karibu sana Katibu Mkuu Kiongozi; tunaye pia Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu na Mzee wa Dodoma; na pia tunaye Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, ambaye ni Spika Mstaafu. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Profesa Elisante Ole Gabriel ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania; tunaye Jenerali Jacob John Mkunda ambaye ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania; tunaye pia Inspekta Jenerali Camillus Wambura ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Said Hussein Massoro ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; tunaye Kamishna Jenerali Mzee Ramadhan Nyamka ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Magereza; tunaye pia Kamishna Jenerali John William Masunga, ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; tunaye Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, James Mwanjokile ambaye ni mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; na pia tunaye Ndugu Neema Mwakalyelye ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Ndugu Alethas Lyimo ambaye ni Kamishna wa Kupambana na Dawa za Kulevya; tunaye pia Dkt. Natu Mwamba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango; tunaye Dkt. Jim James Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge; tunaye Dkt. Philis Nyimbi ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, anamwakilisha Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara; tunaye Ndugu Fadhili Maganya ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Chama cha Mapinduzi Taifa; na pia tunaye Dkt. Edmund Mndolwa ambaye ni Mwenyekiti Mstaafu wa Jumuiya ya Wazazi Taifa akimwakilisha Katibu Mkuu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu George Francis Mlawa, ambaye ni Katibu wa Bunge Mstaafu; tunaye Mheshimiwa Jaji Mstaafu, Kipenka Msemembo Mussa ambaye ni Katibu wa Bunge Mstaafu; na pia tunaye Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge Mstaafu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba ambaye ni Gavana wa Benki Kuu; tunaye Ndugu Charles Kichere ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; tunaye Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa *TRA;* tunaye Mheshimiwa Jaji wa Rufaa ambaye ni Jacobs M. Mwambegele, huyu ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi; tunaye pia Ndugu Neema Mwigulu Nchemba ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Karibuni sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao hawakupata nafasi kwenye Jukwaa la Spika, tutaanza na Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali. Kwanza tunaye Ndugu Majura Mululi Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu; tunaye Ndugu Xavia Daudi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; tunaye Dkt. Tausi Mbaga Kida ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Uwekezaji; tunaye Ndugu Adolf Hyasinth Ndunguru ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); na pia tunaye Ndugu Mary Ngeleja Maganga ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile tunaye Mheshimiwa Balozi Samwel William Shelukindo ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; tunaye Ndugu Gerald Geofrey Mweli ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo; tunaye Ndugu Kaspar Kaspar Mmuya ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani; tunaye Profesa Riziki Sailas Shemdoe, Katibu Mkuu Mifugo na Uvuvi; tunaye Dkt. Hassan Said Abbas ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii; na pia tunaye Mhandisi Felchesmi Mramba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Ndugu Kheri Abdul Mahimbali ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Madini; tunaye Mheshimiwa Balozi Mhandisi Aisha Amour ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; tunaye Dkt. Hashil Abdallah ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; tunaye Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya; tunaye pia Dkt. Franklyne Rwezimula ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; tunaye, (eeh, hiki cheo ndiyo sijaelewa, lakini najua ni daktari, kwa hiyo, acha nimwite hiki cha udaktari. Kingine kilichoandikwa hapa mtaniwia radhi) Dkt. John Anthony Jingu ambaye ni Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Maji; tunaye Ndugu Said Yakub ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; tunaye Ndugu Selestine Gervas Kakele ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na pia tunaye Ndugu Anderson Mutatembwa ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile tunaye Ndugu Jenifa Omolo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina; tunaye Ndugu Lawrence Mafuru ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Uchumi; tunaye Ndugu Amina Shaaban, Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma; na pia tunaye Ndugu Rogatus

Matavila ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Mteule TAMISEMI. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Sasa hawa inabidi nisome Kiingereza kilichoandikwa hapa ili wajue wao ndiyo wanaotajwa. Haya tunaye *His Excellency Ahmada El Badaoui Mohamed (Ambassador of the Union of Comoros and Dean of the Diplomatic Corps), thank you so much for coming. (Makofi)*

Tunaye pia *His Excellency Sandro De Oliveira (Ambassador of the Republic of Angola);* tunaye pia *Her Excellency Mary O'Neill (Ambassador of the Republic of Ireland);* Tunaye pia *His Excellency Mathew Jere (Zambia High Commissioner);* pia tunaye *Madam Debora Mitawa (Deputy High Commissioner Republic of Malawi). Thank you for coming. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Epiphanie Buzizi *(Charge d'Affaires for the Republic of Rwanda), thank you for coming; we also have Olukemi Williams (Development Director of the United Kingdom), thank you so much;* Tunaye pia *Mr. Sylivester Ernest (Senior Political Officer of the United Kingdom); we also have Mr. Sunday John (Economist United Kingdom); we also have Mr. Narender Kumar (Commercial Attache' of the Republic of India); we also have Dr. Rangarirai Gladys Chikwizo (Counselor Republic of Zimbabwe); we also have Dr. Olav Lundstol (Country Economist Royal Norwegian Embassy); we also have Priva Clemence (Senior Advisor Royal Norwegian Embassy); we also have Miss Agnes Keneth (Political Assistant United States of America); we also have Miss Stella Manda (UN Women); and we also have Miss Asnath Gerson Abraham (Liaison Associate UNHCR). Thank you so much for coming. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, *we also have Mr. John George Ng'ariba (Liaison Officer UNICEF Dodoma); we also have Dr. Victor Bakengesa (Program Officer UNFPA); we also have Dr. Patricia Laverley (Resident Representative African Development Bank); we also have Mr. Jens Reinke (Resident Representative IMF); we also have Mr. Chelaus Rutachuruwa (Senior Economist IMF); and we*

*also have Mr. Dhlomo Imieka (Counselor South African High Commission)*. *Thank you for coming. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia viongozi wa dini ambao wameungana na sisi siku ya leo. Tutaanza na Sheihe Kisusu Mvumbo ambaye ni Mwakilishi wa Mufti Mkuu wa Tanzania; tunaye pia Askofu Dkt. Fredrick Shoo ambaye ni Askofu wa KKKT na Mwenyekiti wa *CCT;* tunaye pia Askofu Christian Ndosa ambaye ni Mwakilishi wa Askofu Mkuu wa KKKT Dodoma; tunaye pia Askofu Raphael Maligite ambaye ni Mwakilishi wa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Mkoa wa Dodoma; tunaye pia Sheikh Mustafa Rajabu ambaye ni Shehe Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Ndugu John Maliga ambaye ni Mwakilishi Kiongozi Mkuu wa Kihindu Tanzania; tunao pia Askofu Dkt. Yohana Masinga ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa la *FREDESIAN* Dodoma; tunaye pia Askofu Julias Nassari ambaye ni Mwakilishi wa Askofu Mkuu wa *EAGT* Dodoma; Tunaye Mchungaji Timotheo Holela ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la *ELCT* Dodoma; tunaye Askofu Yussuf Mtolela ambaye ni Mwenyekiti wa *CCT* Dodoma; Tunaye Mhandisi Robert Kitunde ambaye ni Katibu Mkuu wa KKKT. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Maofisa kutoka Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Tunaye Ndugu Benjamin Mashauri ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa; yupo pia Ndugu Salhina Mkumba ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Umma; pia yupo Ndugu Wendi Masoy ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu; na pia yupo Ndugu Jonas Kisiri ambaye ni Afisa Masuuli Ofisi ya *CAG*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine walioko Jukwaa la upande wa kushoto. Tunaye Jaji Dkt. Fatma Khalfan ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu, anamwakilisha Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Dodoma; tunaye Kanali Jonas Kateka Simtoe ambaye ni *Base Commander* JWTZ Dodoma; tunaye pia Mheshimiwa Jabiri Shekimweri ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini; tunaye Ndugu Methuselah Ntonda ambaye ni

*Regional Security Officer;* tunaye pia Ndugu Bertha Joseph Minde ambaye ni *Regional Prison Officer;* na pia tunaye Ndugu Julishael Mfinanga ambaye ni *Regional Fire and Rescue Force Officer*. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Bwana Nehemia Mchechu ambaye ni Msajili wa Hazina; Tunaye pia Ndugu Eliakimu Masu ambaye ni Mtendaji Mkuu wa *PPRA;* tunaye pia Ndugu Abdulmajid Nsekela ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa *CRDB Bank;* tunaye Ndugu Theobald Sabi ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NBC;* tunaye pia Ndugu Juma Kimori ambaye ni Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NMB;* tunaye pia Ndugu Gilead John ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *TIC;* tunaye pia Ndugu Godfrey Nyaisa ambaye ni Mtendaji Mkuu wa *BRELA;* na pia tunaye Ndugu Raphael Maganga ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Ndugu Beatrice Mussa Lupi, ambaye ni Mkurugenzi wa Fedha wa *PSSSF* na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu; tunaye Ndugu Alfred Phillemon Matuntera ambaye ni Meneja wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini *TPA* akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji; tunaye Ndugu Boniphas Shoo ambaye ni Meneja Kanda ya Kati Dodoma *TCRA* akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa *TCRA;* yupo Ndugu Lilian M. Mbassy ambaye ni Kaimu Mtendaji Mkuu wa *Tanzania Development Bank* (hii *Tanzania Development Bank* hapa kwenye mabano imeandikwa "*TID Development*", kwa hiyo, nadhani imekuwa na jina zuri). Haya, tunaye Ndugu Frank Nyabundege ambaye ni Mtendaji Mkuu wa *TADB*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Ndugu Esther Mang'enya ambaye Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya AZANIA, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Masanja Kadogosa ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *TRC*, karibu sana. Tunaye pia Mheshimiwa Mhandisi Ladislaus Matindi Mkurugenzi Mkuu *ATCL*, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Edmund Mkwawa Rais wa *TCCIA*, karibu sana. Yuko pia Prof. Yohana Msanjila Mkuu wa Chuo cha St. John's, karibu sana. Yuko pia Ndugu Maiko Salali Hosea Mwenyekiti wa watu wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma, ahsante sana. Yupo pia

Ndugu Shaban Kissu Mtendaji Mkuu wa Vyombo vya Habari vya Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana. Yuko pia Ndugu Ramadhan Mkoma ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Uhuru Media, karibu sana. Yuko pia Ndugu Sarah Kibonde Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari Serikalini TAGCO karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia watendaji 60 wa Wizara ya Fedha na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Wageni hao ni Ndugu Godwin Semunyu ambaye ni Mkuu wa Mahusiano ya Jumla *NBC Bank*. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Theresia Umbela ambaye ni Meneja Tawi la Bunge *NBC*. Tunaye Ndugu Azzah Mzava ambaye ni Meneja Uhusiano Taasisi za Serikali *NBC Bank,* tunaye Ndugu David Raymond Mkuu wa Masoko, *NBC Bank*. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Happiness Kizigira Meneja Kanda ya Dodoma wa *NBC*. Tunaye pia Ndugu Linlay Kapya ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Serikali *NBC Bank*. Tunaye pia Ndugu Shani Kinswaga ambaye ni Mkuu wa Idara ya Fedha *Exim Bank.* Tunaye Ndugu Stanley Kafu Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano *Exim Bank*. Tunaye pia Ndugu Derrick Lugemala ambaye ni Meneja Mkuu wa Fedha *BOA Bank*. Tunaye pia Ndugu Nandi Mwiyombela ambaye ni Mkuu wa Masoko *Bank of Africa. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu George Sawe ambaye anatoka Chama cha Madalali wa Soko la Hisa Tanzania. Yupo Pia Ndugu Godfrey Malauri ambaye anatoka Chama cha Madalali wa Soko la Hisa Tanzania. Yupo pia Ndugu George Shumbusho ambaye anatoka Chama cha Madalali wa Soko la Hisa Tanzania. Yupo pia Ndugu Sigfried Kuwite ambaye anatoka Chama cha Madalali wa Soko la Hisa Tanzania. Yupo pia Ndugu Khalifa Gwando ambaye ni Meneja Uhusiano Citibank. Yupo pia Ndugu Juma Kimori nadhani Juma Kimori nilishamtambulisha huyu anatoka *NMB Bank* anamwakilisha pia Mtendaji Mkuu wa *NMB Bank*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Vicky Bishubo ambaye ni Mkuu wa Huduma za Benki kwa Serikali *NMB Bank*.

Yupo pia Dkt. Ally Laai ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi *CRDB Bank*, karibu sana. Yuko pia Ndugu Fredrick Nshekanabo ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Fedha *CRDB Bank*. Yuko pia Ndugu Celicius Kizitto *Branch Manager DTB* Dodoma. Yuko pia Ndugu Brayson Tarimo Kaimu Meneja wa Kanda *NMB*. Yupo pia Ndugu Grace Matemu Meneja wa Tawi la Bunge *NMB*, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Enna Victor ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakaguzi wa Ndani. Yuko pia Ndugu Jonathan Ngoma ambaye ni Mjumbe Bodi ya Wakaguzi wa Ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado nimesimama yuko Ndugu Enna Victor ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakaguzi wa Ndani, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Jonathan Ngoma ambaye ni Mjumbe Bodi ya Wakaguzi wa Ndani. Yupo pia Ndugu Vulfrida Mahalu ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya *KLNT*. Yuko pia Daktari Anthony Chamungwana ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya *KLNT*. Yupo pia Ndugu Boma Raballa ambaye ni Afisa Mkuu wa Biashara *CRDB Bank. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza na simu mkiwa humu Bungeni tafadhali. Yupo Ndugu Bruce Mwile ambaye ni Afisa Mkuu Mwendeshaji *CRDB Bank*. Yupo pia Ndugu Bonventura Paul ambaye ni Mkurugenzi wa Matawi ya *CRDB Bank* Tanzania, karibu sana. Yupo pia Ndugu Grace Adam Meneja wa Tawi la Bunge *CRDB Bank* ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Chabu Mishwaro ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kati *CRDB Bank*, ahsante sana. Yupo pia Ndugu Nathan Belete ambaye ni *Country Director World Bank,* haya ahsante sana. Yupo Ndugu Salum Nasor ambaye ni *Public Affairs and Communication Director,* ahsante sana. Yupo pia Ndugu Rogathe Loakaki Afisa Program Sera na Ujenzi wa Nguvu za Pamoja *TGNP* karibu sana. Yupo pia Ndugu Max Rugaimukamu ambaye ni Meneja Miradi Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF*). *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa orodha ya ziada hapa ya wageni wengine ambao tuko nao hapa Bungeni. Wageni wengine ambao tuko nao hapa Bungeni kuna mgeni wetu mwingine anaitwa Martha Mlata huyu ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia nadhani Katibu Mkuu wa KKKT nilishamtangaza pengine kama haikusika. Katibu Mkuu nadhani nimekutangaza siyo? Haya ahsante sana. Yupo pia Samatha Mohamed sijaambiwa cheo chake, karibu sana. Yupo pia Emilian Fanuel ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Iramba karibu sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni tulionao siku hii muhimu sana hapa Bungeni na tunawakaribisha sana. Ninalo tangazo moja hapa nimeletewa taarifa kwamba tunaye pia Balozi wa Kenya nchini Tanzania na huyu ni Mheshimiwa Balozi Isaac Njenga, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu tunawakaribisha sana Bungeni na ni dhahiri nafasi zingekuwa zinatosha tungeweza kuwaalika watu wengi zaidi lakini ninyi mmewawakilisha watanzania wote ambao wako nje ya hapa. Pia kwa upande wa mabalozi na wageni wetu wengine kutoka mashirika mbalimbali wamewawakilisha wadau wetu mbalimbali ambao tunashirikiana nao katika maendeleo ya nchi yetu.

Ninalo tangazo kwa Kamati ya Maandalizi ya Bunge Bonanza. Mnatangaziwa kwamba siku ya tarehe 24 Juni, 2023 kutakuwa na Tamasha la pili la michezo ya burudani lijulikanalo kama *Grand* Bunge Bonanza lenye kauli mbiu "Tupende Michezo Tujenge Taifa Letu." *(Makofi)*

Michezo mbalimbali ya ushindani na burudani itafanyika, michezo hiyo ni kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa meza, kutembea kwa haraka, kurusha vishale, kuvuta Kamba, kurusha tufe, riadha, kukimbia na gunia, mchezo wa rede, mchezo wa bao, mchezo wa karata, kufukuza kuku na kushindana kupenya kwenye

mapipa. Mgeni rasmi katika tamasha hilo anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bonanza hili linadhaminiwa na Benki ya *CRDB* ahsanteni sana. Kwa hivyo nitumie fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa *CRDB Bank* madamu wako hapa yupo Mwenyekiti pia yupo Mtendaji Mkuu wa Benki hii tunawashukuru sana.

Sasa tangazo linaendelea asubuhi bonanza hili litafanyika kuanzia saa kumi na mbili alfajiri katika Shule ya Sekondari ya John Merlini iliyoko Miyuji Jijini Dodoma. Jioni kutakuwa na tafrija itakayofanyika katika viwanja vya Bunge ambako kutakuwa na mchapalo na burudani nyingine ambazo kwa kweli hapa zimetajwa nyingi kweli tutajichagulia zile ambazo tunazitaka na zikiwepo na zile anazofanyaga Mheshimiwa Ally King nazo zitakuwepo naona hapa mambo mazuri, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia nimeambiwa kuna medali lakini sasa hata nikionesha hapa sina hakika itaonwa lakini kuna medali nimeletewa hapa. Sasa inabidi niifungue kwa sababu ililetwa kwenye bahasha na sasa hivi watu wamegundua kuanzisha mambo. Tangia *bundle* lishuke bei basi watu wanaanzisha tu mambo, maana *bundle* lake na simu yake kwa hiyo usimseme. Haya kwa hiyo kuna medali hapa imeandikwa Bunge la Tanzania lakini *Grand* Bunge Bonanza 2023. Kwa hiyo, wale wenye kushindana tutakuwa tukishindana, wengine wale wa kushiriki na wenyewe watapewa medali za ushiriki. Kwa hiyo, wengine watapewa za ushiriki na za kushinda michezo kwa hiyo wasiwe na wasiwasi na inategemea umeshiriki kwenye mchezo gani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa sababu kwa utaratibu wetu tutaendelea wiki ijayo kwa leo tumemsikiliza Mheshimiwa Waziri na sasa kesho kwa utaratibu ule ule, tutakuwa na nafasi ya kutafakari na kusoma kwa kina bajeti hii na mapendekezo haya yaliyoletwa kwetu ili tuyapitishe ama mengine tuyaseme hivi na vile basi kesho ni nafasi yetu ya kusoma.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.52 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu Tarehe 19 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*